# Nipashe

Jumanne Novemba 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581144

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

JACKPOT BABA LAO!
TZS. 412,613,570
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mbunge** amshtukia msimamizi wa mradi kituo cha afya kutoa zabuni kwa mkewe

UKURASA 8



Nipashe TESA

Jumanne Novemba 29, 2022 · TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

MZURI ISSA ALI
Mwanahabari aliyeacha kazi Ikulu kwenda kutetea wanawake, watoto
Ukurasa 15

Mtaalamu wa saikolojia ataja umri sahihi kuanza kumfundisha mtoto
Ukurasa 17

ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

SIKU 16 KUPINGA UKATILI KIJINSIA
MA-DC wanapopambana kumchomoa binti mikononi mwa 'mwanaume' tapeli
• Alimtorosha shuleni kumuoa, arudishwa darasani

WAKUU wa Wilaya, Jasinta Mboneko wa Shinyanga na Tanganyika, Salehe Mhando, wameandika historia kwa kushiriki na kufanikisha kumwokoa binti, aliyetoroshwa siku chache kabla ya kufanya mtihani wa kidato cha pili.

Ni msichana wa Sekondari ya Solwa wilayani Shinyanga (jina tunalo), anayeeleza kuwa Oktoba 28, mwaka huu, alinusurika kukwama kufanya mtihani wa kidato cha pili, baada ya kutoroshwa kwenda Mpanda mkoani Katavi kuozwa.

Akiwa na miaka 16, anaelezea tukio hilo, akisema anapenda shule, lakini kutokana na sekondari anayosoma kuwa mbali alirubuniwa akaingia kwenye mtego na kisha kutoroshwa kwenda kuolewa.

Anaelezea kuwa siku zote anatumia baiskeli kwenda shule iliyoko kilomita 20 na baiskeli inapoharibika anashindwa kuitengeneza kutokana na kukosa fedha ndiyo sababu ya kukumbana na vishawishi vya wanaume wakimtaka kimapenzi.

"Nilikuwa nimekata tamaa kuendelea na msomo sababu ya kusoma mbali, japo napenda nisome," anasema akimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko kwa kumwokoa asiolewe.

"Ndoto zangu ni kuwa mwalimu, na sasa nakwenda kuzitimiza na nitasoma kwa bidii sababu naishi hapa shuleni," anaongeza.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Solwa, Leonard Adamu, anasema wanafunzi katika shule wana utoro kwa sababu ya kutembea umbali mrefu.

Akizungumzia binti aliyetoroshwa anasema walibaini mwanafunzi huyo wa kidato cha pili kutokuwapo shuleni wakati wakifanya maandalizi ya kuwapanga kwa ajili ya mitihani na walipomfuatilia ikagundulika kuwa ametoroshwa kwenda Mpanda.

Anasema baada ya kujua hilo, aliwasiliana na viongozi wa kata kisha taarifa hizo akapewa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta ili aongeze nguvu za kumwokoa mwanafunzi huyo arudi kufanya mtihani na kutimiza ndoto zake.

"Tunashukuru mwanafunzi aliokolewa kwa wakati na akafanya mtihani wake wa kidato cha pili," anasema Adamu.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anasema baada ya kupata taarifa za mwanafunzi huyo kutoroshwa kwenda kuozwa aliwasiliana na Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Salehe Mhando, ili kumfuatilia na kukamatwa lakini muoaji akakimbia.

Anasema juhudi zilifanikishwa na wasamaria wema waliowafikishia polisi taarifa na kwamba alikaa siku moja na ya pili akarudishwa shuleni. Na kwamba alipandishwa gari na kijana aliyemtorosha ambaye ametoroka.

"Nilipopewa taarifa tu juu ya mtoto huyu kuwa ametoroshwa, siku hiyo hiyo nilifanya mawasiliano ya haraka na tukawakamata na kumrudisha mtoto huyu haraka shuleni na akafanya mtihani," anasema Mkuu wa Wilaya.

CHINI YA UANGALIZI

"Mwanafunzi huyu kwa sasa yupo chini ya serikali na anaishi na mwalimu shuleni hapa, na haruhusiwi kwenda likizo kwa wazazi wake, bali wanatakiwa kuja hapa shuleni kumsalimia na nitamsimamia hadi afike chuo kikuu na kutimiza ndoto zake," anaongeza.

Anasema kutokana na tatizo la umbali mrefu wa shule tayari serikali imeshatoa Shilingi milioni 160 kwa ajili ya kujenga shule mpya yenye vyumba vya madarasa nane na itaanza kutoa elimu mwakani.

"Umbali mrefu ni changamoto unawakwamisha wanafunzi wa kike na ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha za kuanzisha shule mpya ya sekondari, ili wanafunzi wasome karibu," anaeleza Mkuu wa Wilaya.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Jasinta Mboneko akizungumza kwenye kongamano la masuala ya wanawake. PICHA: MAKTABA

INAENDELEA UK. 18

UKURASA 13

# Mtoto atoa ushahidi dhidi ya baba yake kesi ya mauaji

UKURASA 7



UKURASA 2

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi, wageni na wajumbe wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) kabla ya kufungua Mkutano wa 10 wa Jumuiya hiyo kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Upatikanaji wa maji Dar sasa uhakika, mradi mpya waiva

UKURASA 3



## Samia awapa mbinu wanawake kuimarika kiuchumi na uongozi

MICHEZO MGUNDA ATEMA CHECHE LIGI KUU BARA UK.32 KATUNI UK.6



Baadhi ya wanachama wa vikundi vya Vicoba katika Kata za Kipunguni, Chanika na Majohe, jijini Dar es Saalam, wakichambua mboga ili kuandaa chakula cha pamoja ikiwa ni sehemu ya kuimarisha umoja, baada ya kumaliza mafunzo ya jinsi ya kuendesha vikundi hivyo, yaliyoendeshwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia awapa mbinu wanawake kuimarika kiuchumi na uongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, amesema wanawake viongozi wanapaswa kuwa na uthubutu bila kuogopa kukosolewa kwa kuwa kiongozi kulaumiwa ni jambo la kawaida.

Rais Samia pia ameeleza kutoridhishwa na kasi ya kujiunga kwa wanachama wa UWT na uendeshaji wa miradi yake ya kiuchumi.

Akifungua jana Mkutano Mkuu wa 10 wa UWT unaolenga kufanya uchaguzi wa viongozi ngazi ya taifa, Rais Samia alisema wengi wanajifungia kwa kuendekeza dhana kwamba ni wanawake.

"Tunapokuwa kwenye vikao, hata kama una fikra ya maana unataka kuisema, unaangalia wanaosema kisha unajiambia 'aaah mimi mwanamke bwana, ngoja ninyamaze'.

"Unaogopa nini? Unaogopa kukosolewa, unaogopa kulaumiwa, unaogopa kuonekana vipi? Lakini usiposema na hilo jambo lisipotekelezeka na kama jambo zuri, umerudisha nyuma, ninaomba tuwe wathubutu, tusemeni, tendeni, ni uthubutu peke yake unaofanya taasisi zisonge mbele.

"Tusipokuwa wathubutu, tukiendelea kujifungia kisa wanawake, hatutakwenda na hata jumuiya haitakwenda. Twendeni tuthubutu, sio tu kusema lakini kufanya kuyasogelea mambo yalipo, unaliona jambo litakufaa, nenda muone mwambie ulilonalo muombe, muulize ukilipata linakwenda kukufaa.

"Tuthubutu na ndio maana tunasema mnapochaguana, basi tuweke watu wenye uthubutu wanaoweza kwenda na kufanya likawa haya mambo ya sitaki lawama au nilaumiwe hayatufikishi pahala, tunalaumiwa, kama viongozi lazima tulaumiwe tunajaribu huku, tunajaribu huku tunalaumiwa.

"Unaweka tozo kukuza mapato unalaumiwa, ukiona lawama nyingi unapunguza kidogo, unajaribu kwingine nini unalaumiwa, unatazama hali unarudi nyuma kidogo na ndiyo tunavyokwenda, tusingethubutu tusingekwenda," alisema.

Rais Samia pia aliwataka wanawake kuvunja makundi baada ya kumalizika kwa uchaguzi, akitamka: "Uchaguzi ukiisha twende tukavunje makundi kwenye jumuiya yetu, niwaombe sana sisi chama ndiyo wimbo wetu kila tunapomaliza uchaguzi, vunjeni makundi ingawa mengine yanakuwa magumu kuvunjika lakini kwa wanawake hakuna msiloliweza."

Pia aliwataka kutorubunika kuuza chama na kuvunja nguvu ya chama kwa kuwa ni kikubwa na kwa sasa hakijatokea kingine cha kukabidhiwa nchi.

Kuhusu kujiimarisha kiuchumi, Samia alisema kuna mambo kadhaa ambayo jumuiya inapaswa kuwekeza kwenye miradi mikubwa ili kupata nguvu kiuchumi.

Alisema mkoani Ruvuma kunachimbwa makaa ya mawe, hivyo wanapochimba hata chama kinachimba, hivyo kuna vumbi jingi linabaki na kuna teknolojia ya kutengeneza mkaa wa kupikia kutokana na vumbi hilo.

"Niliwahi kutoa pendekezo moja katika jumuiya yetu, hebu nendeni mkaangalie ule mradi, chama kinachimba, ninyi katumieni lile vumbi maana wanasayansi wapo, STAMICO (Shirika la Madini la Taifa) wapo, wameshafanya utafiti wa kutosha sasa Wizara ya Madini inakwenda kuzalisha huo mkaa wa mfano.

"Nendeni mkachukue huo mradi, kama ni mashine semeni tutahangaika tupate na utaalamu mfundishwe ili mzalishe mkaa," aliagiza.

Akizungumzia kuhusu wanachama, Samia alisema kuanzia mwaka 2017 hadi 2022, jumuiya hiyo imeingiza wanachama wapya 86,288, idadi ambayo alisema ni ndogo kwa jumuiya hiyo.

"Ukichukua idadi hiyo ukiigawa kwa mikoa 32 na kujua mikoa mengine ni midogo sana kama ile ya Zanzibar unapata wanachama 2,697 tu, sasa hii sio kazi nzuri sana," alisema.

Aliitaka UWT kusimamia misingi ya kuanzishwa kwake ikiwamo kukemea vikali vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watoto na kuhimiza wanawake kuzalisha chakula kwa wingi ili kukabiliana na njaa.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, aliwataka wanawake kushikamana kwa kuwa nguvu ya chama ni mshikamano na umoja, kutetea maslahi ya wanawake nchini kwa kuelewa sera za chama na mipango ya serikali na utekelezaji wake.

"Pale penye upungufu wa kinamama ni jukumu la UWT kufuatilia kukumbusha na kuhakikisha matakwa na matumaini ya kinamama yanafikiwa, jukumu kubwa mnalo la kuisemea serikali na chama," alisema.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema jumuiya hiyo ni kubwa na ina nguvu lakini kuna sehemu imejisahau kutokaa kwenye nafasi yake.

"Kwa sababu kwa nguvu tuliyonayo UWT kuna mahali tunaanza kujisahau, tunaacha kuwa viongozi wa jumuiya, tunajielekeza kuwa viongozi wa watu, hilo jambo linatengeneza changamoto kubwa ya uimara wa UWT na uimara wa nguzo ya wanawake, lazima tutambue chama hiki ni kikubwa kuliko mtu yeyote.

"Lazima tusimame kwenye nafasi yetu, turudi kwenye msingi wa chama chetu, lazima tujue siku zote chama kwanza mtu baadaye, huo ndio msingi wa chama," alisema.

## Serikali yamulika maeneo matatu yenye shida vita ya UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

SERIKALI imebainisha maeneo matatu ambayo bado ni tatizo katika mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI, ikiwataka wadau kuyapa kipaumbele katika mikakati yao.

Katika hotuba yake wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Kisayansi mjini hapa jana, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliyataja maeneo hayo kuwa ni pamoja na maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na tiba kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa naibu waziri huyo, eneo lingine ni makundi yaliyoko nyuma katika kufikiwa na huduma za VVU na UKIMWI akiyataja kuwa yanajumuisha wanaume, vijana na makundi maalumu yaliyo katika hatari kubwa ya maambukizi ya virusi hivyo.

"Ni matumaini yangu kuwa fursa hii itakuwa muhimu katika kuweka nguvu mpya kuhakikisha mafanikio yaliyokwishapatikana mpaka sasa yanaendelezwa na makundi yaliyoachwa nyuma yanafikiwa kwa haraka na kwa ufanisi zaidi ili kufikia malengo ya kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030," alisema.

Katambi alikumbusha kuwa kongamano hilo la kisayansi limekuwa likifanyika kwa miaka mingi tangu mwaka 2016 kama sehemu ya maadhimishio ya kuelekea Siku ya UKIMWI Duniani.

Alisema kuwa kupitia kongamano hilo, jumuiya ya wanasayansi inapata nafasi ya kuungana na jamii kubwa zaidi katika kutafakari na kubadilishana mawazo, uzoefu na mbinu mpya za kisayansi za kupambana na janga la UKIMWI.

"Kongamano la mwaka huu ni muhimu sana kwa kuwa dunia pamoja na taifa letu limeweka mwelekeo mpya wa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ambapo kwa pamoja tumeamua kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

"Ili kutekeleza adhma hiyo, dunia kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia UKIMWI (UNAIDS), imeandaa mkakati mpya wa kuelekea lengo hilo (Global AIDS Strategy 2021-2026). Nasi kama taifa tumeandaa mikakati mipya ya kitaifa na kisekta (Mkakati wa Taifa wa Sekta zote - NMSF V na Mkakati wa Sekta ya Afya - HSHSP V) ili kutekeleza azimio hilo," alisema.

Katambi alisema kongamano hilo linalofanyika chini ya kaulimbiu ya 'Imarisha Usawa', litatoa nafasi ya wadau kujadili mbinu mpya na namna bora ya kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI katika muktadha mpya.

"Nimefahamishwa kuwa kongamano hili la siku mbili, litahusisha wataalamu mbalimbali wakiwamo wanasayansi, watoa huduma za VVU na UKIMWI, wawakilishi mbalimbali wa jamii zinazotumia huduma hizo, wasimamizi na wadau wa maendeleo pamoja na wajumbe toka sekta mbalimbali.

Inatarajiwa jumla ya mawasilisho 26 yatatolewa kwa njia ya mhadhara na mengine mengi kama mchapisho. Mawasilisho yote yamegawanyika katika mada kuu nane yakilenga kutoa nafasi ya mijadala kuelekezwa katika maeneo makuu ya mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini.

"Kusikia mada ni jambo moja na kutekeleza maelekezo ya kisayansi ni jambo tofauti. Ninapenda kuwashauri kuwa, ili tuweze kufanya mageuzi katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI na kupata matokeo chanya, hatuna budi kuzingatia zaidi ushauri wa kisayansi.

"Ninawaomba wote tutakapomaliza kongamano hili kila mmoja wetu kupitia asasi yake kufanya mapitio ya pamoja ya jinsi mada zilizowasilishwa hapa zinaweza kuboresha utendaji kazi wao na kufanya marekebisho stahiki. "Ushirikiano kati ya asasi zinazotekeleza afua zinazofanana ni fursa muhimu ya kuanza kutekeleza mambo yale tuliyojifunza katika kongamano hili.

"Niwashukuru sana TACAIDS (Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI) kwa kunialika kuja kufungu kongamano hili muhimu na pia kuwapa pongezi wote kwa maandalizi mazuri ya tukio hili," alisema Katambi na kulifungua rasmi kongamano hilo.

Washiriki wa kongamano hilo walitoka taasisi mbalimbali zikiwamo wizara, TACAIDS, UNAIDS na watendaji wa ofisi za wilaya za Mkoa wa Lindi.

HABARI KITAIFA

# Kongamano uwekezaji sekta nyeti kufanyika nchini

**Na Maulid Mmbaga**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimeandaa kongamano maalum la kuhamasisha na kukuza uwekezaji na biashara kwenye sekta kipaumbele nchini.

Kongamano hilo linaloanza leo limeandaliwa kwa ushirikiano wa wizara, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo (UNDP) na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam Kaimu Mkurugenzi wa TIC, John Mnali, alisema lengo ni kuchochea kukua kwa uwekezaji katika sekta zenye mrengo wa maendeleo endelevu.

Alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kongamano hilo linalolenga kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizoko nchini zenye mrengo wa maendeleo endelevu kwa wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nchi mbalimbali duniani.

"Fursa zilizoko katika sekta za kipaumbele zenye mrengo wa maendeleo endelevu ni kilimo na chakula. Katika uwekezaji itahusisha usindikaji wa mboga na matunda, uzalishaji wa mafuta ya kula na uzalishaji wa bidhaa zitokananzo na ngozi," alisema na kuongeza:

"Eneo jingine ni nishati mbadala, umwagiliaji, umeme wa jua na mfumo wake, miundombinu itahusisha utengenezaji wa nyumba za bei nafuu, usindikaji wa taka ngumu na usafirishaji."

Aidha, katika sekta ya elimu uwekezaji utakuwa katika miundombinu ya elimu na huduma katika utalii.

Mnali alisema kuwa manufaa ya kongamano hilo linalotarajiwa kuhudhuriwa na wawekezaji wa kampuni zaidi ya 100 kwa njia ya mtandao, litasaidia kuitangaza Tanzania kama miongoni mwa maeneo yenye fursa za mazingira mazuri ya kibiashara kwa kampuni mbalimbali duniani.

Vile vile, kampuni za Tanzania zitapata fursa ya kuongea na kubwa zitakazohudhuria na kupata nafasi ya kufanya biashara pamoja na kuingia ubia katika uwekezaji.

Alisema katika jukwaa la uwekezaji kutakuwa na nafasi za wasilisho la fursa za uwekezaji zinazoendana na malengo endelevu ikiwamo miradi sita ya kuchakata mafuta ya kula, uendelezaji wa ukanda maalumu wa uwekezaji wa kilimo na mradi wa umeme wa jua wa Singida.

Mingine ni ujenzi wa miundombinu ya bwawa la maji la Farkwa, urejelezaji taka na nishati mbadala na maendeleo ya mtandao wa reli kwa huduma za treni za Dar es Salaam.

Mtaalamu kutoka UNDP, Emmanuel Nkko, alisema kongamano hilo litakuwa ni hitimisho la kazi ya utafiti iliyofanyika miezi 18 iliyopita ya kuchambua na kutumia uwekezaji katika kusukuma gurudumu la maendeleo endelevu.

"Sote tunajua Tanzania iko kwenye utekelezaji wa malengo endelevu, na ikiwa ni mwanachama wa umoja wa mataifa, sasa wakati serikali ikiendelea kuchochea shughuli za kimaendeleo kwa taifa na mtu mmoja mmoja, nafikiri ni wakati muafaka wa sekta binafsi kushiriki kupitia uwekezaji," alisema na kuongeza:

"Utafiti umeainisha baadhi ya sekta na fursa ambazo mkurugenzi ameziorodhesha, tunaamini kwamba uwekezaji ukifanywa kwenye hizo sekta utagusa maisha ya wengi na kusaidia nchi kufikia malengo endelevu."



Msimamizi Mwenza wa Taasisi ya KPMG Tanzania, Alexander Njombe (kushoto), akimkabidhi Tuzo ya CEO Bora wa mwaka 2022 kutoka kundi la Taasisi za Serikali, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Upatikanaji maji Dar waimarishwa

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imesema kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la Kidunda na mradi mpya wa maji kutoka Rufiji, utafanya upatikanaji maji kuwa lita milioni 750 kwa siku Dar es Salaam na Pwani.

Jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya upatikanaji wa maji kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ongezeko hilo litafanya mikoa hiyo kuwa na uhakika wa maji kwa miaka 50 ijayo, huku akitangaza kuisha kwa mgawo wa maji uliosababishwa na ukame.

"DAWASA tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia ujenzi wa Bwawa la Kidunda na ujenzi wa mradi wa maji Rufiji utakaomaliza changamoto ya huduma ya maji Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani.

"Miaka mitatu ijayo Dar es Salaam itakuwa na maji mengi na itakuwa salama kwa miaka mingine 50 ijayo. Kwa hiyo, kwa upande wa maji mama 'kaupiga mwingi sana'," alisema Luhemeja.

Alibainisha mikakati ya baadaye ya kuwezesha kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani, ikiwamo wa serikali kutekeleza mradi mkubwa wa Bwawa la Kidunda litakalotoa uhakika wa upatikanaji wa maji kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.



Alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 329 ambazo ni fedha za ndani za mapato ya serikali na utatekelezwa ndani ya miaka mitatu.

"Mradi huu sasa unajengwa kwa muda mfupi sana, kwa miaka mitatu na unajengwa kwa kutumia fedha za ndani za walipakodi, siyo fedha za wafadhili, hakika ni uamuzi mzuri alioufanya Rais Samia kujenga mradi huu.

"Kupitia miradi hii mikubwa kwa miaka mitatu ijayo Dar es Salaam na Pwani zitakuwa na uhakika wa kupata maji kwa kipindi chote cha mwaka, hata ikitokea ikakosekana mvua kwa kipindi cha miaka mitatu," alisema.

Luhemeja alisema kwa sasa DAWASA imeongeza uzalishaji wa maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani kutoka lita milioni 520 kwa siku hadi kufikia lita milioni 590 kwa siku na kwamba mafanikio hayo ni matokeo ya juhudi zilizofanywa na serikali kukamilisha utekelezaji wa mradi wa maji Kigamboni na kuongeza uzalishaji wa lita milioni 70.

"Kupitia uzalishaji huu, ninaweza kusema kwa majimbo yote ya uchaguzi ndani ya Dar es Salaam na Pwani yanapata huduma ya maji ya kutosha," alisema.

Kwa mujibu wa Luhemeja, huduma ya maji ipo ya kutosha kupitia mradi wa visima virefu ambavyo kwa sasa vinazalisha lita milioni 70 na ifikapo Desemba, Kigamboni itakuwa na uzalishaji wa lita milioni 98 za maji kwa siku.

Aliongeza kuwa kwa majimbo sita ya uchaguzi ya Mkoa wa Pwani ya Bagamoyo, Chalinze, Mkuranga, Kibaha Mjini na Vijijini yana hali nzuri ya upatikanaji wa maji na kazi inaendelea ya kusogeza huduma ya maji kwa wananchi wa Chalinze baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji wa Mlandizi-Chalinze-Mboga.

"Mpango tulionao DAWASA ni kuongeza uzalishaji wa maji kwenye Mtambo wa Ruvu Juu ambapo tutaongeza pampu moja kwa lengo la kufikia uzalishaji wa lita milioni 360 kutoka lita milioni 196 za sasa," alifafanua.

Aliwataka wananchi kuendelea kuwa mabalozi wazuri wa utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kulinda mazingira yanayowezesha upatikanaji mzuri wa maji.




Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Omar Shaaban (wa pili kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kulia), Tuzo ya Mkurugenzi Mtendaji Bora wa Mwaka 2022 Tanzania katika Tuzo za Top 100 Executive juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wauzaji vitoweo walia hasara ya mgawo wa umeme

**Na Jenifer Gilla**

BAADHI ya wafanyabiashara wa vyakula wanaotegemea umeme wamesema kipindi cha mgawo wanaathirika kiuchumi kwa kupata hasara.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jijini Dar es Salaam, wafanyabiashara hao wanaouza kitoweo na vyakula vingine vinavyohitaji kuhifadhiwa kwenye majokofu walisema wanapitia wakati mgumu.

Mfanyabiashara wa nyama eneo la Tabata, Michael Mgaya, alisema amelazimika kumwaga kilo tano za nyama na mbili za maini kutokana na kukosa umeme kwa saa 12 na kusababisha hasara ya Sh. 45,000.

Alisema hali hiyo imedhorotesha mwenendo wa biashara yake na kumrudisha nyuma kiuchumi kwa kuwa fedha za mtaji wa kununua kitoweo hicho imepungua hadi kufikia kununua kilo 12 kutoka 20 za awali, hali inayompa wasiwasi wa kufilisika na kufunga biashara.

"Hasara ya siku moja imeathiri sana, hapa kichwa nahisi kinawaka moto, makusanyo ya siku yameshuka kwa sababu kuna kilo nane za nyama hazipo kutokana na kupata ile hasara," alisema Mgawa.

Mfanyabiashara wa samaki wabichi Mwenge, Tina Bochi, alisema mgawo wa umeme umesababisha wateja kupungua kutoka 10 hadi watatu kwa siku baada ya kuwauzia samaki wanaotoa harufu yenye kuashiria kuanza kuharibika.

"Karibu kila siku napata mteja anayerudisha samaki kwa madai kuwa wameharibika, na ukiwaangalia ni kweli kwa sababu kuna siku hatupati umeme kabisa na samaki anatakiwa awe ameganda muda wote ili asiharibike, akiyeyuka tu hachukui muda, ukizingatia kwa sasa joto ni kali," alisema Tina.

Alisema adha hiyo imesababisha makusanyo yake kwa siku kupungua kutoka Sh. 00,000 hadi Sh. 30,000, hali inayomshawishi kufanya uamuzi wa biashara hiyo mpaka mgawo huo utakapokwisha ili kuepuka kuendelea kupata hasara.

Mfanyabiashara wa barafu katika soko la Tandika, Amri Mohamed, alisema ameamua kuacha kufanya biashara hiyo kwa sasa baada ya kupata hasara kwa siku tatu mfululuzo kutokana na mgawo huo.

"Nimeacha kwanza maana napata hasara mifuko ya maji inapasuka tu kwenye friza kwa sababu haigandi, lakini pia siuzi kwa sababu wateja wangu wakubwa wanataka barafu na sio maji ya baridi, lakini ni pigo kubwa kwangu kwa sababu nategemea biashara hii kupata pesa ya kuwapa watoto shule na kulipa kodi ndogondogo za hapa sokoni," alisema.

Aidha, mfanyabiashara wa juisi Gongo la Mboto, Alice Mdoe, alisema mgawo wa umeme umemsababishia kukaa nyumbani bila shughuli yoyote baada ya mtaji wa bidhaa yake aliyotengeneza kuharibika kwa kukosa umeme.

Alisema amepoteza Sh. 100,000 kutokana na vinjwaji hivyo kuharibika na hivi sasa anahangaika kuomba kwa ndugu na jamaa, ili apate mtaji wa kuendelea na biashara hiyo.

Alisema baada ya kukamilika awamu ya kujipanga walikuja na ya utekelezaji wa mambo yote waliyobaini ikiwamo kuongeza idadi ya wateja na kutafuta vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme ikiwamo mradi wa megawati 185 wa Kinyerezi ambao wanategemea kuuingiza kwenye Gridi ya Taifa.

Wiki iliyopita, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, alisema kuna upungufu wa megawati 300 hadi 350 kwa siku, kutokana na ukame uliosababisha maji kupungua.

Juzi akijibu maswali ya wananchi kwa njia ya mtandao, Chande alisema, makali ya mgawo wa umeme yanaendelea kupungua na wiki ijayo watafikia megawati 100 kutoka 350 zilikuwapo mwanzo.

Alisema hadi kufikia Desemba mwaka huu hali ya upatikanaji wa umeme itakuwa nzuri kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kuongeza maji katika vituo vya Kidatu na Iyovu na Februari, 2023 hakutokuwa na mgawo kwa sababu kituo cha Kinyerezi 1 kuongeza upatikanaji wa nishati hiyo.

# Viongozi wa dini watakiwa kuhamasisha upandaji miti

**Na Benny Mwaipaja,** ARUSHA

SERIKALI imewashauri viongozi wa dini nchini, kuhamasisha utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayotishia mustakabari wa taifa kutokana na madhara yanayojitokeza ikiwamo ukame na upungufu wa mvua.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati wa ibada maalumu ya kustaafu kwa Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Brighton Kilewa na kuingizwa kazini Katibu Mkuu mpya wa Kanisa hilo Mhandisi Robert Kitundu, katika Usharika wa Ngarenarok, Dayosisi ya Kaskazini Kati.

Alipongeza hatua zinazochukuliwa na kanisa hilo na mengine kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kuomba agenda hiyo ichukuliwe kwa uzito na madhehebu yote ya dini na wananchi ili kudhibiti uharibifu huo.

"Nimefurahi kusikia kanisa linaunga mkono matumizi endelevu ya maliasili tulizopewa na Mungu, vilevile nimefurahi kusikia kanisa linatambua wajibu wa kutunza mazingira, kama alivyosema Baba Askofu (Dk. Shoo), hali ya utunzaji wa mazingira hapa nchini sio mzuri, vyanzo vya maji ikiwamo mito vimekauka," alifafanua Dk. Nchemba.

"Viongozi wa dini katika mahubiri yenu wekeni msisitizo katika masuala ya utunzaji wa mazingira ikiwamo upandaji miti na matumizi ya nishati mbadala wa kuni na mkaa, nitoe wito kwenu viongozi wa dini endeleeni kushirikiana na serikali kuhamasisha utunzaji wa mazingira."

Pia alilipongeza KKKT na madhehebu mengine ya dini kwa kushirikiana na serikali kutoa huduma za kijamii kwa wananchi ikiwamo huduma za afya, elimu, maji na mambo mengine na kuahidi itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hizo za dini ili kuwahudumia wananchi.

Alisema KKKT inafanyakazi nzuri katika utoaji wa huduma kwa jamii upande wa elimu ina taasisi 120 za kielimu zikiwamo shule za msingi 17 zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia, shule za sekondari 70, vyuo vya ufundi vya kati 21, vyuo vikuu sita na shule maalum tisa kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum maeneo mbalimbali nchini.

"Ninatoa pongezi nyingi kwa KKKT kwa kuwa mstari wa mbele kutoa huduma za afya, nimeelezwa mnavyo vituo 172 vya kutolea huduma za afya, mnazo hospitali 24, ikiwamo Hospitali ya Rufani Kanda ya Kaskazini (KCMC) Moshi, pamoja na vituo vya afya/zahanati 148, katika maeneo mbalimbali nchini. Hongereni sana kwa kuunga mkono jitihada za serikali katika kusogeza huduma za afya karibu na wananchi," alisema Dk. Nchemba.

Alisema demokrasia imeimarika kwa kiwango kikubwa na serikali imeendelea kuwashirikisha wadau wote kujadili namna bora ya kuendesha shughuli za kisiasa hali iliyoleta muafaka na maelewano baina ya vyama vya siasa na wafuasi wa vyama hivyo.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Fredrick Shoo aliipongeza serikali ya kwa jitihada kubwa za kuwaletea wananchi maendeleo na wanaunga mkono jitihada hizo.

Dk. Shoo alisema ni muhimu viongozi wa dini wakahimiza hifadhi ya mazingira kutokana na athari zilizojitokeza kwa kufanya mambo kwa vitendo zaidi ili kunusuru taifa na kuishauri serikali kubuni vyanzo vya nishati mbadala kama jua na umeme katika kukabili tatizo la upatikanaji wake.

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

DAR ES SALAAM DEVELOPMENT CORPORATION

# CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI)
# FOR REDEVELOPMENT OF DDC MAGOMENI PLOT NO. 124 BLOCK "N" TO BE MODERN BUSINESS CENTER AND VIABLE INVESTMENT

**1.0 INTRODUCTION**

Dar es Salaam Development Corporation (DDC) is a Government entity established in 1973 under the District Development Corporation Act of 1973. The Corporation established as Business Investment Centre of Dar is Salaam City Council entitled for promoting economic growth and provision of entertainment service in Dar es Salaam Region. DDC undertake this functional objective through operating business ventures in its plots located within the City Business Centre. DDC owns Plot No 124 BLOCK "N" MAGOMENI, Kinondoni Municipality in Dares Salaam City.

**2.0 OBJECTIVE OF CALL**

The objective for this call is to invite strategic investors to express their interest for partnership investment with DDC in redevelopment of DDC Magomeni Plot to be modern business centre by constructing modern kids play zone, bar/restaurant and storey entertainment social Halls. The expression of Interest (EOI) is an initial process of selecting potential investor to invest in partnership under Private Public Partnership (PPP) model. This call is open to all strategic investors but DDC is not bound to select any investor if none has not meet qualification and condition set for PPP.

**3.0 DDC MAGOMENI OVERVIEW**

DDC Magomeni is one of Business Centre constructed in 1970's when DDC established. Magomeni Plot is purposed for large investment centre covering whole BLOCK "N" MAGOMENI with total size of 6013 SQM. This plot is located in strategic business area along Kondoa Road adjacent to ***New Magomeni Quarters apartments.*** The plot is surrounded by streets in all sides. It is walking distance from Morogoro Road near Usalama Bus Station. The centre is most famous place for music entertainment in Dar es Salaam City. The plot is accessible through all angles of the City Via Bagamoyo road, Morogoro road Kilwa road and Pugu road.

**3.0 INTENDED PROJECT**

DDC intends to redevelop Magomeni Plot to be modern business center by constructing storey entertainment Social Halls, Kids Play Zone, Bar/restaurant service and shops centre and the likes. The preliminary market scan and general outlook of the centre after New Magomeni Quarter apartment indicates redevelopment of that plot in business centre of that nature has quick payback period and makes viable projects.

**4.0 ELIGIBILITY AND QUALIFICATION FOR INVESTOR FOR EOI**

- I. The strategic investor must provide information that shows is capable to undertake the assignment and Investment. The information include experience of undertaking the same assignment and tangible verifiable evidence
- II. The Investor must show and prove that has financial capability of undertaking the project with tress able evidence
- III. The investor should describe type of partnership intending to engage in redevelopment of this plot. For example Building, Operating and Transfer (BOT), Shares in percent ownership, extra.
- IV. The Investor should submit concept note for the intended project showing project description, tentative cost and revenue estimate
- V. The Investor may submit substantial documents

**5.0 MODEL OF APPLICATION**

- I. The Investor has to submit covering letter and documents instructed in 4.0 above
- II. The duly signed expression of interest documents should be submitted on or before 15 December 2022
- III. The Address for Submitting EOI

**The General Manager,**
**Dar es Salaam Development Corporation (DDC),**
**P.0 BOX 1330,**
**DAR ES SALAAM.**

__________ _____

**PAUL MHACHE**
**GENERAL MANAGER**

217169602

***All correspondence should be sent to General Manager, Dar es Salaam Development Corporation, Head Office Located Karioakoo Msimbazi/Mhonda Street, P .O. Box: 1330 Dar es Salaam, You can also contact us by Phone: +255(0) 22 2180842***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vitendo hivi vikomeshwe Siku 16 Kupinga Ukatili

**TAASISI** mbalimbali zinazopinga matukio ya ukatili ziko kwenye maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga vitendo vya Ukatili.

Matukio ya ukatili ni pamoja na vipigo, udhalilishaji na ushambuliaji wa aina yoyote kwa jinsia zote hasa watoto.

Mara nyingi matukio ya watoto kutotendewa haki yamekuwa yakiripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari na vitendo vingine husababisha watu kuamua kujitoa uhai ili kuepukana na mateso wanayoyapitia.

Mijadala inaendelea sehemu mbalimbali kuona namna ya kukomesha vitendo hivyo kwa ushirikiano badala ya kuiachia taasisi moja kupambana navyo.

Ukatili unatokea nyumbani, kazini na maeneo mengine ambayo watu hukutana kufanya shughuli ziwe za kibiashara na nyingine za kujipatia kipato.

Matukio hayo yanaweza kuwa ya udhalilishaji kwa upande wa ajira. Kwa mfano mtu anapotafuta ajira akaambiwa lazima atoe kitu fulani ndipo aipate. Udhalilishaji huo ni sehemu ya ukatili ambao humfanya mhusika kukosa amani na haki yake ya kuwa huru anapokuwa sehemu yake ya kazi.

Unyanyasaji majumbani pia ni ukatili na hutokea kwa watoto, wanaume na wanawake, lakini wengine huogopa kujitokeza kulalamika kwa hofu ya kuchekwa.

Wanasaikolojia wanazungumza kila siku kuwa mtu anapopatwa tatizo linalomsumbua iwe kiakili, kimwili ni vyema akajitokeza na kulisema kuliko kubaki nalo moyoni likiendelea kumuumiza. Katika siku za hivi karibuni matukio mengi ya watu kujitoa uhai yanasababishwa na wengi wao kushindwa kuliongelea hadharani na kuamua kuchukua hatua za kujiondoa uhai.

Juzi katika mjadala uliokutanisha wanaume katika jukwaa moja mtandaoni, walikuwa wakijadili jinsi wanaume wengi wanavyonyanyasika kwenye nyumba zao kwa sababu ya kutokuwa na uwezo kiuchumi matokeo yanayosababisha hata watoto kumdharau na kwa kuwa mama ndiye anayeendesha familia hiyo, watoto humpa heshima yeye.

Hayo ni baadhi ya matukio yanayoendelea kwenye baadhi ya familia na wengine hudiriki hata kupigwa na wake zao kwa kuwa tu hana uwezo kiuchumi.

Ukatili mwingine hutokea kwa wasaidizi wa ndani ambao huachiwa jukumu kubwa la kuangalia watoto wakati wazazi wanapokwenda kazini.

Wasaidizi hao huwa wa kwanza kuamka na wa mwisho kulala na wengine hawapati chakula kizuri kwa kupewa makombo yaliyoachwa uwe mlo wake.

Wengine huambulia vipigo visivyokwisha kwa sababu tu amekuja pale kufanyakazi na kuonekana ana shida ambayo haiwezi kumuondoa na kulazimika kuvumilia.

Katika siku hizo 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, mambo yote haya hujadiliwa na jamii inatakiwa kuwa mstari wa mbele kutoa taarifa inapogundua kuwa nyumba fulani kuna tukio ambalo linakwenda kinyume na haki ya binadamu.

Kwa kufanya hivyo, watu wanaonyanyasa au kutowatendea sawa binadamu wenzao watakaogopa na kuacha kufanya vitendo hivyo. Kila mtu awe mlinzi wa mwenzake ili inapotokea unyanyasaji wa aina yoyote, aweze kuripotiwa na kukomesha unyanyasaji wa aina yoyote ile.

Kila mwaka siku hizi 16 huadhimishwa, lakini kuna baadhi ya watu wanaonekana hawajapata elimu ya kutosha. Hivyo siku hizo ziwe msaada mkubwa wa kuelimisha jamii kuepuka vitendo hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanafunzi kuhitimu bila kujua kusoma, kuandika kutufikirishe

**ELIMU** ni mchakato wa kupata maarifa, ustadi, maadili, imani na tabia, inayopatikana baada ya wanafunzi kupelekwa shuleni ili kuvipata vitu hivyo muhimu kwa ajili ya kuwasaidia kumudu maisha yao ya sasa, ya baadaye na kuchangia maendeleo ya taifa.

Umuhimu wa elimu ulitiliwa mkazi tangu wakati wa nchi kupata uhuru, pale ilipotangazwa vita kwa maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini, ambapo elimu iliwekewa mkazi kufanikisha vita hiyo.

Ili kuendelea kujiongezea maarifa katika elimu, baadhi ya wanafunzi huwa wanakwenda kusoma masomo ya ziada (twisheni), ikiwa ni juhudi za kuhakikisha wanafanikiwa katika malengo yao ya kujielimisha.

Wanafanya hivyo kutokana na umuhimu wa 'twisheni' ambao una utaratibu wake wa kurudia masomo ambapo wanapata fursa ya kuelewa vizuri zaidi masomo baada ya kuyarudia kwa mara ya pili.

Hata hivyo, wakati juhudi za kupambana na adui ujinga zikiendelea, bado yapo maeneo nchini ambayo wanafunzi wanahitimu elimu ya msingi bila kujua kusoma na kuandika, kitendo ambacho ni kama kinakwamisha juhudi hizo.

Kwa mfano, Mkoa wa Mara unatajwa kushika nafasi ya tano kitaifa kwa kuwa na wanafunzi wanaohitimu darasa la saba, bila kujua kusoma na kuandika. Ninadhani ni vyema chanzo cha hali hii kikatafutwa.

Ikumbukwe kuwa serikali imeanzisha utaratibu wa kuwa na darasa la awali katika shule zake zote, ili mtoto aanzie huko na anapoanza darasa la kwanza awe tayari anajua kusoma na kuandika.

Ofisa Elimu wa mkoa huo, Benjamin Oganga, anabainisha hali hiyo mbele ya viongozi wa elimu wa kada na ngazi tofauti, wa wilaya na mkoa muda mfupi kabla ya uzinduzi wa mkakati wa kitaifa wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya elimu msingi.

Kwamba mkakati huo uliozinduliwa kimkoa na Mkuu wa Mkoa huo, Meja Jenerali Suleiman Mzee, utakuwa mwarobaini wa changamoto hiyo na nyingine, zikiwamo zinazotokana na mafanikio katika sekta ya elimu.

Ofisa elimu huyo katika ufafanuzi wake, anasema ufuatiliaji uliofanywa unaonyesha ndani ya miaka mitano, wanafunzi 350,000 katika mkoa huo hawakuhitimu elimu ya msingi.

Lakini viongozi wa elimu kuanzia ngazi ya shule mpaka mkoa wanatakiwa kushirikiana na mamlaka nyingine, kutafuta kila mwanafunzi aliyetakiwa kuwa shuleni, lakini hayupo, ikiwezekana wazazi wa wanafunzi hao wabanwe.

Kwa mikakati hiyo na mingine mingi ninadhani kama mkoa umedhamiria kumaliza tatizo, inawezekana ukafanikiwa na kuondoa aibu hiyo ambayo haitakiwi kuwapo katika karne hii ya 21.

Jambo lingine la muhimu ni ushirikiano wa karibu kati ya walimu, wazazi na walezi na pia wangetambua juhudi zinazofanywa na serikali za kutoa elimu bure kuwa zinalenga kuhakikisha kila mtoto anapata elimu.

Lakini bahati mbaya wapo baadhi na walezi hata wakiona watoto wao hawaendi shule hawawaulizi na pia hawafuatilii shuleni au hata kukagua madaftari yao, ili kujua kinachoendelea.

Kwa mazingira kama hayo ni wazi mbumbumbu wataendeelea kuwapo iwapo kila mmoja hatatimiza wajibu wa kuhakikisha mtoto wake anakwenda shule na anapata elimu ambayo inatolewa bure.

Sidhani kama bado kuna visingizio tena kuhusu masuala ya ada, kwani kinachotakiwa ni mzazi au kununua sare, madaftari na vifaa vingine vya shule ambavyo kimsingi ni vya muhimu katika elimu.

Ushirikiano wa karibu ni wa muhimu kwa wadau wote wa elimu kwa jili ya kumaliza tatizo hilo, wazazi na walezi ni wadau mojawapo, hivyo sidhani kama itapendeza wakijiweka pembeni.

Lakini pia wanafunzi nao wasichukulie shule kama sehemu yao ya kukutana na kucheza tu, bali watambue kuwa hiyo ni sehemu ya kupata elimu ili kuondokana na adui ujinga ambaye anaweza kukwamisha ndoto zao na hata kuwatumbukiza kwenye shimo la kuangamia.

# Waziri ashauri sekta binafsi kuwaajiri waliosoma nchini

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imetoa rai kwa taasisi binafsi kuwaangalia kuwaajiri wahitimu wazawa ili kuwaondoa katika mkwamo wa kupata ajira na kuwawezesha kuchangia uchumi wa nchi.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Chande ametoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam alipowatunuku wahitimu wa taaluma wa ngazi tofauti 4,272 wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Alisema taasisi binafsi zinapaswa kuwaangalia wahitimu wa elimu ya juu ndani ya nchi na kuwapa kipaumbele kuajiriwa badala ya wanaohitimu nje pekee kwa kuwa wahitimu hao wanayajua vizuri mazingira na vikwazo vilivyoko kwenye jamii. Alisema idadi ya wahitimu wa elimu ya juu imeongezeka kutoka 209,114 hadi 220,230 mwaka 2020 na kwamba ni muhimu taasisi kusaidiana na serikali kwenye suala na ajira.

"Hakuna chungu kinachoweza kuivisha kilichomo ndani bila mafiga matatu. Walimu, wanafunzi, wazazi au walezi na wahisani, vyote hivi vimeshirikiana wakafikia kuhitimu," alisema Chande.

Aliwataka wakufunzi wajikite katika kuwapa wanafunzi mafunzo na mbinu mbalimbali ili wafanye utafiti ambao utatatua matatizo kwenye jamii.

Naibu Waziri huyo pia aliwataka wahitimu waliopata mikopo ya masomo, warejeshe ili iwe endelevu kwa wanufaika wengine.

"Wahitimu muwe wazalendo, mjenge taifa lenu kwa kufanya kazi kwa bidii, kuwa kioo cha chuo, kuwa wabunifu na kuepuka rushwa na ukatili wa kijinsia," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la IMF, Prof. Emmanuel Mjema, alisema chuo kitaboresha viwango vya mafunzo kwa wanafunzi na kupata wahitimu watakaojiajiri ndani na nje ya nchi.

"Elimu pekee inaweza kumkomboa Mtanzania dhidi ya maadui watatu; ujinga, maradhi na umaskini, kila mmoja ana jukumu la kufanya hivyo," alisema.

Kaimu Mkuu wa chuo, Dk. Emmanuel Mnzava alisema kina kampasi Mwanza, Dodoma, Simiyu na sasa kinamalizia ujenzi wa Kampasi ya Geita kwa ufadhili wa serikali.

"Kama tunavyofahamu, elimu ni chachu ya mabadiliko ya kitabia, kiutendaji na uwezo wa kubadilisha mazingira yanayotuzunguka," alisema Dk. Mnzava.

Alifafanua kwa mara ya kwanza, wanafunzi 59 walihitimu mwaka 1972 na sasa chuo kinatoa zaidi ya kozi 33 katika fani mbalimbali zikiwamo fedha, bima, uhasibu na nyinginezo.

"Hadi mwaka 2021, jumla ya wanafunzi 39,723 walitihimu chuoni hapa katika kozi mbalimbali," alisema.

**Hadi mwaka 2021, jumla ya wanafunzi 39,723 walitihimu chuoni hapa katika kozi mbalimbali.**




Ofisa Huduma kwa Wateja, Faithful Joshua, akitoa elimu kwa mwananchi aliyetembelea banda la TADB wakati wa maonesho ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Rock City Mall jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto atoa ushahidi dhidi ya baba yake kesi mauaji

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Mbweni, Kulwa Rajabu (32) ametoa ushahidi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu dhidi ya baba yake mzazi, Boi Rajabu anayetuhumiwa kumuua Abbas Mwijuma kwa kumchoma kisu tumboni.

Vilevile, Boi ameiomba mahakama azungumze na mwanawe angalau kidogo baada ya Kulwa kumaliza kutoa ushahidi wake.

Kulwa, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Subira Mwaluguri alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya wa Mahakama hiyo kuwa yeye ni mkazi wa Mbweni, Mitaa ya CCM.

Alidai kuwa Februari 8, 2019, majira ya usiku mnene, akiwa amelala, aligongewa mlango na shangazi yake aliyemtaja kwa jina la Mwakadi akimweleza kwamba amesikia baba yake (Boi) amemchoma kisu Mwijuma.

"Shangazi alipoondoka nilimpigia simu na kumuuliza yuko wapi, akasema yupo nyumbani kwake amelala, nikamwambia njoo kwangu, alipofika nilimuuliza kama amemchoma kisu Mwijuma, akakataa.

**Nikamwambia baba asiondoke nyumbani kwangu kwa sababu watu wanaweza kumdhuru, kulipokucha aliondoka kwenda kwenye shughuli zake za uvivu majira ya saa 12 alfajiri.**

"Nikamwambia baba asiondoke nyumbani kwangu kwa sababu watu wanaweza kumdhuru, kulipokucha aliondoka kwenda kwenye shughuli zake za uvivu majira ya saa 12 alfajiri," alidai Kulwa.

Baada ya shahidi kudai hayo mahakamani, Wakili Mwaluguri alimtaka Kulwa amwoneshe mtu anayemzungumzia katika kesi hiyo kwa kumgusa, ambapo alitoka katika kizimba chake kwa kujivuta kidogo akielekea kwenye kizimba ambacho alikuwa amekaa baba yake mzazi.

Kabla ya Kulwa kufika katika kizimba, baba yake alisimama juu na mwanawe akamshika bega na kudai kuwa ndiye Boi Rajabu ambaye ni baba yake mzazi.

Pia wakati Kulwa anarudi baba yake alikaa chini huku akimwangalia mwanawe huku akijifuta uso wake kwa kitambaa na macho yake kuonekana yana rangi nyekundu.


Wakati Kulwa anatoka baada ya kujibu maswali ya wakili wa baba yake, Hilda Mushi, Hakimu Mbuya alimuuliza mshtakiwa kama anataka kuzungumza na mwanawe.

"Ndiyo, ninataka kuzungumza na mwanangu angalau kidogo na huyo aliyekuwa naye ni mama yangu mzazi," alidai mshtakiwa Boi.

Hakimu Mbuya alisema mahakama haikuwa na kipingamizi katika hilo na kesi ikiisha, atapata nafasi ya kuzungumza nao, mshtakiwa akimshukuru hakimu kwa hilo.

Inadaiwa Februari 8, 2019 mshtakiwa, akiwa Mbweni Miti Mitatu, alimuua Abbas Mwijuma.

## KABWELA



HABARI KITAIFA

# Mbunge abaini madudu ujenzi kituo cha afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MBUNGE wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, ameibua 'madudu' katika mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Ntuntu unaogharimu Sh. milioni 500 baada ya msimamizi wa mradi huo kudaiwa kumpa kazi ya kusambaza vifaa mke wake.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Ntuntu baada ya kukagua ujenzi wa kituo hicho juzi, Mataturu alisema kuna usimamizi mbovu unaosababisha kisikamilike kwa wakati na hivyo kumwomba Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutupia jicho ujenzi wa kituo hicho.

"Msimamizi amekosa sifa ya kuwa msimamizi wa mradi, haiwezekani wewe umepewa mradi unakwenda kumpa mkeo ndiye anakuwa 'supplier', unategemea hizo fedha zisiliwe? Hatuwezi kuona usimamizi mbovu unaoendelea," alidai.

Mtaturu alisema hapingani na suala la watu kupewa zabuni za ujenzi, akitahadharisha "unapokuwa sehemu ya maslahi huwezi kusimamia vizuri".

"Nimeambiwa Sh. milioni tano tu ndio ipo kwenye mchakato wa ununuzi wa vifaa, nimwombe DC (Mkuu wa Wilaya) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi wa mradi huu," alisema.

Mbunge huyo alionya yeyote aliyechezea fedha za serikali katika mradi huu hatabaki salama na kwamba suala hilo atalipigia kelele hadi bungeni ili kuhakikisha fedha zilizotolewa zinakamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya na si vinginevyo.

Alisema kuwa zilitolewa Sh. milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa majengo matatu ya kituo hicho ambayo yamekamilika vizuri lakini tatizo limejitokeza katika Sh. milioni 250 zilizotolewa awamu ya pili kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wajawazito, chumba cha maiti na jengo la upasuaji kwa kuwa ujenzi wake unasuasua.

Mganga Mkuu wa Wilaya Ikungi, Dk. Solomon Ombati, akizungumza na Nipashe kwa simu kuhusu suala hilo, alisema kuwa baada ya malalamiko ya mbunge kuhusu msimamizi huyo, hatua zimeshachukuliwa kwa kumwondoa na sasa ujenzi unasimamiwa na Mhandisi wa Wilaya.

Dk. Ombati pia alisema mke wa msimamizi wa mradi hakuwa msambazaji wa vifaa bali alikuwa ni miongoni mwa wanakikundi cha kufyatua matofali ambayo ndiyo yalikuwa wakitumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya.

"Baada ya mbunge kulalamika, maofisa kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Tiba, walifika katika kituo cha afya na kukagua na kujiridhisha majengo yaliyojengwa awamu ya kwanza yako vizuri na sasa huduma za matibabu zimeanza kutolewa," alisema.



Rais wa Lions Club ya Infinity Dar es Salaam, Nafisa Khanbhai (wa nne kulia), akimkabidhi Mwalimu Msaidizi wa Shule ya Msingi Buguruni Viziwi, Richard Kweka (wa nne kushoto) mito, mashuka na magodoro 146 katika hafla iliyofanyika shuleni hapo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Msaada huo umetolewa na Jumuiya ya Shree Jain Sangh Dar es Salaam kwa kushirikiana na Klabu ya Chama cha Lions Club Infinity. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi shule mpya ya sekondari wagharimu bilioni 7.7/- Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya,**

SONGEA

SERIKALI imejenga shule mpya 11 za sekondari mkoani Ruvuma kwa gharama ya Sh. bilioni 7.7, uongozi wa mkoa huo umebainisha.

Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia mipango katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Jumanne Mwankoo, jana mjini hapa alisema shule hizo mpya kuwa zimejengwa katika halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma.

Alisema shule hizo zimejengwa kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP) ambapo kila halmashauri imejengwa shule moja kwa thamani ya Sh. milioni 470, isipokuwa Halmashauri za Tunduru iliyojengwa shule tatu na Namtumbo iliyojengewa shule mbili ikiwamo ya wasichana ya mkoa iliyojengwa eneo la Migelegele kwa gharama ya Sh. bilioni tatu.

"Mradi wa SEQUIP umewezesha kila shule ya sekondari kuwa na jengo la utawala, vyumba vya madarasa, vyoo, mfumo wa maji, maabara, maktaba na jengo la TEHAMA, shule zote zinatarajia kuanza kuchukua wanafunzi Januari 2023," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, alikagua moja ya shule hizo katika Halmashauri ya Madaba.

Akitoa taarifa ya mradi wa shule hiyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Madaba, Sajidu Mohamed alisema mradi wa ujenzi umetengewa Sh. milioni 470 na ulianza utekelezaji Machi mwaka huu na hadi sasa fedha zilizotumika ni zaidi ya Sh. milioni 468.

Alisema ujenzi wa mradi huo upo katika hatua za ukamilishaji ambapo hadi sasa umefikia asilimia 95 ukihusisha ujenzi wa madarasa manane, jengo moja la utawala, vyumba vitatu vya maabara, matundu 20 ya vyoo, minara miwili ya matanki na mfumo wa kunawa mikono.

Alisema ujenzi umefikia asilimia 65 kwa majengo mawili ya maktaba na chumba cha TEHAMA na kwamba mradi unatarajia kukamilika kwa asilimia 100 kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Thomas, alimwagiza mkandarasi kushughulikia dosari zote zilizojitokeza ikiwamo mipasuko kwenye kuta.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kutekeleza mradi huo, hivyo ni lazima majengo yalingane na thamani ya fedha kwa kutekeleza mradi katika ubora na viwango.

Katibu Tawala Wilaya ya Songea, Pendo Ndumbaro aliahidi maagizo yote yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa yatafanyiwa kazi, akimwagiza mkandarasi kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha mradi huo.

Serikali inatekeleza mradi wa SEQUIP kwa kujenga shule mpya za sekondari 1,000 nchi nzima.

## Tanzania kunufaika Mpango Usimamizi Rasilimali za Bahari

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Magangaa, amefungua warsha ya mafunzo ya kikanda kuhusu Mpango wa Matumizi ya Eneo la Bahari (MSP) na Ukanda wa Pwani ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi jijini Dar es Salaam.

Warsha hiyo inalenga kujenga uwezo wa wataalamu kutoka nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi katika kuandaa na kutekeleza Mpango wa Matumizi ya Eneo la Bahari, usimamizi wa taarifa za kimazingira, kubadilishana uzoefu na kufahamu hatua zilizofikiwa na nchi wanachama katika kuandaa na kutekeleza mpango wa matumizi ya eneo la bahari.

Mary alisema jana kuwa Tanzania ni mwenyeji wa kikao kazi hicho kinachohusisha wajumbe kutoka zaidi ya nchi 10 wanaotekeleza Mkataba wa Nairobi unaohusu hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi.

"Warsha hii imehusisha nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi na nchi zinazoshiriki ni pamoja na Tanzania, Comoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Shelisheli na Afrika Kusini," alisema.

Mary alisema warsha hiyo itasaidia kuja na mpango na usimamizi endelevu wa matumizi ya rasilimali za bahari ikiwa ni pamoja na mgawanyo sahihi wa matumizi ya bahari.

Alisema Tanzania inajipanga mapema katika kuandaa mpango huo kwa kuzingatia kuwa uchumi wa buluu ni miongoni mwa agenda za dunia.

"Ninapozungumzia uchumi wa buluu ninasisitiza usimamizi endelevu na shirikishi wa mifumo ikolojia ya pwani na bahari ya Tanzania ili kuendelea kutoa bidhaa na huduma muhimu ikiwa ni pamoja masuala ya uvuvi na uchimbaji wa mafuta na gesi pale vitakapogundulika," alisema.

**HABARI KITAIFA**

## Vijana wapatiwa vifaa vya kisasa umwagiliaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

VIKUNDI 13 vinavyoundwa na vijana vinavyojishughulisha na kilimo cha mboga katika halmashauri sita za Mkoa wa Singida, vimekabidhiwa pampu 13 za umwagiliaji zinazotumia nishati ya jua zenye thamani ya Sh. milioni 23.4.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, alikabidhi pampu hiyo juzi kwa vijana wa vikundi hivyo kutoka Halmashauri za Wilaya ya Manyoni, Itigi, Mkalama, Singida, Iramba na Manispaa ya Singida.

Mwaluko, akizungumza na vijana hao katika ukumbi wa ofisi za shirika lisilo la kiserikali la SEMA mkoani hapo, alisema mashine hizo zitawasaidia kuongeza kipato katika shughuli za kilimo cha bustani na kuwataka wazitunze ili kudumu kwa muda mrefu.

Aliwataka vijana waache kulalamika hakuna ajira na badala yake wajitume kufanya kazi za kilimo na ufugaji kwa kuwa bidhaa zitokanazo na shughuli hizo zina soko kubwa ndani na nje ya mkoa.

Katibu Tawala huyo alilishukuru Shirika la NSV kupitia mradi wake wa OYE (Opportunities for Youth Employment) kwa msaada wa mashine hizo ambazo zimegharimu kiasi cha Sh. milioni 1.8 kila kimoja.

Ofisa Mwandamizi wa Usimamizi na Tathmini Mradi wa OYE, Belinda Masawe, alisema mashine hizo hutumia nishati ya jua ambayo haitawaingizia gharama za uendeshaji wanakikundi.

Belinda alisema mashine moja ina uwezo wa kumwagilia shamba lenye ukubwa wa ekari mbili kwa msimu mmoja na inadumu kwa zaidi ya miaka 10 ikitunzwa vizuri.

Alisema vikundi hivyo vimepewa muda wa miaka miwili wa uangalizi na endapo zitaharibika kabla ya hapo, vitarudishwa kwa muuzaji.

Awali akitoa maelezo ya ukaribisho, Ofisa Vijana wa Mkoa wa Singida, Fredrick Ndahani, alisema fursa za biashara katika Mkoa wa Singida ni nyingi kwa kuwa kuna miradi mingi imeanzishwa ikiwamo bomba la mafuta na miradi ya machimbo ya madini na soko ni kubwa.

Alisema serikali imeweka mazingira mazuri kwa vijana kuhakikisha wanajiajiri na wanapata mitaji kupitia mikopo ya halmashauri ambayo kuna asilimia nne maalum kwa ajili ya vijana kutoka kwenye fungu la asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

# Waziri ampa siku 15 DED kukamilisha ujenzi madarasa

**Na Cosmas Antony,** TARIME

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amempa siku 15 Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Tarime Mkoa wa Mara kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa baada ya halmashauri hiyo kuwa nyuma katika utekelezaji wa ujenzi huo.

Amesema Halmashauri jirani ya Tarime Vijijini iko katika hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huo wa ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari.

Silinde alitoa agizo hilo jana baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa hayo katika Mkoa wa Mara na kubaini Halmashauri ya Mji wa Tarime iko nyuma na kuitaka itumie muda huo wa wiki mbili kumpa taarifa ya ukamilishaji wa madarasa hayo ikiambatana na picha na atarudi mwenyewe kukagua.

Alisema amebaini kuwapo uzembe uliosababisha kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa madarasa katika halmashauri hiyo, akitamka: "Nimetoka Tarime Vijijini, wao wanamalizia ukamilishaji wa madarasa hayo katika kupiga rangi na wengine washamaliza na vifaa vyote wananunua.

"Hapa mjini kwanini ninyi mpaka sasa bado? Mkurugenzi ninataka taarifa baada ya siku 15 kuona mlivyokamilisha na picha ofisini kwangu kama mlivyoahidi kuwa siku hizo mtakuwa mmekamilisha ujenzi na nitarudi kukagua."

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara alimwomba Naibu Waziri Silinde kuwasilisha serikalini kilio chao cha muda mrefu cha kupatiwa mabweni katika shule yao ya sekondari Kemambo kwa kuwa kwa sasa wanakabiliwa na tatizo la baadhi ya wanafunzi kuwa watoro na kukimbilia kwenda kufanya kazi migodini ili wapate fedha.

Silinde, akimjibu mbunge huyo, alisema serikali imelichukua jambo hilo na wako mbioni kutoa fedha za ujenzi wa mabweni hasa katika shule ambazo zipo mbali na makazi ya jamii za kifugaji ili kuwafanya wanafunzi wasome kwa utulivu bila kuingiliana na shughuli za kijamii.



Mkurugenzi wa Udhibiti Uchumi wa TCAA, Daniel Malanga, akizungumza kwenye ufunguzi wa mkutano wa 42 wa mwaka wa Chama cha Waongozaji Ndege Tanzania (TATCA) mwishoni mwa wiki katika ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# TRA yakunwa ulipaji kodi kwa hiari

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imeutaja Mkoa wa Njombe kuongoza kwa wafanyabiashara wake kulipa kodi kwa hiari kulinganishwa na mikoa mingine nchini.

Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alibainisha hilo wakati wa kilele cha wiki ya shukrani kwa mlipakodi ambayo ni maalum katika kutambua mchango wa wafanyabiashara nchini kote.

Kidata alisema wafanyabiashara mkoani hapa wamekuwa mfano wa kuigwa kwa kuwa wanalipa kodi kwa hiari pasi na kushurutishwa.

"Faraja ambayo tunayo kwa walipakodi wa Mkoa wa Njombe ni kuwa ulipaji wa kodi kwa hiari upo juu kulinganisha na baadhi ya mikoa," alisema Kidata.

Alisema ulipaji kodi kwa hiari ni uzalendo ambao wafanyabiashara wanatakiwa kuendelea nao kwa kuwa unadhihirisha uhitaji wa kuchangia maendeleo ni wajibu wa kila mmoja.

Aliwapongeza walipakodi wote nchini kwa kujitoa katika ulipaji wa kodi kwa kuwa shughuli zote za maendeleo zinazofanyika nchini ni matokeo ya wananchi kulipa kodi.

Kidata aliagiza watendaji wa mamlaka hiyo kujikita katika kutoa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara wote nchini ikiwamo matumizi sahihi ya mashine za risiti za kiektroniki (EFD).

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa mamlaka hiyo katika ngazi zote.

Alisema milango ipo wazi kwa wafanyabiashara pale wanapoona kuna sehemu hawajaridhika na watapewa ushirikiano ili haki itendeke katika shughuli wanazozifanya.

"Sisi kama serikali ndani ya Mkoa wa Njombe hatuna tatizo kubwa na wafanyabiashara wetu, yale ambayo yanajitokeza tunapeana elimu ya namna ya kuyatatua," alisema Mtaka.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Njombe, Sifaely Msigala, alisema TRA inatakiwa kuweka mifumo mizuri katika ukusanyaji kodi ikiwamo kushirikiana na mamlaka zingine kuhakikisha kunakuwa na bei elekezi katika kila kundi la bidhaa inayonunuliwa ili kuweka mazingira rafiki kwa wote.

"Tofauti ya kodi inayotozwa bandarini katika bidhaa ya aina moja, imekuwa ikileta usumbufu mkubwa mpaka leo kwa wafanyabiashara," alifafanua Msigala.

Katika hatua nyingine, TRA Mkoa wa Katavi imetoa vyeti kwa walipakodi bora wa mwaka mkoani humo kwa lengo la kutambua mchango wao katika ulipaji wa kodi na kutoa hamasa kwa wengine kuiga mfano huo.

Kamishina wa Upelelezi wa Kodi wa TRA, Andengenye Mwaipopo, alisema vyeti hivyo vimetolewa kwa walipakodi wadogo, wa kati na wakubwa.

Mwaipopo alitaja vigezo walivyozingatia katika kutoa vyeti hivyo kuwa ni pamoja na ulipaji stahiki wa kodi na kuwasilisha ritani za kodi kwa wakati.

Waliopewa vyeti hivyo kutoka Wilaya ya Mlele niWillium Marco na Aniseth Lusambo na Mteis Traders Company Limited.

Walipakodi wadogo kutoka Katavi ni waliopata vyeti hivyo ni Abdala Sound, Benard Sayi na Shabir Hassanal; walipakodi wa kati ni Madema Company Limited, Infinity Oil Co.LTD na MM (2001) Company Limited na walipakodi wakubwa ni RK General Supplies Company Limited, Xiamen Ongoing Construction Group Company Limited na Katavi Mining Campany Limited.

# Bilioni 3.6/- zatumika ujenzi jengo magonjwa ya mlipuko

**Na Mwandishi Wetu,**
KIGOMA

SERIKALI imejenga jengo la magonjwa ya mlipuko na kununua vifaa tiba eneo la Nyamusi katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma kwa gharama ya Sh. bilioni 3.6 kwa lengo la kudhibiti magonjwa hayo pindi yatakapotokea.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Robert Rwebangira, alisema jengo hilo limejengwa katika wilaya hiyo kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu kutoka nchi za jirani ambazo huko magonjwa ya mlipuko kama Ebola na dengue hutokea na hivyo kuwa rahisi kuingia nchini.

"Wilaya ya Kasulu ina mpaka mrefu eneo la Kitanga ambao unaruhusu watu kuingia bila udhibiti maalum wa kujua hali zao za afya na hivyo kuna uwezekano mkubwa wa wao kupita wakiwa tayari wana ugonjwa na kusababisha kusambaa kwa wakazi wa maeneo hayo na ya jirani," alisema.

Rwebangira pia alisema Wilaya ya Kasulu inatunza wakimbizi kutoka nchi za Burundi na Congo ambao kwa nyakati tofauti hutembelewa na ndugu zao kutoka maeneo tofauti, hivyo ni muhimu kuwa na kituo hicho ambacho kitawezesha kukidhi magonjwa hayo ya hatari kwa binadamu kwa haraka zaidi.

Alisema jengo hilo lina eneo la vitanda vinane kwa ajili ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum, wodi mbili (moja ya wanawake na nyingine ya wanaume), eneo la kufua nguo, eneo la kutunza miili pamoja na kichomea taka maalum.

Alisema jengo hilo limejengwa likiwa na miundombinu yote inayowezesha huduma stahiki kwa wagonjwa na ulinzi kwa watoa huduma sambamba na kuhakikisha kuwa ugonjwa hausambai na kuleta madhara zaidi.

Alisema jengo hilo lina uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa 12 kwa wakati mmoja.

Mganga Mkuu alifafanua zaidi kuwa chanzo cha magonjwa ya mlipuko ni wanyama na kwamba zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wa Kasulu ni wakulima na wafugaji, hivyo kuwa hatarini kupata maambukizo.

Alisema kigezo hicho pia kilizingatiwa katika uamuzi wa serikali kujenga jengo hilo wilayani Kasulu ili kukabiliana na hatari inayoweza kujitokeza kwa muda usiotarajiwa.

Rwebangira alisema wilaya hiyo pia imeridhia kutoa Sh. milioni 550 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tano zenye uwezo wa kutunza familia tano na nyumba tatu zenye uwezo wa kutunza familia tisa kwa lengo la kutosheleza huduma za dharura katika hospitali ya wilaya hiyo.

"Eneo la hospitali ni jipya, hakuna nyumba za kupanga, hivyo wafanyakazi wengi isipokuwa wanaolala zamu waliishi Kasulu mjini takribani Km 20 kutoka hapa, busara imetumika kujenga nyumba hizi ambazo zimekamilika kwa asilimia 85 na muda wowote ndani ya mwezi huu wafanyakazi wataingia na hivyo kupunguza adha za dharura na changamoto za usafiri," alifafanua.

Rwebangira alisema kipaumbele zaidi kitatolewa kulingana na majukumu ya watoa huduma ikiwamo wanaotoa huduma za dharura za upasuaji, wanaotoa huduma za dawa za usingizi, madereva pamoja na wauguzi.

Mkazi wa Kasulu, Felister John alisema kuna haja jengo hilo la magonjwa ya mlipuko lifunguliwe na kuanza kufanya kazi, akipongeza uamuzi wa kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya watoa huduma za afya.

Mkazi mwingine Tija Moshi alisema kuwapo madaktari karibu na kituo hicho cha afya kutasaidia kutoa huduma za dharura ikiwamo ya upasuaji kwa kinamama wajawazito na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.




ASP Dumu Mwalugenge wa Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, akitoa mafunzo kwa waendesha boda-boda kuhusu matumizi ya alama za barabarani ikiwa ni sehemu ya kampeni ya Tanzania Breweries Ltd (TBL) iitwayo 'Okoa Maisha' jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RUWASA yawezeshwa vifaa kuchimba visima

**Na Steven William,** MUHEZA

TAKRIBANI visima 10 vinachimbwa katika kata 10 wilayani Muheza mkoani Tanga kwa lengo la kutatua kero ya uhaba wa maji kwa wananchi.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Muheza, Cleophace Maharangata, alibainisha mkakati huo juzi alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema wamepokea magari mawili yenye mitambo ya kuchimba visima yalitolewa na serikali kwa ajili ya uchimbaji wa visima.

Maharangata alisema magari hayo yameletwa kwa ajili ya kutoa huduma katika Mkoa wa Tanga na uongozi umeamua uchimbaji wa visima uanzie wilayani Muheza.

Wakati wa mapokezi ya magari hayo juzi, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM ) Wilaya ya Muheza, Laicky Gugu, aliipongeza serikali kwa kutekeleza wajibu wake kikatiba kwa kuwapa mitambo hiyo ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi, akisisitiza kuwa Muheza inakabiliwa na kero ya uhaba wa maji.

Alisema miradi mingi ya maendeleo ya ujenzi haikamiliki kwa wakati kutokana na ugumu uliopo katika kupata maji, hivyo magari hayo yatasaidia kukamilika kwa miradi hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Erasto Mhina, alisema uchumi wa wananchi wa Muheza utakua kutokana kuwapo uhakika wa kupata huduma ya maji.

Alisema uhaba wa maji unachangia wilaya hiyo kushindwa kupata wawekezaji wengi, akisisitiza madiwani watasimamia uchimbaji wa visima hivyo ili wananchi wanufaike na mkakati huo wa serikali wa kumaliza tatizo la uhaba wa maji nchini.

# Waziri ataka maboresho mitaala Taasisi ya Uhasibu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameitaka Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) kuendelea kurekebisha mitaala yao ili kukidhi haja ya soko la ajira nchini.

Vilevile, ameitaka taasisi hiyo kufanya utafiti ili kutatua kero mbalimbali kwenye jamii na kuchangia maendeleo ya uchumi nchini.

Alitoa maagizo hayo juzi kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba wakati wa mahafali ya 20 ya TIA mkoani Singida.

Waziri huyo alisema serikali inahitaji wataalamu wenye weledi, maarifa na umahiri wa kutatua kero na si kuongeza kero.

"Zingatieni kwa umakini suala la umahiri katika mitaala yenu ili tuweze kuwa na wataalamu wenye uwezo wa kuleta mabadiliko kiuchumi," alisema.

Waziri huyo pia aliwataka wahitimu wa vyuo vikuu nchini kutumia muda wao mwingi kujisomea vitabu mbalimbali vinavyoshabihiana na taaluma zao badala ya kutumia muda mrefu kwenye mitandao ya kijamii.

Alisema wanachuo watakapojenga utamaduni wa kusoma vitabu na kujikumbusha mambo waliojifunza, itawasaidia kuongeza maarifa mapya na umahiri katika kazi za uhasibu badala ya kutumia muda wao kwenye mitandao ya kijamii.

Alisema wahitimu wa vyuo wanapaswa kuwa mfano bora kwa kufanya kazi kwa haki, juhudi na ubunifu na kujiepusha na vitendo vya rushwa na ubadhirifu kwa kuwa taifa linategemea kwa kiasi kikubwa mchango wao.

"Wale mnaodhani kusoma vitabu ni kazi ya wazee baada ya miaka mitano muwe na uhakika hiyo shahada mliyopata haitakuwa kichwani. Dunia inabadilika sana, leo hii tupo katika mabadiliko ya nne ya viwanda ambayo teknolojia ndio inachukua nafasi," alisema.

Aliongeza kuwa moja ya mambo ambayo ni tatizo kubwa kwa kizazi cha sasa ni kutokusoma vitabu, akisisitiza kunahitajika mabadiliko kwa kuanza kusoma vitabu ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kuongeza ujuzi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya chuo hicho, Wakili Saidi Chiguma, alisema taasisi inatoa elimu inayoendana na mahitaji ya soko, hivyo kusababisha chuo hicho kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi zaidi ya 25,000.

Aliwataka wahitimu kutumia elimu waliyopata kuiletea nchi maendeleo ya kiuchumi na wasiishie hapo badala yake waendelee kuongeza viwango vya elimu.

"Elimu ni kama kiumbe hai, inatakiwa itumike na iwe inahuishwa mara kwa mara vinginevyo inakufa," alitahadharisha Wakili Chiguma.

Wahitimu 3,666 katika chuo hicho mwaka huu wametunukiwa katika ngazi ya astashahada na shahada, mahafali hayo yakihusisha tawi la Singida, Mwanza na Kigoma.



# Vifo vya kujinyonga wenyeviti wa vijiji vyaacha maswali

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

VISA viwili vinavyohusu wenyeviti wa serikali za vijiji katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, kujitoa uhai kwa kujinyonga katika kipindi kisichozidi wiki tatu, vimeacha maswali yasiyojibika, huku wananchi wa maeneo hayo wakishinikiza serikali kuchunguza chanzo cha vifo vyao.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wananchi na viongozi wao, walipaza sauti zao wakitaka Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro, kuchunguza mfululizo wa matukio hayo ya wenyeviti kujinyonga, kwa kuwa vifo vyao vimeacha maswali mengi ambayo hayajajibiwa.

Novemba 25, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kyeri kilichoko Kata ya Machame Magharibi, Erasto Mushi (58), alikutwa akining'inia juu ya mti wa msesewe katika shamba la kahawa akiwa amejinyonga.

Aidha, Novemba mosi, mwaka huu, Mwenyekiti wa Somanga, wilayani humo, Geofrey Massawe (45), alijiua kwa kujinyonga kwa kutumia kamba ya kufungia ng'ombe aliyokuwa ameifunga juu ya mti wa parachichi.

Akizungumzia visa hivyo, Diwani wa Machame Magharibi, Martin Munisi, alisema hadi sasa bado wananchi wa Kyeri, wanajiuliza na haelewi ni tatizo gani lililompata mwenyekiti wao hadi kuamua kukatisha uhai wake, wakati hakuwa na mgogoro na familia yake.

"Marehemu hajaacha ujumbe wowote, tulijua mchana juzi, baada ya kijana mmoja aliyeenda huko shambani kwenye majani, kuona chini kuna kiroba, kuna panga, kuna mabuti na aliposogea mbele kidogo, ndiyo akakuta kuna mtu amening'inia," alisema.

"Tunaomba uchunguzi ufanyike kuhusu visa hivi, kwa sababu mojawapo ya madhara ya watu kujiua ni kuacha matatizo katika familia. Vifo hivi huwa ni vya ghafla, kwa hiyo huiacha familia bila kujiandaa na wakati mwingine hata taifa linapoteza nguvu kazi."

Wakati Penda Kimaro, alisema ni muhimu serikali na vyombo vyake vikafanya uchunguzi ili kubaini kama ni uhalifu au ni hali inayosababishwa na mfumo mzima wa maisha kubadilika, ikiwamo upatikanaji wa fedha, migogoro ya kikazi, familia au siasa.

Alipoulizwa jana kuhusu tukio la kujiua kwa Mwenyekiti wa Kyeri, Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP), Simon Maigwa, alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa Mwenyekiti huyo alijiua mwenyewe, kwa kujinyonga kwa kutumia kamba ya manila.

Alisema bado wanachunguza sababu za kujinyonga kwa mwenyekiti huyo, kwa kuwa hajaacha ujumbe wowote.



Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Michael John, akikagua madawati 80 katika Shule ya Sekondari ya Masagalu iliyoko Kata ya Masagalu wilayani humo alipofanya ziara. **PICHA: DEGE MASOLI**

## IAA yalaani mwanafunzi kushambuliwa, kudhalilishwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MENEJIMENTI ya Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), imelaani tukio la kushambuliwa na kujeruhiwa kwa mwanafunzi wa chuo hicho na askari wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa la SUMA JKT, ukisema tayari wamekutana na uongozi wa shirika hilo kulijadili kabla ya kuchukua hatua.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Cairo Mwaitete, alisema chanzo cha tukio hilo kupishana kauli na kusababisha kuwapo kwa majibizano kati ya mwanafunzi na askari huyo.

Alisema tukio hilo lilitokea Novemba 22, mwaka huu katika Ndaki ya chuo hicho cha jijini Arusha.

Kwa mujibu wa Dk. Mwaitete, IAA, imelazimika kutoa ufafanuzi huo kutokana na ukatili uliofanyika baada ya kusambaa kwenye mitandao ya kijamii ujumbe wa video kuhusu mmoja wa wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Arusha, kushambuliwa na kujeruhiwa na askari huyo.

"Na hapa tumekubaliana kuchukua hatua ya kumsimamisha kazi askari husika na mpaka hivi sasa tayari askari husika amesimamishwa kazi mara moja, baada ya tukio hilo," alisema.

Pia wamekubaliana askari husika achukuliwe hatua za kisheria (kiutendaji na kijinai), SUMA JKT kufidia gharama za matibabu pamoja na kutoa fidia ya fedha kwa mwanafunzi husika.

"SUMA JKT wameahidi kutoa tamko la kuomba radhi kwa kitendo kilichotokea cha askari wake kukiuka taratibu za kiutendaji," alisema.

**Pia wamekubaliana askari husika achukuliwe hatua za kisheria (kiutendaji na kijinai), SUMA JKT kufidia gharama za matibabu pamoja na kutoa fidia ya fedha kwa mwanafunzi husika.**

# Masauni aonya urasimu utoaji pasi za kusafiria

**Na Hamida Kamchalla,** MKINGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, ameonya kuhusu urasimu unaoendelea wa utoaji wa hati za kusafiria pamoja na vibali vya makazi kwa wageni katika Mkoa wa Tanga, akiagiza wanaofanya hivyo kuacha mara moja.

Alionya hayo jana, alipokwenda kufunga mafunzo ya maofisa Uhamiaji yaliyokuwa yakifanyika Chuo cha Rafael Kubaga, zamani kikijulikana kama Bomba Kichakamiba kilichoko Wilaya ya Mkinga.

"Kuna malalamiko kutoka kwa wananchi na wageni katika kupata huduma za passport (hati za kusafiria) na vibali kwa wageni.


"Kwa sasa nchi imefunguka, kuna wimbi kubwa la watalii na wawekezaji kutoka nje ambao wanahitaji huduma zenu, lakini bado kuna urasimu katika utoaji wa huduma hizo. Hebu ninyi watu wa Uhamiaji niwaombe mbadilike." Akionyesha kukerwa na urasimu huo, Waziri Masauni, alisema serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa katika mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika uombaji wa hati na vibali vya makazi kwa wageni, hivyo ni lazima watende haki badala ya kufikiria maslahi binafsi.

Kuhusu tatizo la uhaba wa vitendea kazi kama magari, Waziri Masauni, alisema katika bajeti ya mwaka huu, serikali imewatengea Uhamiaji, Sh. bilioni 5.6 kwa ajili ya ununuzi wa magari 30, ambayo yatatumika kurahisisha utendaji kazi wa jeshi hilo.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alisema kumekuwapo na kero ya ongezeko la uingiaji wa wahamiaji haramu nchini, jambo ambalo linaitia hasara serikali ya kuwahudumia.

"Uhaba wa vitendea kazi pamoja na askari wa Uhamiaji kutokuwa na mbinu za kitaalamu za kijeshi za majini zimekuwa zikisababisha wakati mwingine kutofanikiwa katika operesheni za kudhibiti wahamiaji haramu wanapotumia njia za baharini," alisema Mgumba.

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji nchini, Dk. Anna Makakala, alisema kuwa mafunzo kwa maofisa hao yatasaidia kuleta mabadiliko ya kiutendaji na maboresho ya mifumo ili kutoa huduma zinazokidhi viwango vya kimataifa.



# Wanafunzi wahadharishwa matumizi mitandao ya kijamii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI Msaidizi wa Usalama wa Mtandao wa Wizara ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Stephen Wangwe, amewafunda wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), akiwashauri kupunguza matumizi yasiyo na tija kwenye mitandao ya kijamii ili kuepuka athari wakati wanapotafuta ajira.

Akizungumza na wanafunzi hao, Wangwe, alisema serikali inaunga mkono chuo hicho kuanzisha Shahada ya Usalama wa Mtandao, kwa kuwa itawasaidia vijana wengi kutumia vizuri mitandao hiyo, ukizingatia wao ndio watumiaji wakubwa.

"Tumekuja na dhima hii kubwa ya utoaji elimu kwa umma, ikiwamo usalama mtandao kutokana na IAA kuwa na shahada mahususi ya usalama mtandao, ambayo inahitajika zaidi na makundi haya ya vijana ili apunguze athari zinazojitokeza kwenye mitandao na jamii.

"Kwenye mtandao kuna masuala mengi tunayokabiliana nayo, ikiwamo baadhi kufanyiwa uhalifu na kuibiwa fedha zao au kazi. Hivyo sasa tunafungua milango, kwa wanatasnia wa masuala ya TEHAMA kuziba mianya ya uhalifu."

Aidha, Wangwe, alisema mbali na uhalifu huo wamebaini uwapo wa udhalilishaji na utapeli, ambao kupitia TEHAMA wameweka mfumo wa kuwabaini watu hao, ambao wanatumia njia ya udanganyifu, lakini nawaomba vyombo vya Dola kuimarisha usalama zaidi katika mitandao.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa Wizara hiyo, Innocent Mungi, alisema moja ya majukumu ya wizara ni kutoa elimu hiyo ili kutoa tahadhari kwa wanafunzi wanaochukua masomo ya TEHAMA kuhusu umuhimu wa ulinzi wa taarifa zao binafsi ili kuondokana na utapeli mtandaoni.

Nembrice Emmanuel, mwanafunzi wa chuo hicho, alisema amejifunza mengi, kwa kuwa awali walikuwa wakitumia mitandao pasipo kujua athari zake na umuhimu wake.

"Tulikuwa hatujui kuwa kuweka taarifa zetu kwenye mitandao ya kijamii ni hatari hivi, kwani tulikuwa tukitumia teknolojia kila siku pasipo kujua athari zake lakini sasa tunajiepusha na hili," alisema.



Baadhi ya wahitimu wa kidato cha nne wakicheza muziki na wazazi/walezi wao jana wakati wa sherehe za mahafali ya 15 ya Sekondari ya Wasichana ya John the Baptist, Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# TRA yatoa tuzo maalum kwa kampuni ya Coca-Cola

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMPUNI ya Bonite Bottlers Ltd ya Moshi (BBL), inayozalisha vinywaji baridi jamii ya Coca Cola, imepewa tuzo maalum na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kama mlipakodi bora wa ushuru wa forodha.

Mkurugenzi wa Fedha wa TRA, Makao Makuu, Linah Edward, alikabidhi tuzo hiyo jana kwa mwakilishi wa Meneja Mauzo na Masoko wa Bonite Bottlers Ltd, Christopher Loiruk.

"Hawa Bonite wanafanya vizuri na wanalipa kwa wakati, huwa hawasubiri kufuatwa. Tunahimiza wafanyabiashara wengine wafuate nyayo zao. Bila kigugumizi ni mfano wa kuigwa; na mwingine tunayempa tuzo hiyo ya mlipakodi bora wa forodha ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Marenga Investment Ltd, Joseph Kimoso," alisema Linah.

TRA imeeleza jumla ya mashauri 105 yaliyokuwa katika mahakama za kikodi nchini yameondolewa na kupatiwa ufumbuzi kwa maridhiano ya kisheria.

Kwa mujibu wa Linah, mamlaka hiyo itaendeleza jitihada zake za utatuzi wa migogoro na mashauri ya kodi nje ya mahakama kwa njia ya maridhiano ya kisheria ili kuimarisha imani ya walipakodi na kutoa muda wa kutosha kujikita katika shughuli za biashara badala ya kuendesha mashauri ya kodi.

"Katika kuhakikisha tunaendana na mabadiliko ya kiuchumi duniani na ufanyaji biashara, mamlaka inaendelea kujijengea uwezo wa ndani, kwa kuwapatia mafunzo ya watumishi wake kwa njia mbalimbali, ndani na nje ya nchi na kujikita katika eneo korofi la ukwepaji kodi za kimataifa na kodi zinazohusiana na bidhaa za mtandaoni," alisema Linah.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 katika robo ya kwanza kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, mamlaka hiyo imekusanya Sh. trilioni 5.923 ikiwa ni ufanisi wa asilimia 99.1 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 5.978.

Kuhusu biashara ya magendo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alitangaza kuwa kuanzia sasa wakikamata magari na mali za magendo mkoani humo watazitaifisha na kuwa mali ya serikali. Kwa mujibu wa Babu mpaka sasa, katika Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, kuna magari manane na pikipiki yamekamatwa yakiwa na mali za magendo.

"Wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara za magendo waache mara moja. Naelekeza TRA kuongeza juhudi zaidi katika eneo hili la magendo ili kutokomeza tatizo hili ambalo sio la kiungwana kukwepa kulipa kodi. Ongezeni nguvu kwenye mipaka tuwakamate, tukishawakamata watu wanne, watano, wengine watajifunza," alisisitiza.

# Wadau wa elimu wakutana kujadili uboreshaji sekta hiyo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WADAU wa elimu katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, wamekutana kujadili namna bora ya kuweka mpango mkakati wa pamoja wa kuboresha na kuendeleza sekta hiyo, bila kuathiri sheria na sera.

Akizungumza jana na wadau hao, Katibu Tawala Wilaya ya Arumeru, James Mchembe, alisema serikali imetoa fursa kwa asasi za kiraia kushiriki katika utekelezaji wa mpango huo kwenye sekta ya elimu, kwa kuwa kuna mahitaji yasiyoendana na uwezo wa kirasilimali.

Alisema asasi hizo ni kiungo cha msingi katika kutekeleza vipaumbele vya serikali vya kutoa huduma za jamii kisekta huku akisisitiza kuwa serikali inatekeleza majukumu yake, lakini mafanikio ya elimu yanapewa nguvu na wadau hao.

"Serikali ina thamini kazi zenu mnazozifanya hivyo kwa niaba ya serikali, natumaini matokeo ya kikao kazi hiki, yatakwenda kutoa suluhisho na dira ya utatuzi wa matatizo ya elimu, kwa lengo la kuwakomboa watoto wetu kupitia elimu," alisema Mchembe.

Aidha, Mratibu wa Miradi wa Shirika la ACE Africa, Bugesi Matayo, alisema wazazi wamekuwa na mawazo potofu juu ya sera ya elimu bure na kujiweka pembeni na kuacha kuwahudumia watoto wao, hasa kuchangia chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa.

Vilevile, alisema wamekubaliana kukaa na uongozi wa halmashauri hiyo, kupanga mipango hiyo, kwa ajili ya mwaka ujao wa masomo, ukiwa na lengo la kuboresha sekta ya hiyo na kutatua matatizo yanayowakabili wanafunzi shuleni.

Katika kikao kazi hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Selemani Msumi, aliziomba asasi hizo kutochoka kuisaidia jamii hususani watoto ambao wanaoandaliwa kulitumikia Taifa na ili ndoto zao zitimie katika maisha yao kupitia elimu.

"Tunafahamu elimu ni msingi wa maisha, mna jukumu la kushirikiana na serikali kuhakikisha watoto wanapata elimu bora, katika mazingira mzuri bila kuwapo kwa vizuizi kwa kuwa tukiungana tukawa wamoja tutafanikiwa kusukuma mbele gurudumu la maendeleo," alisema.

Nipashe
TESA
Jumanne Novemba 29, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



MZURI ISSA ALI
Mwanahabari aliyeacha kazi Ikulu kwenda kutetea wanawake, watoto

Ukurasa 15



Mtaalamu wa saikolojia ataja umri sahihi kuanza kumfundisha mtoto

Ukurasa 17

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

### SIKU 16 KUPINGA UKATILI KIJINSIA

# MA-DC wanapopambana kumchomoa binti mikononi mwa 'mwanaume' tapeli

• Alimtorosha shuleni kumuoa, arudishwa darasani



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Jasinta Mboneko akizungumza kwenye kongamano la masuala ya wanawake. **PICHA: MAKTABA**

WAKUU wa Wilaya, Jasinta Mboneko wa Shinyanga na Tanganyika, Salehe Mhando, wameandika historia kwa kushiriki na kufanikisha kumwokoa binti, aliyetoroshwa siku chache kabla ya kufanya mtihani wa kidato cha pili.

Ni msichana wa Sekondari ya Solwa wilayani Shinyanga (jina tunalo), anayeeleza kuwa Oktoba 28, mwaka huu, alinusurika kukwama kufanya mtihani wa kidato cha pili, baada ya kutoroshwa kwenda Mpanda mkoani Katavi kuozwa.

Akiwa na miaka 16, anaelezea tukio hilo, akisema anapenda shule, lakini kutokana na sekondari anayosoma kuwa mbali alirubuniwa akaingia kwenye mtego na kisha kutoroshwa kwenda kuolewa.

Anaelezea kuwa siku zote anatumia baiskeli kwenda shule iliyoko kilomita 20 na baiskeli inapoharibika anashindwa kuitengeneza kutokana na kukosa fedha ndiyo sababu ya kukumbana na vishawishi vya wanaume wakimtaka kimapenzi.

"Nilikuwa nimekata tamaa kuendelea na msomo sababu ya kusoma mbali, japo napenda nisome," anasema akimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko kwa kumwokoa asiolewe.

"Ndoto zangu ni kuwa mwalimu, na sasa nakwenda kuzitimiza na nitasoma kwa bidii sababu naishi hapa shuleni," anaongeza.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Solwa, Leonard Adamu, anasema wanafunzi katika shule wana utoro kwa sababu ya kutembea umbali mrefu.

Akizungumzia binti aliyetoroshwa anasema walibaini mwanafunzi huyo wa kidato cha pili kutokuwapo shuleni wakati wakifanya maandalizi ya kuwapanga kwa ajili ya mitihani na walipomfuatilia ikagundulika kuwa ametoroshwa kwenda Mpanda.

Anasema baada ya kujua hilo, aliwasiliana na viongozi wa kata kisha taarifa hizo akapewa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta ili aongeze nguvu za kumwokoa mwanafunzi huyo arudi kufanya mtihani na kutimiza ndoto zake.

"Tunashukuru mwanafunzi aliokolewa kwa wakati na akafanya mtihani wake wa kidato cha pili," anasema Adamu.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anasema baada ya kupata taarifa za mwanafunzi huyo kutoroshwa kwenda kuozwa aliwasiliana na Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Salehe Mhando, ili kumfuatilia na kukamatwa lakini muoaji akakimbia.

Anasema juhudi zilifanikishwa na wasamaria wema waliowafikishia polisi taarifa na kwamba alikaa siku moja na ya pili akarudishwa shuleni. Na kwamba alipandishwa gari na kijana aliyemtorosha ambaye ametoroka.

"Nilipopewa taarifa tu juu ya mtoto huyu kuwa ametoroshwa, siku hiyo hiyo nilifanya mawasiliano ya haraka na tukawakamata na kumrudisha mtoto huyu haraka shuleni na akafanya mtihani," anasema Mkuu wa Wilaya.

**CHINI YA UANGALIZI**

"Mwanafunzi huyu kwa sasa yupo chini ya serikali na anaishi na mwalimu shuleni hapa, na haruhusiwi kwenda likizo kwa wazazi wake, bali wanatakiwa kuja hapa shuleni kumsalimia na nitamsimamia hadi afike chuo kikuu na kutimiza ndoto zake," anaongeza.

Anasema kutokana na tatizo la umbali mrefu wa shule tayari serikali imeshatoa Shilingi milioni 160 kwa ajili ya kujenga shule mpya yenye vyumba vya madarasa nane na itaanza kutoa elimu mwakani.

"Umbali mrefu ni changamoto unawakwamisha wanafunzi wa kike na ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha za kuanzisha shule mpya ya sekondari, ili wanafunzi wasome karibu," anaeleza Mkuu wa Wilaya.

INAENDELEA UK. 18

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

## SIKU 16 KUPINGA UKATILI KIJINSIA

# Taifa liwatambue kwa tuzo watetezi wa haki za wanawake na watoto

• Bila juhudi zao usawa kijinsia, unapuuzwa na kukwamishwa

AZIMIO la Umoja wa Mataifa (UN) la watetezi wa haki za binadamu 1998, linawatambulisha kuwa ni watu binafsi au vikundi vinavyofanya kazi ili kukuza, kulinda au kujitahidi kwa ajili ya ulinzi na utambuzi wa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi kwa njia za amani.'

Aidha, halijawasahau kinamama likielezea kuhusu watetezi wa haki za binadamu za wanawake (WHRDs), likiwatambulisha kuwa ni wanawake na wasichana wanaofanya kazi ya kukuza au kulinda na kuendeleza haki za binadamu wanawake.

Kwa Tanzania WHRDs ni wengi na kazi zao katika kutetea kuwapo usawa wa kijinsia na ulinzi wa haki za kinamama hauwezi kuacha au kusahau mchango wao mkubwa.

Lakini, leo ni vyema kuwataja wachache wakiwamo wanahabari wanawake, ambao pengine bila juhudi zao masuala yanayohusiana na usawa wa kijinsia nchini yangeweza kupuuzwa na hata kukwamishwa zaidi.



Dk.Ananilea Nkya



Profesa Penninah Mlama



Rebecca Gyumi.

Leo dunia inapoadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Binadamu za Wanawake, wanahabari hawa na kinamama wengine wanakuwa na nafasi ya kipekee nchini. Mathalani, timu ya wana TAMWA ikiongozwa na Leyla Sheikh, Pili Mtambalike, Annanilea Nkya, Edda Sanga walipiga kambi kusimama na wadau wengine wakiwamo wanasheria wanawake TAWLA kusukumu kupitishwa sheria ya makosa ya kujamiiana maarufu kama SOSOPA, mwaka 1998 kupinga ukatili ndani ya ukeketaji na ubakaji.

Pamoja na sheria hiyo juhudi za wanahabari hao na WHRDs zimewaondoa kinamama wengi kwenye unyanyapaa na mitazamo hasi ambayo kwa miaka mingi, imewaathiri kiafya, kisaikolojia na hata uwezo wao wa kufanya kazi kwa ufanisi.

Ni wazi utetezi wa haki za wanawake kwenye media ni lazima uanzie na kusoma ili kuwa na ujuzi na weledi kwenye uandishi.

Akiwa Mkurugenzi wa TAMWA, Ananilea Nkya, miongoni mwa WHRD anatambua umuhimu wa kupanda mbegu ya 'usawa wa kijinsia leo kwa ajili ya maendeleo ya kesho, kuanzia 2007 anaanzisha Scholarship ya TAMWA kusomesha wanahabari wanawake, akiamini kuwa lazima kuchukua hatua kuwalinda, kuwaendeleza kitaaluma wanahabari wanawake ambao ni shina la WHRDs.

Ndiyo wanaotumia kalamu, vipaaza sauti kwenye redio na televisheni na hata kwenye majukwaa mengi ya mitandaoni kutetea haki za wanawake.

Leo wanawake wanahabari wamesoma kupitia Scholarship ya TWAMWA, wakiwamo Salome Kitomari Mwenyekiti wa Bodi ya MISATAN, mwandishi wa makala hii, Dk. Rose Reuben Mkurugenzi wa TAMWA, yupo pia Amina Mollel aliyewakuwa mbunge viti maalumu.

**KUFICHUA UNYANYASAJI**

Wanawake wanahabari ambao ni mdomo wa WHRDs wamefanyakazi kubwa ambazo zipo kwenye ajenda za kitaifa, mfano TAMWA kwa miaka yote imeibua unyanyasaji na mauaji ya wanawake wazee mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Maelfu ya bibi na wanawake wenye umri wa makamo wameuawa wakisingiziwa kuwa ni wachawi, imeripoti taarifa hizo kwenye media za kitaifa na kimataifa. Aidha, imekemea ukeketaji wanawake, watoto wachanga na wasichana wa mikoa ya Manyara, Arusha, Dodoma, Mara, Singida na Kilimanjaro.

Imeibua mikasa ya ndoa na mimba za utotoni, kutembelea na kuandika taarifa za mikoa iliyokuwa na mila hilo.

Kazi za wanahabari na watetezi wa haki za wanawake zimefikia hatua za juu hata kimataifa kwa kutafiti na kuitambua mikoa inayoongoza kwa unyanyasaji watoto kingono na kusababisha ndoa na mimba utotoni.

Mfano Utafiti wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kutetea Watoto UNICEF wa 2012, unaitaja mikoa inayoongoza kwa ndoa za ututoni ukitajwa Shinyanga wenye asilimia 59, Tabora 58, Mara 55, Dodoma ni wa nne kwa asilimia 51 na Lindi ni wa tano kwa asilimia 48.

Pamoja na ndoa ipo mikoa inayoongoza kwa mimba kwa mabinti, ni pamoja na Shinyanga, Tabora, Mara, Dodoma, Manyara, Lindi na Mtwara ni wazi kuwa wadau kama UNICEF, WHRDs na waandishi wa habari wanawake ni muhimu kwa maana kazi zao zinavyoendelea kulinda wanawake na kama hazitaibuliwa ukandamizaji hautamalizika.

Pia wadau hawa ni muhimu kwa vile wanaikumbusha serikali na watunga sera umuhimu wa kuangalia sheria kandamizi zinazoumiza wasichana mfano Sheria ya Ndoa mwaka 1971.

Hapa ndipo Rebecca Gyumi, anapotinga ulingoni, leo taifa linapoadhimisha siku ya WHRD, ana nafasi ya kipekee, kwa vile hakukaa pembeni, akiangalia haki za kinamama zikivunjwa.

Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, asasi inayolenga kumwezesha na kumpa nafasi mtoto wa kike kwa njia ya elimu na kutatua changamoto zinazozuia haki ya mtoto wa kike kupata elimu, anasimama kubomoa Sheria ya Ndoa ya 1971.

Anatinga Mahakama Kuu, kupinga kifungu cha 13 na 17 cha Sheria ya Ndoa, sura ya 19, kinachoruhusu wasichana kuozwa wakiwa na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi na miaka 14 kwa idhini ya mahakama na kutaka marekebisho kuondoa vifungu kandamizi.

Wakati huo akiwa na miaka 31, anapingana na mfumo wa sheria wa nchi unaowakandamiza watoto, ameshinda na kufanya mageuzi ya kihistoria mwaka 2016 na sasa wanawake wanategemea serikali ipandishe kisheria umri wa kuolewa uwe zaidi ya miaka 18.

Rebecaa WHRD anapata Tuzo ya Kimataifa, anayopewa na UNICEF, akitajwa kuwa Mwanamke wa Mwaka wa 2016, aidha Desemba 2018, pia anajipatia Tuzo ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa.

Aliposhuhudia watoto wa miaka 13 wakiozwa tena wengine wakiwa ni wanafunzi wenzake,waliokatisha masomo baada ya kupata mimba alianza mapambano na hata wewe mama, binti, msichana chukua hatua kupinga na kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

.Ndiyo wanaosaidia kuikumbusha serikali ya Muungano na ya Zanzibar pale inaposhindwa kutimiza wajibu wake wa haki za binadamu na za wanawake, pamoja na watoto kwa kuweka mizani na mikataba ya kitaifa ambayo nchi imeridhia na sheria mbalimbali inayolinda haki hizo.

WHRD kama Rebecca ni muhimu kukumbusha na kutoa mapendekezo kwa serikali na wadau kama, wafanyabiashara, wakulima, waajiri, wenye viwanda kuhakikisha ulinzi wa haki za wanawake, watoto na makundi ya wanyonge ili wawe na mazingira bora ya kuishi na kumudu maisha yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Wanawake Tanzania Trust (WFT-Trust), Mary Rusimbi, ni miongoni mwa wanaodhimishwa leo, anafanya kazi mchana na usiku kuwezesha wanawake kujiamini na kuendesha maisha yao.

Mary mwanachama na mwanzilishi wa mashirika ya uwezeshaji na utetezi wa haki za wanawake mfano Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Mwaka 2016, Profesa Peninah Mlama, anapokea Tuzo ya UNICEF ya Change Maker, akiheshimiwa kwa kazi kubwa ya kuwezesha wasichana Tanzania na Afrika pia. Ndiye Ofisa Mkuu Taaluma wa Kwanza , Afrika Mashariki na Kati, akifanyakazi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ni msomi 'aliyeinjinia' programu ya ujumuishaji wa jinsia (gender mainstreaming) UDSM. Ni wa kwanza kuhimiza wasichana wapewe nafasi maalumu ya kujiunga na chuo hata kama ufaulu ukipungua kidogo.

Anatambua kuwa tofauti na wavulana wana vikwazo vingi japo wana uwezo, ndipo anaanzisha utaratibu wa kuwafundisha tena, kuwapa mitihani na wengi wanafaulu na kudahiliwa vyuoni, ni juhudi za kutaka kina mama wapate haki ya kusoma elimu ya juu na kutumikia taifa kama madaktari, wanasayansi, wahandisi na wahadhiri wa ngazi mbalimbali.

ELIMU

NA SALMA SHAALI, ZANZIBAR

### SIKU 16 KUPINGA UKATILI KIJINSIA

## MZURI ISSA ALI

# Mwanahabari aliyeacha kazi Ikulu kwenda kutetea wanawake, watoto

• Alidharauliwa, kukataliwa, kunyimwa chakula

"NILIAMUA kutoka serikalini nikiwa Ikulu na kuingia katika Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) kwa sababu nilijiona nitakuwa na nafasi ya kuwazungumzia zaidi wanawake. Niliamini wananihitaji zaidi kuliko ninavyohitajika serikalini," anasema Dk. Mzuri Issa Ali, Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA Zanzibar, akiongoza kwa miaka 20 sasa, tena akianza jukumu kwa kujitolea bila mshahara.

Bila shaka uamuzi huo wa kuondoka Ikulu kuhangaikia matatizo ya wanawake na watoto vijinini uliwaacha wengi midomo wazi, kwa vile alikuwa na uhakika kimaslahi na fursa bora.

Leo Wazanzibari wana kila sababu ya kusema Dk.Mzuri ni mwanamke wa kuigwa kwani amefanya makubwa yasiyotegemewa kwa kuleta maendeleo katika jamii na nchi pia.

"Ni mpambanaji, shupavu na jasiri anayetoa muda mwingi kufanyakazi ili haki za wanawake na watoto zizingatiwe," anasema Sophia Ngalapi, mfanyakazi wa TAMWA Zanzibar.

Anamsifu kwa kazi kubwa ya kuwainua wanahabari wachanga ili wasimame na kuimudu taaluma wakiripoti habari zinazojenga usawa kati ya wanawake na wanaume na ulinzi wa haki za wanawake na watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa TAMWA, Dk. Ananilea Nkya, anamtaja Mzuri kuwa ana sifa zote muhimu za uongozi bora ndiyo sababu, uongozi wake umeleta mafanikio kwa Wazanzibari na wanahabari.

"Sifa za kiongozi bora ni uaminifu, uchapakazi, maono na uwezo wa kuwasiliana na kujenga mahusiano na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi serikalini, wanahabari na jamii ili uweze kufanikiwa," anasema Dk. Ananilea na kuongeza;

"Ukitazama mafanikio ya miradi inayohusu haki, usawa na ustawi wa wanawake kiuchumi Mzuri alibuni na kuisimamia utekelezaji wake utabaini ni kiongozi wa kuigwa.'"

Anataja mradi wa Women Empowerment in Zanzibar (WEZA), akisema umeondoa maelfu ya kaya kwenye ufukara na kuziepusha na ukatili wa kijinsia kama kuzuia ndoa za utotoni



Dk. Mzuri Issa Ali

zilizowakwamisha wasichana kielimu tofauti na wavulana.

"Kwa kujitolea, uaminifu uliotukuka, Dk. Mzuri ameijenga TAMWA Zanzibar kuwa taasisi bora ikiwa na ofisi iliyojengwa kwa nguvu za wafanyakazi na wanachama," anadokeza Dk. Ananilea.

Anaungwa mkono na Ofisa Uhusiano wa TAMWA, anayesema: " Dk.Mzuri alikuja na wazo la kujenga na kuifanya TAMWA Zanzibar kuwa taasisi inayojiletea maendeleo yenyewe akishirikiana na wana TAMWA anasimamia jengo linaloelekea kukamilika, itaendelea kubaki kumbukumbu kuu ya uongozi wake".

Utendaji wake unafuta dhana ya zamani kuwa mwanamke hawezi kufanyakazi kama mwanaume kutokana na fikra za mfumo dume ndani ya jamii ni jambo la kujivunia kwa TAMWA, wakati wa uongozi wake TAMWA yeye ni mwanamke kutoka familia maskini aliyeishi maisha yaliyojaa dhiki, dharau, kashfa na misukosuko ambayo huenda mimi au wewe tusingeweza kukabiliana nayo, lakini ameweza.

**KUPIGANIA ELIMU**

Mzuri anaamini kuzingatia elimu akisema ndiyo ufunguo wa maisha, wakati wote wa uongozi akishirikiana na wenzake Zanzibar na Bara walianzisha na kuendesha mfuko kusomesha wanachama chuo kikuu na kunufaisha wengi.

"Kiukweli sitasahau fadhila alizonitendea dada yangu, ni miongoni mwa watu walionisaidia kutimiza ndoto zangu alinisomesha kuanzia kidato cha pili 2007 hadi mwaka 2016 nilipomaliza chuo," Arafa Abdallah Juma mdogo wake Dk. Mzuri, anakumbusha.

Licha ya changamoto alizokumbana nazo hakuwahi kukata tamaa, badala yake alijipa matumaini na kuwa na ari ya kutaka kuwakomboa wanawake jambo analolienzdeleza hadi leo.

Maisha ya Mzuri yalikuwa ya umaskini yaliyojaa dhiki ambayo imemwezesha kuwa jasiri, mpambanaji na anayesimama na kupambania haki za watu hasa wanawake.

"Alianza kupenda kujitegemea tangu mdogo, nakumbuka alinishauri tufanye biashara ya maandazi na alikuwa akinisaidia kazi na hata kabla ya kwenda shuleni," anasema Mgeni Hemed Seif, mama mzazi wa Mzuri na kuongeza kuwa biashara hiyo ilimlipia ada, vifaa vya shule na kodi ya nyumba.

**SAFARI YA UONGOZI**

"Ndoto yangu ilikuwa ni kusoma ili nisaidie wazazi, ndugu na jamii yangu. Nilitamani sana kuona wanabadilika na kuondokana na mifumo, mila na sheria kandamizi kwa mwanamke," anasema Mzuri na kwamba mwaka 1997 alimaliza kidato cha sita Sekondari ya Lumumba, muda mfupi baadaye alipata kazi Gazeti la Nuru au sasa Zanzibar Leo.

Baadaye alihamishiwa serikalini mwaka 2008, akifanya kazi Ikulu akiwa Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano, akishughulikia kutengeneza kalenda na jarida la Ikulu, hata hivyo, anasema alihisi kuwa serikalini ni rahisi kupata mtu wa kuziba pengo lake, akaamua kujiunga na TAMWA anakohudumu hadi sasa.

Anamtaja mwanahabari mwanamke mchapakazi Dk. Ananilea Nkya, kuwa ndiye aliyemshauri kuingia TAMWA , akiwa mshauri wake, akimsifu Mzuri kwa namna alivyofanya kazi kwa uzalendo, akiandika habari zinazohusu masuala ya wanawake kwa kujitolea na kwa ueledi.

"Nilimwona kuwa ndiye mwanaTAMWA mwenye nia na moyo wa kuijenga TAMWA Zanzibar kwa sababu wakati niliposailiwa kuwa Mkurugenzi wa TAMWA Septemba 2001 tulikuwa hatuna ofisi Zanzibar, nami nililiambia jopo lililonisaili kwamba maono yangu ni kuona uwepo wa TAMWA imara Zanzibar yenye kubeba sauti ya wanawake na watoto".

**CHANGAMOTO**

Kila jambo utakalolifanya linaweza kukabiliwa na vikwazo na kwa Mzuri ni vingi ikiwa ni pamoja na kuishi katika mazingira magumu, masimango na mateso yote yakisababisha kufanya biashara akiwa mdogo.

"Nilinyanyasika hadi kutaka kujitupa baharini kwa vile kila mtu hakuwa tayari kuishi na mimi. Kwa mfano kuna kipindi nilihamishiwa kwa shangazi yangu, hakunitaka ikabidi nipelekwe Pemba nako hawakutaka kuishi na mimi, nilirejeshwa Unguja kule kule ambako nilikuwa sitakiwi," anaongeza zaidi Mzuri:

"Nilichukuliwa kama mfanyakazi wa ndani, nililazimika kufanya kila kitu lakini hata chakula sikupewa. Nililazimika kumsaidia kazi jirani yetu aliyekuwa akifanya biashara ndogo ndogo ili angalau nipate chakula." Anakumbusha.

**KUSONGA MBELE**

Kwa kuwa alikusudia kuona haki na usawa vinatendeka kati ya wanawake na wanaume, alijifunza namna ya kufanya kazi na kujua mambo mengi yanayowahusu japo alijua mengi kupitia maisha aliyoishi.

Anawasifu wazazi wake kwa kumuunga mkono kwa kila hatua aliyokuwa akiipiga, licha ya hali ngumu waliyokuwa nayo na baada ya kuingia kwenye ndoa mume wake, anampa ushirikiano mkubwa ili afanikiwe kwenye majukumu yake ya kiuongozi.

Licha ya kuwa kiongozi anayetegemewa na jamii, bado anatimiza majukumu yake akikaa na familia yake, kukagua madaftari ya mtoto na kufuatilia kazi zake za shule.

"Mama yangu alianza kufanya kazi TAMWA tangu mimi nilipokuwa mdogo lakini sijawahi kuona tofauti katika malezi yake kwani amekuwa mstari wa mbele katika kunielekeza namna ninavyotakiwa kuishi na watu, kiukweli najivunia sana kuona mama yangu amekuwa ni mwanamke wa kuigwa na jamii. Inanipa hamasa yakutaka kuwa kama yeye," anasema Rabia Abdi Khamis mtoto wa Dk. Mzuri.

Dk. Shaaban Issa Muhammed ni mume wa Mzuri, anaeleza namna anavyopenda utendaji kazi wa mke wake, akisema anapenda usawa wa jinsia zote husussan wanawake, anapenda uadilifu pamoja na kuona watu wengine wakifanikiwa zaidi, pia anajituma tena sio ofisi tu hata nyumbani anapenda kuzungumza kwa busara akifanya majukumu yake kama yanavyomlazimu.

"Panapotokea dharura yeyote ananipa taarifa kama kuna msaada wa mawazo tunajadiliana kwa pamoja ili kuona yanafikia muafaka wa jambo hilo".

Mzuri anataka jamii ibadilike na kuondoka na mfumo dume, kwa kuweka usawa wa jinsia, kuwa waadilifu na wanawake kuwa vipaumbele katika kushiki nafasi za uongozi kitendo ambacho kitasaidia kupaza sauti zao kwa ajili ya kuzungumzia changamoto zinazowakabili.

SAYANSI

**NA BONIFACE GIDEON, TANGA**

STERM PARK & VIJANA...

# Neema ya miaka miwili, kituo pekee nchini kinachokuzia vijana sayansi

• Darasa shuleni na kituoni; nyumbani 'Kilimo Janja'




Wanafunzi wa Sterm Park, jijini Tanga wakiwa katika mjumuiko wao. **PICHA ZOTE: BONIFACE GIDEON**

WAKATI dunia sasa ni ya kisayansi, nchi za dunia ya tatu zikiwamo za Afrika Mashariki, sasa ziko katika safari kuendeshwa kisayansi, ingawa bado hazijajitosheleza.

Jijini hapa kuna hatua ya kituo cha kisanyansi kiitwacho Stem Park Tanga kilichoanzishwa na serikali hivi karibuni, kwa kushirikiana na wadau, ikiwa na dhamana ya kuwatafuta wanasayansi popote walipo, inawajengea uwezo wa nadharia na vitendo, kisha kinawalea mpaka mafanikio.

Taarifa ya kituo hicho kilichoko Chumbageni jijini hapo, inasema matarajio ni sura ya mafanikio kuonekana, kwa wanasayansi wachanga wanaopatikana, tangu Mei mwaka 2020 kilipoanzishwa, kuwapo wanafunzi 9,000.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi sasa kuna zaidi ya wanafunzi 120 walioingia kambini kufundishwa namna ya kutatua matatizo mbalimbali ya kijamii, kwa kutumia sayansi ikiwamo; kilimo janja, mahesabu na uhandisi na wametoa matokeo makubwa.

Inatajwa kuwa aina ya majibu yanayoisaidia jamii kutatua changamoto zinazoikabili jamii, hasa katika kupata majisafi na salama, kilimo cha kisasa maarufu 'Kilimo Janja.'

**WAZO LA KUASISI**

Mmoja wa wakurugenzi waanzilishi wa kituo hicho, Dk.Lwidiko Edward, anasema kufanikisha ujenzi wa kituo hicho, Halmashauri ya Jiji la Tanga iliwapa eneo la ujenzi ambacho baada ya kukamilika, ujenzi ukafanyika na kukamilika mwaka 2000.

"Kituo hiki kipo chini ya usimamizi wa (taasisi) Project Inspire', kwa kushirikiana na wadau, ikiwamo Halmashauri ya Jiji la Tanga, Botnar Foundation na tunao ndugu zetu serikali ya Marekani ambao ndio wafadhili wakuu," anaeleza Dk.Lwidiko

Kuhusu mfumo unaotumika kuwapata wanasayansi, anafafanua: "Baadhi ya mbinu tunazotumia kuwapata wanasayansi wachanga kwanza tuna utaratibu wa kutembelea shule kwa shule, tunawafundisha kwa vitendo zaidi huko shuleni ili kuwahasisha wanafunzi waje kituoni.

"Pia tuna utaratibu wa kambi ambayo wanafunzi wanakuja kwa idadi maalumu, wanakaa kwenye kambi kwa muda fulani na baada ya hapo, wakimaliza mada husika wanarudi kwao na utaratibu wa mwisho ni huru, mtoto yeyote kuja kituoni muda wowote kujifunza sayansi," aeleza Dk. Lwidiko.

Mkurugenzi huyo anaeleza: "Kituo hicho kina walimu ambao ni wanasayansi na mwanafunzi anaruhusiwa kwenda muda wowote kujisomea, mwanafunzi anaruhusiwa kuja hapa muda wowote na wengi wao wanashinda hapa.

"Kituo hiki kila kitu kuanzia vitendea kazi, hadi walimu wa sayansi ambao nao ni vijana wadogo pia tunawajengea uwezo walimu ili wawe na mbinu bora za kufundishia wanafunzi na kuhamasisha wanafunzi wapende sayansi."

Kimsingi, ni kambi inayolenga kuwajengea uwezo hasa wanafunzi wa sekondari kuwa na uwezo wa kutumia sayansi katika utatuzi wa changamoto za kijamii, pamoja na kuwahamasisha kupenda sayansi.

"Lengo letu ni kuhamasisha kubadilisha utamaduni wa kujifunza masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na mahesabu, lakini kwa kambi hii zaidi tutaangazia kwenye Sayansi ya Kilimo cha Kisasa (Kilimo Janja).

"Wanafunzi watajifunza teknolojia ambayo itawasaidia kuwa na uwezo mkubwa katika sekta ya kilimo, ambayo ni muhimu zaidi katika maisha ya binadamu," anasisitiza Dk. Lwidiko.

**WADAU WANENA KILICHOKO**

Ofisa Utamaduni kutoka Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania, Chad Morris, anasema ni huo ni muhimu kitaifa, kutokana na uhalaisia wa dunia inayokabiliwa na mabadiliko mengi na ya kasi, huku uhitaji wa kisayansi ukiongezeka kila siku.

"Wanasayansi duniani kote wanaandaliwa tokea wakiwa wadogo kiumri na kiakili, hadi wanakuwa wakubwa kiumri na kiakili na sisi Marekani tuliliona hilo," anasema Morris.

Anafafanua kuwa serikali ya Marekani imetoa fedha za ujenzi na maendeleo ya kituo hicho, lengo letu sisi ni kuhakikisha Tanzania inapata wanasayansi wengi zaidi watakaoisaidia nchi baadaye.

Ofisa huwa Kimarekani, anaahidi kwamba, serikali yao itaendelea kutoa mchango kwa Tanzania, kuhakikisha inakuwa na vituo vingi zaidi vya sayansi vitakavyosaidia kupata wanasayansi wengi zaidi baadaye.

Baraka Chaula ni mwanafunzi kidato cha tatu kutoka Shule ya Sekondari Tanga Ufundi, mchepuo wa PCB (Fizikia, Kemia na Baolojia), anasema kwa muda mfupi aliokaa kambini hapo kujifunza kutatua matatizo, amejifunza na tayari kuna baadhi ya mambo ana uwezo wa kuyatatua mwenyewe.

"Mfano 'ishu' ya majisafi na salama na masuala ya 'Kilimo Janja' mimi kwa sasa nina uwezo wa kuifundisha jamii," anaeleza na kuongeza:

"Mimi mwenyewe nina uwezo wa kwenda kuanzisha 'Kilimo Janja' na nikawa mfano katika jamii. Nashukuru uwepo wa kituo hiki, kimenisaidia kuongeza kiwango cha uelewa."

Pia mwanafunzi huyo anawatoa hofu wenzake akiwatamkia kuwa "sayansi sio ngumu, bali dhana ya kuogopa ndiyo kikwazo, kwa kuwa wanafunzi na jamii wanatishana mtaani, kabla hata mwanafunzi hajasoma.

"Wanafunzi wengi wanaikimbia sayansi, kwa sababu jamii inayowazunguka inawatisha juu ya ugumu watakaokutana nao, hususani kwenye mitihani yao. Hivyo, mwanafunzi analazimika kuwekeza nguvu zake kwenye masomo mengine ambayo ana uhakika wa kufaulu kwa urahisi zaidi.

"Mimi niwatoe hofu sayansi sio ngumu na mtazamo ubadilike. Lakini, kwa wanafunzi wenzangu niwaambie tu kuwa sayansi inahitaji mazoezi kila siku na muda wote ndio unaweza ukafaulu vizuri," anasisitiza mwanafunzi Chaula.

Pia wazazi wa watoto wanaosoma katika kituo hicho, wanasema kuna mabadiliko makubwa, ililinganishwa na hapo awali. Mzazi Mary Joseph, ana maelezo: "Mwanangu kwa sasa ana uwezo wa kupima na kutibu maji na anakuja na matokeo makubwa.

"Mengine naona amelima vitalu vitatu vya mboga, 'anasema - sema' mwenyewe ni mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya masomo yake ya sayansi ya kilimo. Pia mwanangu muda wote yupo 'bize' sana na kumpata nyumbani ni usiku, muda wote yupo kituo cha sayansi. Mimi kama mzazi, najisikia fahari sana kwa hili."

Salim Mbilinyi, ni mzazi mwingine, anayeungana na simulizi ya kuhisi fahari watoto wao kusoma sayansi muda wote, hususan katika kituo pekee cha sayansi nchini.

"Ni matarajio makubwa sana kwa miaka kadhaa ijayo, nchi itakuwa na wanasayansi wakubwa kwetu. Uwepo wa Kituo cha Sayansi pekee Tanzania katika mkoa wetu (Tanga), sisi kwetu ni fahari kubwa sana na tunaahidi kutoa ushirikiano mkubwa muda wote serikali inapohitaji watoto wetu," anahimisha mzazi, Mbilinyi.



Wanafunzi wakipata maelekezo ya mafunzo kwa vitendo katika kituo cha kisayansi cha Sterm Park, Tanga.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Mtaalamu wa saikolojia ataja umri sahihi kuanza kumfundisha mtoto

•Ukimkorofisha mjamzimto, umemtibua mtoto tumboni



Mwanasaikolojia Khadija Mhenga akitoa elimu kuhusu malezi ya mtoto. **PICHA: SABATO KASIKA**

"MTOTO huzaliwa ubongo ukiwa mtupu, hana tabia yoyote, ni mfano wa karatasi nyeupe ambayo haina chochote, sasa hapo ndipo utakapoanza kuchora au kuandika tabia, kiwe kizuri au kibaya. Ni kazi unayofanya kama ni mzazi, mlezi tena ukisaidiwa na ndugu, majirani, runinga, redio na simu za mkononi."

Ndivyo anavyoanza kueleza Khadija Mhenga, mtaalamu wa saikolojia, akizungumza katika mafunzo ya malezi kwa watoto katika semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), jijini Dar es Salaam, ikiandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kushirikisha wadau kutoka maeneo mbalimbali ya jijini hilo.

Khadija ambaye ni mtaalamu wa masuala ya ustawi wa jamii akiwezesha washiriki wa semina hiyo anasema mtoto hafundishwi hisia anazaliwa nazo ndiyo maana akihisi jambo analia, anacheka, akipata shida kooni anakohoa.

Anasema:"Mama akiwa na mimba, ukimkorofisha, umemtibua mtoto pia. Ifikapo miezi saba, mtoto anasikia, usitaje kwa watu jinsi inayoipenda, kama mtoto aliye tumboni ana jinsi tofauti na ile unayoipenda, hukasirika, na akizaliwa atakuchukia," anasema.

Mtaalamu huyo pia anataja kipindi muhimu cha malezi kuwa ni miaka sifuri hadi sita, hapo ndipo mtoto hutengeneza tabia zote ikiwamo upendo kwa wazazi au walezi wake, na kwamba muda huo ukipita, basi tena.

"Kwa kawaida huwa tunashauri kuwa, katika umri huo mtoto asipelekwe shule za bweni, wala kwa bibi, shangazi au kwingineko kama wazazi wake wapo, ni muhimu alelewe na wazazi wake tu," anasema.

Anafafanua kuwa katika umri huo ndipo panapotengenezwa muunganiko wake na wazazi katika malezi bora na kwamba mzazi akikosea hapo, inawezekana baadaye mtoto asiwe na upendo kwa wazazi.

"Katika mazingira hayo, mtoto anaweza kukaa hata muda mrefu bila kumpigia simu mzazi wake, kwa sababu mtoto ameweka muunganiko kwa matron, bibi au shangazi ambaye ndiye amemlea," anasema.

Anaongeza kuwa kati ya miaka miwili hadi mitatu, watoto hupenda kujidekeza, na kwamba wazazi wasiwapige, kwa kuwa huwa wanatengeneza muunganiko wa kuwafanya kuwa karibu na wazazi wao.

**KUMLINDA MTOTO**

Mtaalamu huyo anasema kuna mambo kadhaa ambayo mzazi anatakiwa kuyajua, ili kumlinda mtoto wake dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono unaoweza kukumbana nao.

"Ni muhimu kutambua kuwa unyanyasaji mtoto kingono ni kumshika sehemu zozote za siri, mtoto kumshika mtu mwingine sehemu zozote za siri, kumuonyesha picha za ngono," anasema.

Khadija anaongeza kuwa kumpiga picha zenye mikao ya kingono, mzazi kuvua nguo mbele yake au kumvua mtoto nguo mbele ya watu, yote hayo pia ni unyanyasaji wa kingono dhidi yake.

"Wanyanyasaji wengi ni wanaume, ingawa wapo pia wanawake wachache, wakatili wengi hutengeneza urafiki kwa watoto na kujifanya wanawapenda, lakini si kweli kwamba kila anayempenda mtoto ni mkatili, na pia wakatili wengi hutengeneza mazingira ya kuaminiwa na familia," anasema.

Anafafanua kuwa mara nyingi ukatili huo hutokea kwa siri na kwamba waathirika wengi huwa hawatoi taarifa kutokana na kutishiwa kuuawa na wanyanyasaji au kuua wazazi wao.

"Mara nyingi unyanyasaji huu hufanywa na watu wa karibu ambao tunawapenda na kuwaamini, anaweza kuwa mjomba, baba mdogo, baba mkubwa, marafiki wa familia, wafanyakazi wa familia na majirani," anasema.

**MAMBO YA KUEPUKA**

Anasema watoto ndiyo dira ya baadaye na kwamba kila mzazi au mlezi ana jukumu la kuwalinda kwa kuwaonya kukaa mapajani mwa mtu yeyote, awe mjomba, jirani na wengine, kwa kuwa si salama kwao.

"Epuka kuvaa nguo mbele ya mwanao pale tu anapotimiza miaka miwili, mwambie akupishe unahitaji faragha, usimruhusu kumwita mwanao mchumba au mke wangu na usimlazimishe kutembelea watu," anasema.

Katika ufafanuzi wake, anasema hata awe ni ndugu, si vyema kumlazimisha amtembelee iwapo hataki, na kwamba ikibidi, basi mzazi ahoji kwa upole, kirafiki, ili kujua ni kwa nini mtoto hataki.

"Lakini mzazi au mlezi awe makini iwapo mtoto wake anampenda mtu fulani. Ajaribu kufuatilia tabia za marafiki wa mtoto wake na vitu anavyokuwa navyo kwenye mkoba wake wa shule. Muonye tabia ya kuombaomba," anasema.

Vilevile anawataka wazazi na walezi kuwauliza watoto wao wanaokaa bweni kujua wanalala wangapi kwenye kitanda. Pia wapitie filamu zote hata zile za katuni wajiridhishe kabla watoto hawajaanza kuziangalia.

"Mzazi au mlezi, kumbuka, mtoto wako akimlalamikia mtu yeyote, usikae kimya, fuatilia na umuonyeshe kuwa unaweza kumtetea na kumlinda. Mfundishe jinsi ya kujisafisha sehemu zake za siri anapofikisha miaka mitatu. Mwambie asiruhusu mtu yeyote kumshika huko, hata wewe usizoee," anasema.

**KUUTAMBUA UKATILI**

Herbert George mshiriki wa semina hiyo, anasema kila mzazi au mlezi anaweza kumtambua kirahisi mtoto aliyefanyiwa ukatili, kwamba anaweza kudhoofika kiafya, kuwa na msongo wa mawazo, kukosa usingizi, kutojiamini na kuwa na tabia ambazo mwanzoni hakuwa nazo.

"Bahati mbaya baadhi ya wazazi na walezi ni wakali kupita kiasi, hali ambayo hata kama mtoto amefanyiwa ukatili, hawezi kuwaambia, badala yake atakaa kimya na kuendelea kuumia," anasema George.

Anasema watoto wanakumbana na mambo mengi ya kutisha kuanzia nyumbani, mitaani na hata shuleni, na kwamba wanakosa pa kuyasemea kutokana na wazazi na walezi wanaoishi nao kutowasikiliza.

Rhoda Mdoe mshiriki mwingine, anasema ni wajibu wa wazazi na walezi kujua watoto wao wanapenda nini, kuwafundisha kutambua matendo hatarishi, kujua rafiki zao, kuwasikiliza, kuwapa nafasi ya kujieleza na kuwalea katika imani ya dini.

"Ukiwa mkali kwa mtoto, itakuwa ni rahisi kwa mtu mwenye nia mbaya kumrubuni kirahisi na kujifanya anamjali kuliko wewe, hivyo ongeeni na watoto kwa upendo na kuwasilikiza wanachosema," anasema Rhoda.

Anaongeza kuwa akiona mtoto anapenda kujitenga na wenzake au anamiliki vitu vya thamani kama pesa, simu na zawadi usizojua zimetoka wapi, ushtuke na kuchukua hatua haraka.

## SIKU 16 KUPINGA UKATILI KIJINSIA

# MA-DC wanapopambana kumchomoa binti mikononi mwa 'mwanaume' tapeli

INATOKA UK. 13

Aidha, wilaya imepokea Shilingi milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 45 kwa shule za sekondari wilayani Shinyanga kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani.

Mwalimu Mlezi shuleni hapo Olivia Kalinga, ambaye anaishi na mwanafunzi wa kidato cha pili aliyetoroshwa, mara baada ya kukabidhiwa na Mkuu wa Wilaya, anasema mwanafunzi huyo baada ya kumaliza mtihani wake anaendelea kumpatia masomo ya ziada.

Anasema ameshazoea kuishi naye na sasa ni kama rafiki yake, na anampatia ushauri nasaha ili atoe mawazo ya kuolewa aingize ya kuendelea na masomo ili kutimiza ndoto zake.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo ambaye (jina limehifadhiwa), anasema ameridhia mwanawe abaki hapo shuleni kuishi na mwalimu ili asome karibu na shule na kutimiza malengo yake na kuepushwa na kurubuniwa.

"Nakuja kumtembelea mwanangu hapa shuleni, na kuja pia na chakula ili kumpunguzia mzigo mwalimu pamoja na kumletea mahitaji mengine," anasema.

Ofisa Elimu Kata ya Solwa Wilaya ya Shinyanga, Elizabeth Mapunda, anasema shule hiyo mpya ya Sekondari Solwa itaondoa adha ya kutembea umbali mrefu na wasichana watapunguziwa kama si kuepushwa na vishawishi vya walaghai njiani.

"Wanafunzi wanaposoma mbali na shule ni tatizo kumaliza, wakihitumu wakiwa salama, kwa mwaka huu 2022 kuanzia Januari hadi Oktoba wasichana wawili wa sekondari wameshapewa ujauzito na kuacha masomo," anasema Elizabeth.



Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Solwa wilayani Shinyanga ukiendelea, utawaondolea adha wanafunzi kusoma katika umbali mrefu. **PICHA: MARCO MADUHU**

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Aisha Omary, anasema wilayani humo kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu, wanafunzi wanne wameokolewa kuozeshwa ndoa za utotoni na wanaendelea na masomo.

Anasema serikali kwa kushirikiana na wadau wanaendelea kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii, na madhara ya kuozesha wanafunzi ndoa za utotoni pamoja na utoaji wa taarifa pale wanapoona mtoto akifanyiwa ukatili na ndiyo maana kila siku taarifa zinatolewa na kuokoa wanafunzi kuozeshwa.

Mzazi Mabula Bundala anatoa wito kwa viongozi, kuwa wanapotaka kujenga shule wawashirikishe wananchi kutoa maoni wapi pa kujenga shule na siyo kushirikishwa kwenye kuchimba msingi, huku watoto wao wakilazimika kwenda kusoma umbali mrefu.

"Kuna maeneo mengi ambayo yapo wazi, lakini wananchi hatushirikishwi kutoa maoni wapi shule zijengwe zaidi ya wao viongozi kukaa na kujadili viwanja vya shule zinazojengwa ila sisi tuna shirikishwa kwenye kutoa nguvu kazi tu," analalamika Mabula.

Anasema anaishukuru serikali kwa uamuzi wa sasa waliouchukua wa kujenga shule nyingine mpya ya Sekondari ya Solwa, ili wanafunzi wasome karibu na kuwaondolea adha ya kurubuniwa njiani.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara ya 18 kifungu (a) kinasema kila mtu ana uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake, ibara ya 20 kifungu (i) kinasema kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine na kutoa mawazo yake hadharani.

Diwani wa Solwa, Awadhi Mbaruku, anasema kila ujenzi wanashirikisha wananchi kupitia mikutano ya hadhara, na ambao wanalalamika ni wale wasiohudhuria mikutano.

Anasema katika ujenzi wa shule mama ya Sekondari Solwa, wananchi wenyewe ndiyo waliamua ijengwe mahali ilipo sasa ambapo ndipo panalalamikiwa kuwa ni mbali, na hata shule hiyo mpya inayojengwa sasa wameshirikishwa na kuridhia ijengwe jirani na Shule ya Msingi Solwa.

Anawaomba wananchi wanapokuwa wakiitwa kwenye mikutano wahudhurie ili kutoa maoni yao na kukubaliana kwa pamoja katika ujenzi wa miradi ya maendeleo wapi iwekwe, pamoja na kutoa nguvu kazi.

## WANENAVYO MALENGA

### SHUKA LA KULALIA

Tuonane paradiso, wimbo huo wasogea,
Huko kusiko mateso, japo kwenda twategea,
Punga mkono kwa leso, utakaye kupotea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Ufanyapo maamuzi, kile unachotetea,
Tambua wewe mzazi, wengi wakutegemea,
Jua adhabu ya mwizi, kubaya utachekea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Uache ubinafsi, ya kwako kuegemea,
Cheki ya kwako nafasi, wengi wanakuchekea,
Hao vema wape chansi, shilingi ukichezea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Sisi tumekusikia, unavyojielezea,
Kwa kweli unavutia, vipande kitumegea,
Ila wajipalilia, jamii yateketea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Wengi tuliwasikia, ya kwao wakitetea,
Paradiso kusikia, wimbo kumpelekea,
Wake waliobakia, nyonga zao zalegea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Ulitakia kufikia, boma tukakujengea,
Ni renta umeishia, wengine wamepokea,
Hutaki kujiambia, uendako wapelea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Lakini twajifunzia, akili inajongea,
Pembe ukijivikia, mbeleni zinalegea,
Nta ikashaishia, kichwani zinapotea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Ulivyozipigilia, hadi zikakukolea,
Wengine tulidhania, zitafikia kumea,
Sasa kuangalia, zilipo zinapelea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Ukifa watakujia, mate wakikutemea,
Pale wamekuzikia, viboko utachezea,
Kama utawasikia, kwao mbali potelea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

Kichwakichwa liingia, nasi tukakupokea,
Tulikusihi tulia, we ukatupotezea,
Ni zamu yako kulia, sindano inakolea,
Usipende kujinyonga, kwa shuka la kulalia.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Ripoti uchunguzi ajali Precision inapozidi kuacha maswali zaidi



Ndege ya Precision Air baada ya kutumbukia ziwani hivi karibuni. **PICHA: ALJAZEERA**

KUTOLEWA kwa taarifa ya awali kuhusu ajali ya ndege ya abiria ya shirika la Precision Air iliyotengenezwa Ufaransa, itakuwa fundisho kwa watakaokwenda vyuoni na kuanza kutafuta vianzio vya upelelezi, uchunguzi, taarifa na mawasiliano yake.

Sarakasi ilianza pale ndege ilipoanguka halafu ikajulikana kuwa ni mvuvi kijana Jackson Majaliwa, aliyetumia kasia la kuendesha mtumbwi kuubamiza mlango wa ndege ufunguke abiria watoke, kazi iliyompa fedha, tuzo, elimu na kazi.

Isingehitaji utaalamu wa hisia iwe ni kama binadamu au kama Waafrika ambavyo baadhi watasema, kujua kuwa jambo hilo lingewakera mno wakubwa serikalini , pengine wale wanaokumbuka wakiilinganisha na hadithi ya Robinson Crusoe na watu mbilikimo aliowakuta kwenye kisiwa cha Liliputi.

Ni wazi kulikuwa na jitihada za wazi kuuaminisha umma kitu tofauti katika taarifa rasmi iliyolenga kusema 'simjui mtu huyu,' ila jambo hilo likaleta kizaazaa mitandaoni. Ikabidi serikali ikanushe taarifa hiyo kupitia kwa msemaji wake, licha ya kuwa ilikuwa imetawanywa kama taarifa ya wizara tena yenye kina, si tamko ukurasa mmoja kuweza kutungwa na mtu yeyote anayefahamu kilichojiri.

Upande mwingine wa maelezo ambao pia ulileta taabu si katika uchunguzi ila kutoa taarifa rasmi, ambako wanafunzi wataaluma ya habari watakuwa wamepata picha ni vikwazo gani vinaambatana na suala zima la utoaji taarifa.

Ilionyesha wazi kuwa kuna tofauti kati ya kile kilichopo na kile kinachohitajiwa kusikilizwa au kusikika, hali ambayo itakuwa imeleta taabu katika kusimamia uchunguzi wa ajali ya ndege na kuandika taarifa ya uchunguzi huo.

Hali hiyo isingejulikana kwa watu ila kutokana na vurugu iliyotokea katika kuitoa rasmi taarifa hiyo.Ulikuwa mkanganyiko wa karne, kwa wizara kutoa taarifa ya kina kama chapisho (inaitwa PDF kitaaluma, yaani chapisho lililofungwa jinsi lilivyo) likawekwa katika mtandao wa wizara.

Liliponukuliwa chapisho linasemaje ikawa kizaazaa, hasa kwa kumkana kweupe shujaa wa kuokolewa abiria wengi, hali inayoinyanyasa wizara ambayo ina jukumu la kusimamia uokoaji, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Kwa vile hata hivyo kulikuwa na jitihada za kuokoa watu ndani ya ndege baada ya kutua kwa dharura kwenye kina kifupi cha maji ya Ziwa Victoria kando ya uwanja wa ndege wa Bukoba, uwepo wa jitihada hiyo ukapewa kipaumbele, si ule wa nje.

Kutoa kipaumbele kwa uokoaji kutoka ndani ya ndege ni ishara kuwa mifumo ya uongozi wa safari za ndege na nini cha kufanya, inafanya kazi njema, ila shida ilikuwa ni vifaa kutokuwepo.

Kwa jambo hilo, kukatokea kiwango cha kushangaza cha usahaulifu unaokuwa kana donda ndugu, na taarifa rasmi ikajaa miito ya kuongeza 'uwekezaji' au kufanyika uwekezaji wa nguvu katika eneo hilo la usimamizi wa dharura na uokoaji.

Ulikuwa ni mtazamo wa kimfumo wenye nia ya kufumbia macho siyo uhaba ila kutokuwepo kimsingi miundombinu na mfumo wa uokoaji, licha ya uwepo wa vikosi na vyeo ambavyo huambatana na vifaa, utayari vitani.

Yako maeneo kadhaa ambayo taarifa ya awali ya wizara iliyataja ila hayakuwepo katika muhtasari wa waziri, katika mkutano na midia ulioanza kutayarishwa asubuhi, ukatarajiwa saa 10 jioni, halafu ukaanza takriban saa mbili usiku.

Jitihada yote hiyo ya kujipanga ilikuwa ni kielelezo cha kina cha uangalifu nini kizungumzwe, ambako kifasihi ni kuwa ilikuwa inatolewa siyo nguvu ya hoja ila hoja ya nguvu kuwa huu ndiyo ukweli, siyo kingine.

Kutumia muda mwingi kujipanga na kuhitaji kufuta maelezo ya awali ni jambo ambalo lisingesimama kama ni kesi mahakamani, au kuwa na shahidi anayejichanganya katika maelezo yake, haelezi anachokumbuka.

Ni tukio ambalo limetoa picha halisi ya ugumu ya 'kusukuma mbele gurudumu la maendeleo,' kwani kilichotokea kilidhihirisha kuwa idara za serikali kimsingi zinafanya kazi za kuingia na kutoka wakilipana mishahara, si kujiandaa kwa kutatua matatizo.

Ajali za ndege kimsingi ni nadra, hivyo kuna uwezekano wa kuacha kuchukua tahadhari zozote, siyo kwa vile hakuna bajeti ila fedha hiyo inaweza kutumiwa kwa njia yoyote nje ya vifaa, akiridhia mtendaji mwandamizi. Ikitokea wakaonekana hadharani eti hapakuwa na kikosi cha uokoaji katika kituo muhimu kama uwanja wa ndege, au utayari wa kikosi cha mamlaka nyingine yoyote, hawaelezi ilitokeaje upungufu mkubwa kiasi hicho kudhihirika na labda nani anawajibika. Wanashinikiza 'uwekezaji' zaidi, waongezewe pesa.

Hapo kuna suala la mbinu za uhasibu kwani kuchunguza ajali ni kama kufanya ukaguzi wa kilichotokea, yaani kilichoingia na kilichotoka utayari wa ndege kuruka na miundombinu ya inapotua, halafu udhaifu wa utendaji kazi iwe ni ndani ya ndege au eneo la kutua.

Katika ajali hiyo, uchunguzi mzima ni kama ulilenga jinsi ndege ilivyokuwa inatua halafu ikaishia katika maji, halafu nani aliokoa abiria.

Yako maeneo yalijitokeza kwa kusikiliza ilichosema serikali lakini vyombo vya habari havikujadili, kwani uokoaji ulibeba dhima.

Yako maelezo kuwa ndege hiyo tayari ilikuwa inatua, ikiwa imetanguliza vielelezo vyote vya utayari wa kufanya hivyo.

Ina maana kuwa hali ya uwanja, licha ya kuwa na mvua na mawingu, haikumzuia rubani kupata njia ya kutua, ila ilianza kutikisika kwa nguvu ikiwa tayari inakaribia kutua, ikakosa mwendo na kushuka pale ilipofikia, yaani kando ya uwanja na ndani ya maji.

Inawezekana sula hilo likaelezewa kwa kina katika ripoti ya uchunguzi ya watengenezaji wa ndege hiyo kutoka Ufaransa, kwani suala muhimu kwao ni ubora wa ndege na kama kulikuwa na hitilafu katika ndege, au hapana. Suala la kutingishika wakati inaanza kutua inaelekea litaonekana katika kisanduku cheusi 'black box,' au hata kwa wasafiri waliosimulia walichokiona kwani marubani wote wawili hawakuokolewa.

Hiyo pia ni aina ya ukaguzi, kuwa wafuatiliaji wa habari walielekeza nguvu kwa mkasa wa uokoaji na siyo katika ajali yenyewe, japo marubani walikufa, ila kisanduku kipo baadhi ya maswali yatajibiwa.

# HABARI PICHANI



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Estim wakirekebisha baadhi ya maeneo ya uzio wa barabara ya Morogoro, Mbezi Kwa Yusuph, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Taaluma Utafiti na Ushauri, Prof. Appolinary Kamuhabwa, akizungumza jijini Dar es Salaam juzi baada ya kumalizika mbio za Reunion Run kilometa 5, 10 lengo ni kukutana na kufahamiana kwa waliosoma chuo hicho na kutoa ujumbe kwa jamii kujitahidi kufanya mazoezi. Kulia ni Kaimu Mwenyekiti wa Chuo, Dk. Khadija Malima. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Kipande cha Kilomita tano cha Barabara ya Majita kutoka Kijiji cha Kusenyi hadi Kitongoji cha Kwikonero katika Kijiji cha Suguti, mkoani Mara, kikiwa kimewekwa lami. Ujenzi ulianza miaka mitatu iliyopita, lakini hadi sasa haujakamilika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CHEMSHABONGO NA -00 24 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
1. kasirika ghafla
8. mwanzo
9. ndugu mkubwa wa kiume
10.sehemu iliyotengenezwa rasmi watu kukaa na kuzungumza
11.pengine 12.ujiuji unaotoka kwenye volkano 13. rejea mahali
14.mwisho wa kitu 17.afya
19.shauku ya kufanya jambo
21.msafiri 22.chakula chenye umbo la nyuzi 25.Kazeh ya sasa
27.kambi 28. kipaumbele

Chini:
1. taarifa
2. zama 3.magonjwa 4. Uo 5. giza
6. fikiri jambo kwa makini
7. kuwa na hamu ya kupata kitu
14.mganga
15.yenye madoadoa mwili mzima
16.weka kitu ndani
18.upungufu wa kitu 20.kata
23.korongo la maji yatiririkayo wakati wote 24.badilisha kitu kwa fedha 26. labda




## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KIUA
TUNDA
TANGAZA
ADAA
DAIMA
IMARA
ADHABU
MARAIS
HIMAYA
MUNGU
ANASA
MAALUM
MAUTI
TAWI
UTALII
MBUYU
HAU
MADA
UDI
NINI
NANI
TUMA
AMAA
ONA
TOA
AGA
ZOA
UHAI
AWA




Majibu toleo lililopita





## Wananchi washauriwa kuzikatia bima mali zao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya CRDB imewashauri wananchi kuzikatia bima mali zao kwa lengo la kuepuka hasara zitokanazo na majanga kama vile ajali, ujambazi, mafuriko na moto.

Meneja wa CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jenipher Tondi, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki jijini hapo wakati wa hafla ya kuitambulisha huduma mpya ya bima iliyoanzishwa na benki hiyo 'Kuwa Shujaa, bima mchuma'.

Alisema huduma hiyo ni muhimu kwa mtu yeyote anayemiliki mali ikiwamo nyumba, magari na biashara kwa sababu ikitokea tatizo lolote wanafidiwa kwenye mali hizo.

Alisema bima inayotolewa na benki hiyo ni nzuri kutokana na kuwa na matawi na mawakala nchi nzima ambao wanahudumia mtu yeyote anayehitaji huduma hiyo.

"Benki yetu kwa sasa ina matawi 268 nchi nzima ambayo yote yanatoa huduma hii ya bima kwa hiyo nawashauri wananchi wakate bima kupitia kwetu, kwa mtu yeyote ambaye anamiliki mali bima ni muhimu," alisema Jenipher.

Meneja Uhusiano wa Kitengo cha Bima wa CRDB, Haji Mmbaga, alisema kutokana na maendeleo ya teknolojia mtu yeyote anayetaka kulipia bima anaweza kulipia eneo lolote alipo na sio lazima aende benki ama kwenye tawi la benki.

Alisema benki hiyo imejiwekea utaratibu ambao haumzuii mteja kupata huduma kwenye tawi lolote la benki hiyo na hivyo akawashauri wananchi hasa wafanyabiashara kuchangamkia.

"Unaweza ukawa umekata bima ya chombo chako kwenye tawi la Mwanjelwa hapa M Mbeya lakini ukapata majanga ukiwa Dodoma, hutalazimika kurudi na badala yake unaingia kwenye tawi lolote lililoko jirani na unapata huduma," alisema Mmbanga.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliipongeza benki hiyo kwa kubuni utaratibu huo akieleza kuwa kutokana na hali ilivyo sasa hivi kila mtu mwenye mali ni muhimu kukatia bima mali hiyo.

Aidha, aliwashauri watendaji wa benki hiyo kuongeza utoaji wa elimu ya bima kwa wananchi ili waichangamkie zaidi huduma hiyo kwa ajili ya ulinzi wa mali zao.

Homera alisema huduma ya bima inatakiwa iendelee kusisitizwa kwa wananchi ili waichangamkie na kuitumia kwa ajili ya ulinzi wa mali zao.

# Serikali yarejesha zaidi ya hekta 70,000 za Hifadhi ya Ruaha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imerejesha zaidi ya hekta 74,000 kutoka pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali na kuruhusu ardhi hiyo itumiwe na wananchi kwa shughuli nyingine za kiuchumi.

Uamuzi huo ulitolewa na timu ya mawaziri wanane wa kisekta wanaoshughulikia migogoro ya ardhi nchini, ambayo juzi ilitembelea wilayani Mbarali kwa lengo la kukagua uwekwaji wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Akiongoza timu hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Seleimani Jafo, alisema uamuzi wa kurejesha ardhi hiyo kwa wananchi unalenga kuwawezesha wananchi wa vijiji vilivyo pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kupata ardhi.

Alisema ardhi hiyo itatumiwa na wananchi wa vijiji hivyo kwa shughuli za kilimo na ufugaji ili kuepuka kuendelea kuwa na mwingiliano kati ya shughuli zao na shughuli za uhifadhi.

Alisema hekta hizo zilizorejeshwa kwa wananchi kati yake 37,400 zimeachwa ili zitumike kwa ajili ya ufugaji na nyingine 36,600 zimepangwa zitumike kwa shughuli za kilimo.

"Tumefanya hivyo kwa sababu ya kuweka mbele uzalendo kwa nchi yetu ambapo sasa kazi za kiuchumi zitafanyika, lakini uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla yatabaki kuwa salama," alisema Jafo.

Alisema uwekaji wa mpaka utakapokamilika, kila upande baina ya wananchi na Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA) kupitia Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, utatambua maeneo yake na hakutakuwapo na mwingiliano na kumaliza mgogoro wa muda mrefu baina ya hifadhi hiyo na wananchi wilayani Mbarali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kazi ya uwekwaji wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali inaendelea kwa kufuata maelekezo ya wataalamu na uamuzi wa serikali.

"Mpaka sasa tumeshaweka mpaka umbali wa zaidi ya kilometa 61 na kazi inaendelea, shughuli hii tunaifanya kwa kuzingatia maelekezo ya mawaziri wa kisekta ambao wamepewa jukumu na Rais la kuhakikisha mgogoro huu unakwisha," alisema Homera.

Wananchi wa Wilaya ya Mbarali wamekuwa na mgogoro wa ardhi dhidi ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, wakipinga mipaka iliyowekwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali namba 28 la mwaka 2008 (GN 28) wakidai kuwa umewekwa ndani ya ardhi yao.



Mrakibu wa Dawati la Jinsia Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Inspekta David Mtulo, jana alitoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa Sekondari ya Sinde. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Shirika lawajengea uwezo viongozi wa vijiji, kata

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Save the Children, linalofanya kazi wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe, limeanza kuwajengea uwezo viongozi wa vijiji na kata kwa kuwapatia mafunzo ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya watoto wenye umri chini ya miaka minane.

Mratibu wa Mradi wa Shirika la Save the Children Wilaya ya Mbozi, John Tobongo, alisema wakishirikiana na serikali wameamua kutoa mafunzo hayo kipindi hiki cha maandalizi ya bajeti ya mwaka 2023/2024 ili kujumuisha mambo yote muhimu yanayohusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kuanzia miaka 0 - minane.

Kipindi hicho ni muhimu kwa mtoto kwa sababu ubongo wa wake hukua kwa asilimia 90, wameona ni umuhimu kuanza na viongozi wa kata nane na vijiji ambao baada ya mafunzo hayo nao watayafikisha kwa wananchi kupitia mikutano yao ya hadhara.

Alizitaja kata nane zilizoanza kupatiwa mafunzo hayo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kuwa ni Ukwile, Ipunga, Isalalo na Nyimbili nyingine ni Nanyala, Itumpi, Shiwinga na Rwanda.

"Tumeanza kuwajengea uwezo viongozi mbalimbali wa vijiji na kata kwa lengo la kutusaidia katika vikao vyao vya bajeti kuiweka ajenda ya makuzi na malezi ya watoto na kupanga vipaumbele gani watakaviweka kwa ajili ya kuwasaidia watoto," alisema Tobongo.

Alisema tayari nchi imeandaa programu jumuishi ya makuzi, malezi na maendeleo ya awali ya mtoto ambayo ilizinduliwa mwaka 2021 na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Dk. Doroth Gwajima, inayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Songwe, Atusungukye Dzombe, alisema mpango huo utaanzia ngazi ya jamii wakiwamo, wazazi/walezi, viongozi kijiji, kata, wilaya na ngazi ya mkoa, taifa na wizara zote za kisekta matarajio ni kuona mtoto wa kitanzania anafikia katika utimilifu wa ukuaji wa hatua zote zinazohitajika.

"Tunategemea kuona mtoto kwenye eneo la lishe, afya, ujifunzaji wa awali, malezi yenye mwitikio chanya malezi ambayo hayana ukatili pamoja na suala la ulinzi na usalama wa mtoto unazingatiwa kwenye jamii, kila mtu ahakikishe suala la ulinzi na usalama wa mtoto katika hatua zake za ukuaji wa awali," alisema Atusungukye.

Aliitaka jamii kutoa ushirikiano ili mpango huo uweze kufanikiwa na kufikia malengo mahususi ambayo yatasaidia ukuaji wa mtoto.

Maria Makene, Ofisa Mtendaji kata ya Isalalo, alisema watoto wamekuwa wakisahaulika kuwekwa kwenye mipango ya vijiji, kata na halmashauri kupitia vikao vyao ameshauri kuweka ya masuala ya watoto.





# UVCCM yamchagua Mohamed Kawaida Mwenyekiti mpya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu wa 10 wa Uchaguzi wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), wamemchagua Mohamed Ally Mohamed (Kawaida) kuwa Mwenyekiti mpya wa umoja huo kwa kura 523 huku akiahidi kujenga umoja imara na kutoruhusu watu kuuyumbisha.

Kawaida ambaye alikuwa Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kusini Unguja, amechukua nafasi ya Kheri James, aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Juni 2021 na Rais Samia Suluhu Hassan.

Nafasi ya Mwenyekiti na Makamu wake zilikiwa wazi kwa zaidi ya mwaka mmoja na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Tabia Mwita Maulid, aliteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Uchaguzi huo uliofanyika juzi chini ya usimamizi wa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, huku nafasi ya Makamu Mwenyekiti, Rehema Omary, akiibuka mshindi kwa kupata kura 416.

Alisema Kawaida amekuwa Mwenyekiti wa umoja huo baada ya kuwashinda wagombea wenzie Farid Haji aliyepata kura 25, Massimu Kassu, aliyepata kura mbili na Abdallah Natepe, aliyeambulia kura moja.

Aidha, alisema kwa upande wa Sombi ameibuka mshindi kwa kuwashinda wagombea wenzake Khadija Ismail, aliyepata kura 41, Dorice Mgetta aliyepata kura 19 na Victoria Mwanziva, aliyepata kura 69.

Dk. Ackson alitaja nafasi nyingine kuwa ni wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), ambao ni Lulu Mwacha, Ramadhan Mlao na Mussa Mwakitinya kutoka Bara, Muhsin Hajji Ussi na Mwanaenzi Hassan Suluhu kutoka Zanzibar.

Nafasi tatu za Ujumbe wa Baraza Kuu la Jumuiya hiyo Taifa Tanzania Bara, zimechukuliwa na Shamira Mshangama aliyepata kura 358, Gloria Katalambula (232) na Jenipha Mamuhindo (139).

Akizungumza baada ya kushinda, Kawaida aliwaeleza vijana kuwa ni wakati wa kutambua vipaumbele vyao kama taifa ambavyo ni kuendeleza uhusiano bora wa kiuchumi nchi za jirani, utawala bora haki na usawa katika mambo mbalimbali.

"UVCCM unatakiwa kuwa mstari wa mbele kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kutimiza maono yao ya kuifanya Tanzania iwe moja ya nchi zinazoendelea kwa kasi."

"Niwaahidi UVCCM chini ya utawala wetu wa miaka mitano utakuwa wa kushirikiana, kushauriana na kusimamia vipaumbele vya nchi na utekelezaji wa Ilani ya CCM kuanzia ngazi ya shina."

"Ikumbukwe jumuiya ya umoja huu sio lele mama hivyo katika kipindi chetu tutahakikisha tunakuwa imara na jeuri kwa mtu yeyote atakayejaribu umoja wetu, Muungano wetu, mshikamano wetu, mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar uhuru wa Tanzania na watakaotaka kuhatarisha hali ya usalama wa taifa," alisema.

Makamu Mwenyekiti UVCCM, Rehema Sombi, alisema mchakato wa uchaguzi umeisha hivyo kazi iendelee na kama kuna sehemu walikwazana wasameheane ili kujenga jumuiya kwa maslahi mapana ya nchi.



Wanafunzi wahitimu wa elimu ya awali katika Shule ya Awali na Msingi St. Mary's wakitoa burudani ya ngoma kwenye mahafali ya darasa hilo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki hii jijini Dodoma. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wachimbaji wadogo waiomba serikali ruzuku ya zana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WACHIMBAJI wadogo wa madini nchini wameiomba serikali kuwapatia ruzuku na mitaji ya kununua zana za kuendeleza uchimbaji huo ili kujikwamua kiuchumi na kuchangia pato la taifa.

Walibainisha hayo mwishoni mwa wiki kwenye jukwaa la sekta ya uzinduaji lililoandaliwa na HakiRasilimali, wakati Taasisi ya kuendeleza uchimbaji mdogo nchini FADev ilipokuwa ikiongoza mjadala wa serikali kurasimisha sekta ya uchimbaji mdogo.

Walisema serikali inapaswa kuwashika mkono wachimbaji wadogo ili wainuke ikiwamo kuwapatia ruzuku na sio kuwasukumia kwenye taasisi za kifedha (benki) mahali ambapo hawawezi kukopesheka. "Serikali kupitia Wizara ya Madini tunaiomba itupatie ruzuku wachimbaji wadogo na sio kutusukumia kwenye benki ambazo haziwezi kutupatia mikopo," alisema Rachel Njau.

Aidha, mchimbaji Pili Husein kutoka Mererani, alitoa ushuhuda anavyonufaika na ruzuku ya serikali Sh. milioni 80 ambayo aliipata mwaka 2013.

Alisema ilimsaidia kumkuza katika sekta hiyo ya uchimbaji mdogo wa madini, huku akiiomba serikali kuendelea kutoa ruzuku hizo kwa wingi.

Naye Kamishna Msaidizi kitengo cha wachimbaji wadogo kutoka Wizara ya Madini, Francis Mihayo, alisema serikali iliweka utaratibu wa kuwapatia ruzuku wachimbaji wadogo, lakini baadhi yao walizitumia fedha hizo kinyume na matarajio na kulazimika wasitishe.

"Mwaka 2013 serikali iliweka utaratibu wa kuwasaidia wachimbaji wa wadogo baada ya kuitambua fursa ya madini pamoja na kuwapatia ruzuku, lakini unampatia mtu ruzuku akanunue lori la kubeba vifusi vya udongo wa madini ana kwenda kununua Kirikuu, mwingine badala ya kununua pampu ya kuvuta maji mgodini anunua pampu ya nyumbani," alisema Mihayo.

Katibu Mtendaji wa FADev, Mhandisi Theonestina Mwasha, alisema serikali pamoja na taasisi zisizo za kiserikali zinapaswa kuwashika mkono wachimbaji wadogo pamoja na kuwapatia elimu na kutambua uchimbaji ni kama biashara zingine na wana mchango mkubwa katika pato la taifa.

Alisema taasisi yao ya kuendeleza uchimbaji mdogo, wameshaunda vikundi 15 vya wachimbaji wadogo na kuwapatia ruzuku, pamoja na wengine kuwaunganisha kwenye taasisi za kifedha ili wapate kukopesheka, na kuwapatia pia elimu namna ya kuhifadhi taarifa zao za kibenki.

# Wazazi wakumbushwa ulazima wa kuandikisha watoto shule

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema ni lazima wazazi kuwaandikisha watoto wao kupata elimu ya awali ili kuwajengea mbinu sahihi zitakazowasaidia kujifunza kwa ufanisi mambo mbalimbali kabla ya kujiunga na darasa la kwanza.

Mratibu wa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto darasa la kwanza na la pili kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Hawa Selemani, alibainisha hayo juzi alipokuwa akitoa hotuba kwenye mahafali ya darasa la awali Shule ya Msingi St. Mary's Dodoma.

Alisema, elimu ya darasa la awali ni jambo la lazima kwa watoto kwa kuwa ndiyo sehemu za sahihi ya kuwajengea uwezo wa kujifunza mambo mbalimbali kabla ya kuanza darasa la kwanza.

Kutokana na hali hiyo alisema wazazi ni lazima kuwaandikisha watoto wao katika shule za awali ili kuwapatia mbinu sahihi za kujifunza kutoka kwa walimu wenye weledi.

"Wazazi msilazimishe watoto wenu kwenda kusoma tuisheni kwani wanajifunza mambo mengi na kwa ufanisi pale wanapotumia michezo, kuwapa mitihani au kuwafundisha mambo ya juu ya uwezo wao ni kuharibu ubongo wao.

"Msifikirie kuwa mtoto kupatiwa mitihani ya mamanba makubwa ndiyo njia sahihi ya kujifunza hapana hapo tunaharibu ubongo wa watoto wetu, mtoto anatakiwa kujifunza kwa vitu ambavyo ni vya 'level' yake hiyo mitihani siyo sasa wataikuta darasa la kwanza na la pili wakifika huko," alisema.

Aliwataka wazazi kutoa ushirikiano kwa walimu na kufuatilia maendeleo ya watoto wao wanapokuwa shule ili kubaini kero mbalimbali zinazowakabili kitaaluma.

"Walimu wanawahitaji ninyi wazazi katika kufuatilia maendeleo ya watoto kama mtaweka mikono yenu kwa watoto hawa ili wapate mbinu sahihi za kujifunza basi hakutakuwa na magonjwa wala wezi pia wapeni watoto wenu uhuru wa kuchagua kile wanachotaka na nyinyi muwape sapoti kwa kila wanacho kitaka," alisema. Aliwapongeza wazazi nchini kwa kubadili mtizamo na kuanza kutoa fursa sawa kwa watoto wote kwenda shule bila kujali jinsia zao.

"Zamani wazazi wengi walikuwa wanapendelea watoto wa kiume peke yao kuwapeleka shule, lakini hivi sasa mtizamo huo hasi umebadilika na kama ambavyo naona hapa wote wapo katika idadi inayolingana," alisema.

Mkurugenzi wa Shule ya St. Mary's Dodoma, Tibe Rwakatare, alisema wataendelea kuboresha miundombinu kwa ajili ya watoto kujifunzia hasa katika elimu ya awali ambayo ndiyo msingi wa mambo yote.

"Tunaendelea na ujenzi wa shule ya awali ambayo mwakani itawezesha watoto wa darasa la awali kuwa na eneo lao na kuondokana na hali hii ya kuchanganyika na wa shule ya msingi," alisema.

Rwakatare, alisema wanapanga kuwa na maktaba kubwa ya shule ambayo itawasaidia watoto kupata vitabu vingi kwa ajili ya kujisomea.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Benard Maalafu, alisema wataendelea kuimarisha usimamizi wa wanafunzi wanapokuwa ndani ya shule na nje ili kuhakikisha wanapata elimu bora.





## Jamii yaelezwa umuhimu kuwekeza kwenye afya

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Kinga na Elimu ya Afya, Dk. Salum Slim, ameitaka jamii kuwekeza zaidi katika afya ili kupata nguvu ya kufanya kazi za kiuchumi kwa manufaa yao na taifa kwa jumla.

Akizindua mradi wa kuboresha afya huko Nungwi Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja mwishoni mwa wiki, alisema kukiwa na wagonjwa wengi wasioweza kufanya kazi, taifa halitopata maendeleo.

Aliwataka wananchi kuzitumia vyema fursa za kuchunguza afya, zinazotolewa kupitia miradi na misaada mbalimbali ili kama wana matatizo ya kiafya wajue na kuanza tiba mapema.

Mradi huo wa kuimarisha afya ya moyo unatekelezwa kwa pamoja na taasisi ya 'HealthyHeartAfrica' ya Kenya na HIPZ Zanzibar chini ya ufadhili wa Taasisi ya Uingereza, AstraZeneca wakishirikiana na kitengo cha maradhi yasiyoambukiza Zanzibar (NCD).

Dk. Slim alisema uzinduzi wa mradi huo wa majaribio unalenga kuvifikia vijiji 15 vya Mkoa wa Kaskazini Unguja, ukianzia kijiji cha Nungwi, kabla kuendelea katika mikoa mingine ya Zanzibar.

"Afya bora ni jambo la msingi na kutibu maradhi yasiyoambukizi kuna gharama kubwa ambazo wananchi wengi hawazimudu kutokana na hali duni ya kipato," alisema.

Naye Meneja wa kitengo cha maradhi yasiyoambukiza Zanzibar, Subira Bakari, alisema asilimia 33 ya wananchi wa Zanzibar wanaugua shinikizo la damu, ingawa idadi hiyo ni ya wanaohudhuria kliniki na kutambua hali zao.

Alisema kwa kuwa serikali inatoa matibabu bure, inabeba mzigo mkubwa kutokana na wananchi wengi kupuuza umuhimu wa kinga, fedha na nguvu nyingi zinatumika kwenye kutibu.

Mkurugenzi wa mradi katika taasisi ya kuimarisha afya Zanzibar (HIPZ), Simon Kuhnert, alisema miongoni mwa malengo yao ni kuona wananchi wa Zanzibar wanaishi maisha bora mbali na maradhi yasiyoambukizi na mengine.

Naye Mkurugenzi wa huduma za afya endelevu kimataifa katika Taasisi ya Astra Zeneca nchini Uingereza, Dk. Allan Mackenzie, alisema shinikizo la damu ni ugonjwa unaoua watu wengi duniani, lakini kwa kutumia sayansi yanaweza kuzuilika iwapo kila mmoja atatimiza wajibu wake kuanzia kinga hadi matibabu.

# Uchumi wa buluu kuwezesha wanawake katika uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, amesema nia ya Serikali ya Zanzibar katika uchumi wa buluu, ni kuhakikisha nguvu zote zinawekezwa katika uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

Aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa kujadili rasimu ya mkakati wa mpango kazi wa kujumuisha masuala ya jinsia na wanawake katika uchumi wa buluu uliofanyika mjini hapo.

Alisema uwekezaji huo utajikita zaidi katika sekta ya uvuvi, ukulima wa mwani, usarifu wa dagaa, ufugaji wa matango bahari na kaa. Alisema katika kuleta maendeleo ya haraka ya jamii, serikali ipo mstari wa mbele kuhakikisha ushirikishwaji kwa ukamilifu wa kinamama, kwa kuwasaidia katika elimu, ubunifu, zana za kufanyia kazi, mitaji na masoko.

"Napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru waandaaji wa shughuli hii Shirika la Umoja wa Mataifa la UN Women, kwa mchango wenu mkubwa katika mwendelezo wa kuiunga mkono Tanzania, lakini katika kuisaidia na kuiimarisha ajenda yetu ya uchumi wa buluu hapa Zanzibar, hususan katika kupigania na kuhakikisha kuwa haki, pamoja na maslahi ya wanawake katika uchumi wa buluu, yanashirikishwa na kutekelezwa kwa ukamilifu," alisema.

Alisema mkakati huo ni muhimu kwa Zanzibar, katika kufanikisha mwendelezo wa juhudi za serikali za kuhakikisha haki na usawa wa wanawake na jamii kwa ujumla katika kufanikisha azma ya utekelezaji wa uchumi wa buluu, hasa katika sekta za uvuvi na mazao ya baharini.

Aidha, alisema wizara yake itahakikisha inaunga mkono katika utekelezaji wa programu zote za maendeleo ikiwamo utekelezaji wa mkakati huu unaolenga kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wote wananufaika na utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu.

Waziri huyo alisema serikali inaendelea kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), ikiwamo lengo nambari tano ambalo ni kuleta maendeleo, usawa na haki kwa jinsia zote ili kufikia malengo hayo.

Hata hivyo, alisema serikali imefurahishwa na mchakato wa mkakati huo na mapitio ya awali yametambua jitihada zinazofanywa kuhakikisha ushirikishwaji wa wanawake na kubainisha mikakati ya kuboresha hatua zinazotekelezwa na serikali na wadau hususani uwezeshaji wa mbinu bora za kilimo, uvuvi, mazao ya baharini, ujasiriamali na ubunifu.

Pia kuboresha katika biashara na masoko, kuongeza ubora wa huduma bidhaa pamoja na upatikanaji wa huduma za kifedha mambo yote yatachangia utekelezaji wa sera ya uchumi wa buluu.

Naye mshauri elekezi wa mkakati huo wa jinsia kutoka UN WOMEN, Shukuru Nyagawa, alisema wameangalia maeneo matano yanayohusiana na uchumi wa buluu ikiwamo uvuvi, kilimo, utalii, usafirishaji na utawala bora na kueleza changamoto mbalimbali wanawake wanazokutana nazo kwenye shughuli hizo.

Alisema ni kwasababu ya uelewa wao mdogo, ukosefu wa mitaji, nyenzo bora za ufanyaji kazi na ukosefu wa fursa za kushiriki na mkakati huo wa jinsia ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa nyenzo ya uchumi wa buluu.

Alisema mkakati huo umetoa mapendekezo mbalimbali ambayo yanahusika kuhakikisha bidhaa za wanawake katika uchumi wa buluu zinapewa soko na kufikiwa na mitaji.

"Wanawake ili waingie katika masoko lazima wawe na teknolojia za kuchakata bidhaa zao vizuri na zenye ubora ili kupata masoko ya ndani na nje na kunufaisha wananchi," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema uchumi wa buluu hauwezi kukua bila ya ushirikishwaji wa wanawake kupitia miradi ya kimaendeleo.




Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (kulia), akipokea cheti cha kupambana na vitendo vya udhalilishaji kutoka kwa Waziri wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Riziki Pembe, kwenye uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sheria kupambana vitendo vya udhalilishaji mbioni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUTOKANA na kuongezeka kwa kasi ya matukio ya udhalilishaji wa kijinsia, Serikali ya Zanzibar imesema ipo katika mchakato wa kutayarisha sheria ya kupambana na vitendo hivyo ambavyo vinaathiri jamii hasa ya wanawake na watoto.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mussa Kombo, katika mkutano wa maadhimisho ya siku 16 ya kupinga ukatili wa kijinsia ukiambatana na uwasilishwaji wa taarifa ya utafiti wa kuanzishwa kwa Sheria ya Kiislamu itakayokusanya sheria zingine muhimu uliwasilishwa mbele ya wadau na viongozi wa asasi za kiraia mjini hapa.

Kombo alisema miongoni mwa majukumu makubwa ya Tume ya Kurekebisha Sheria ni kuona wanazifanyia kazi pamoja na marekebisho ya sheria ambazo zinaonekana zimepitwa na wakati.

Alisema zipo sheria nzuri ikiwamo ya mtoto ambayo Serikali ya Zanzibar ilipata tuzo ya kimataifa, lakini kadri siku zinavyokwenda imebainika marekebisho makubwa yanahitajika.

"Ofisi ya Tume ya kurekebisha sheria tupo katika mchakato wa kuja na sheria ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia ambayo hiyo itahusisha moja kwa moja matukio yenye kudhoofisha maendeleo ya wanawake na watoto," alisema.

Alizitaja Sheria ya Mahakama ya Kadhi, Sheria ya Ofisi ya Wakfu na mali ya amana zinahitaji marekebisho makubwa katika kuwatumikia wananchi wake.

Alisema bado wanawake wanateseka hasa wanapopewa talaka na huenda kuanza maisha mapya huku wakiachiwa mzigo wa malezi ya watoto bila ya msaada wa baba wa watoto hao.

Alisema suala la matunzo kwa watoto ni moja ya changamoto kubwa wakati wanandoa wanapotengana na matokeo yake husababisha kuwapo kwa watoto wa mitaani wanaozurura ovyo kwa kukosa matunzo.


"Marekebisho ya sheria muhimu zinazowahusu watoto na wanawake zinahitajika kufanyika kwa sababu kasoro zake zimejitokeza na kusababisha usumbufu mkubwa kwa jamii yetu," alisema.

Katika mkutano huo uliwasilishwa utafiti uliotayarishwa na Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) ambao umeelezea umuhimu wa kuwapo kwa sheria moja ya Kiislamu ambayo itashughulikia moja kwa moja taasisi muhimu zinazosimamia mwenendo wa jamii hiyo.

Mhadhiri mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Dk. Sikujua Hamdani Omar, alisema Sheria za Mahakama ya Kadhi, Ofisi ya Wakfu na mali ya amana pamoja na Sheria ya Mtoto kunahitajika sheria moja ambayo itashughulikia moja kwa moja na kutoa huduma kwa jamii hiyo.

Alisema Sheria ya Mahakama ya Kadhi imebeba mambo mengi kwa wakati mmoja ikiwamo masuala ya ndoa, talaka matunzo ya watoto na ndio maana yanafanyika marekebisho yake mara kwa mara bila ya kukidhi mahitaji yake kwa walengwa.

Aidha, alisema suala la mirathi limekuwa na changamoto kubwa kwa watu kukwepa Taasisi ya Wakfu na mali ya amana na kurithishana kienyeji zaidi na hapo ndipo panapoibuka migogoro na wahusika wengine kukoseshwa haki zao.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Askari polisi waonywa kujihusisha rushwa matukio ukatili kijinsia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limewaonya askari wanaosimamia dawati la jinsia na watoto mkoani humo, kutojihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa kushughulikia kesi za matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Kauli hiyo ilitolewa jana mkoani hapo na Kamanda wa Polisi mkoani humo, Janety Magomi, katika mafunzo ya maofisa wa jeshi hilo pamoja na askari wa dawati la jinsia.

Alisema kuna baadhi ya askari si waadilifu wanajihusisha na vitendo vya rushwa kwenye kesi za matukio ya ukatili wa kijinsia.

Kamanda Magomi alisema, vitendo hivyo vinakwamisha utekelezaji wa sheria na kusababisha waathirika wa matukio hayo kukosa haki.

Askari hao walipatiwa mafunzo hayo ikiwa ni sehemu ya kwenda kutekeleza mradi wa kupinga ukatili wa wanawake na watoto wilayani Shinyanga, kwa ufadhili wa Shirika la Women Fund Tanzania (WFT-Trust).

Alisema vitendo vya rushwa ni tatizo katika usimamizi wa haki na kuwataka askari wa dawati la jinsia, katika utekelezaji wa mradi huo wawe mfano wa kuigwa.

Magomi alisema askari wakijiepusha na rushwa watasaidia kupunguza matukio hayo.

"Tunapopata kesi za ukatili wa kijinsia sisi askari polisi, tunapaswa kusimamia haki kama kiapo cha kazi yetu kinavyotutaka na sio kujihusisha na vitendo vya rushwa," alisema Magomi.

Katika hatua nyingine, aliwataka askari hao wanapokuwa wakisikiliza kesi za ukatili watumie lugha nzuri ili kutowaogopesha waliofanyiwa vitendo hivyo na kupata taarifa kamili, huku akiwasisitiza kuendelea kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wananchi na madhara yake.

Kwa upande wake, Mratibu wa dawati la jinsia mkoani Shinyanga, Monica Sehere, alisema katika mradi huo wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia wilayani Shinyanga watazifikia kata 14, huku wakiwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za ukatili pamoja na kutowaficha wahalifu.




Mkurugenzi wa Mambo ya Ndani wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ndositwe Haonga (katikati), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa mkuu wa kituo cha kulelea watoto yatima, Halima Ngoja (aliyevaa shungi), ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Shukrani kwa Mlipakodi wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TRA yawakumbuka wafungwa wanawake taulo za kike

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato Nchini (TRA), mkoa maalumu wa kikodi Kahama, imetoa msaada wa taulo za kike kwa ajili ya wafungwa wanawake katika gereza la wilayani ya Kahama mkoani Shinyanga.

Hatua hiyo itawasaidia wafungwa wa kike kujikinga na magonjwa wanapotumia vitambaa ambavyo sio safi na salama.

Aidha, vitu vingine vilivyotolewa ni pamoja na sabuni, kandambili, miswaki na dawa ya meno lengo likiwa ni kuunga juhudi za serikali kuwahudumia wafungwa hususani wanawake.

Akikabidhi msaada huo jana wilayani Kahama na mwakilishi wa Kamishna Mkuu wa TRA, ambaye ni Mkurugenzi wa Mambo ya Ndani, Ndositwe Haonga, wakati wa maadhimisho ya siku ya shukrani kwa mlipa kodi, alisema wafungwa wana mahitaji kama walivyo raia wengine katika jamii, wanahitaji misaada ili kukidhi haja zao.

Alisema taulo hizo zitapunguza mahitaji ya wafungwa wanawake wakati wa kujisitiri ndani ya mizunguko yao ya kila mwezi na kuondokana kutumia vitu sio salama kiafya.

Aliwaomba wadau wengine kujitokeza na kulisaidia kundi hilo kwa kuwa lina mahitaji sawa kama wanawake wengine ndani ya jamii.

Akipokea msaada huo, Mkaguzi Msaidizi wa Magereza, Anastazia Mwamlima alisema, wafungwa wanawake wana mahitaji mengi kwa taulo hizo zitasaidia kupunguza mahitaji yao.

Alisema wamekuwa wakiwahudumia kulingana na bajeti wanazozipata na wanapoingia katika mizunguko yao hutoa taarifa kwa uongozi na kuwapatia taulo safi ambazo zinawakinga na maradhi ikiwamo fangasi.

Katika hatua nyingine, TRA imetoa msaada wa vitu mbalimbali katika kituo cha kulelea watoto yatima kilichoko Kata ya Zongomela, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kama sehemu ya kupambana na ukatili wa kijinsia.

Vitu hivyo ni mchele, sukari, mafuta ya kula, madaftari, kalamu, sabuni, juisi, maji, biskuti, maharage na mafuta ya kupata.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Halima Ngoja, aliushukuru uongozi na wafanyakazi wa TRA kwa msaada huo na kuahidi kila mtoto kunufaika na msaada huo.

Alisema uendeshaji wa kituo hicho unategemea wadau pekee na msaada huo ni muhimu kwao.

Alisema kituo kina jumla ya watoto 49 kati yao 21 wapo shuleni na 28 bado wadogo na wanawapata kupitia ofisi ya ustawi wa jamii ya Manispaa ya Kahama.

# Mjumbe CCM aahidi kukisimamia chama kiuchumi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa Mkoa wa Tabora, Mohamed Hamdan, ameahidi kusimamia chama chake ili kiendelee kuwa imara kiuchumi na kisiasa.

Alisema kwamba pamoja na kukisimamia chama hicho ameahidi kuimarisha uhai wa chama na kuwezesha jumuiya zake kuwa na uchumi imara ili ziweze kujitegemea katika shughuli mbalimbali mkoani Tabora.

Akizungumza na Nipashe, ofisini kwake jana, alisema CCM ni chama kikubwa kilichobeba matumaini ya Watanzania na katika kipindi cha miaka mitano atahakikisha kinakuwa imara kwa kufufua miradi ya kiuchumi ya jumuiya zote.

Alibainisha kuwa hana shaka na chama chake katika nyanja za kisiasa kwa kuwa kina wanasiasa waliobobea, lakini kinahitaji kusimamiwa vizuri ili kiweze kuwa imara zaidi mkoani humo.

Alisisitiza kuwa atahakikisha jumuiya zote za chama hicho UVCCM, UWT na Wazazi zinakuwa na miradi ya uhakika itakayowaingizia kipato ili kufanikisha utekelezaji majukumu yao ya kila siku ikiwamo kuunganisha wanachama wao.

Aliongeza kuwa atatembelea wilaya zote saba za mkoa huo na kukutana na viongozi wa chama na jumuiya zake ili kuwahamasisha kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi zilizoko katika maeneo yao ikiwamo kuendeleza miradi iliyoko.

Alifafanua kuwa wana CCM wote wanapaswa kuwa kitu kimoja ili kuwa na chama imara huku akiwataka kuweka makundi yao ya uchaguzi pembeni ili kudumisha umoja na mshikamano utakaofanya chama kiendelee kuaminiwa zaidi.

"Uchaguzi umeisha, naomba wana CCM wote turudi kujenga chama chetu, umoja na mshikamano wetu ndio silaha ya ushindi katika chaguzi zijazo ule wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025," alisema.

Alisema makundi kwa sasa yanatakiwa kuvunjwa ili kukijenga chama kwa kuwa kinatakiwa kisimamiwe na kuwa imara kwa sababu kina wanachama wazuri waliobobea kisiasa.

Alisisitiza kuwa mafanikio ambayo chama kimepata tangu kuanzishwa Februari 5, 1977 yametokana na umoja na mshikamano wa viongozi na wanachama na wanatakiwa kuyadumisha.

Alisema atahakikisha chama na jumuiya zake zinakuwa na uchumi imara ili kufanikisha utekelezaji majukumu yao ikiwamo kutembelea wanachama wake na wananchi kwa ujumla ili kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Alimpongeza Mwenyekiti wa CCM Taifa, Samia Suluhu Hassan kwa kufanyakazi na kusimamia Ilani.

# Waasi 40 wa Burundi wauawa DRC

**KINSHASA,** DRC

MSEMAJI wa Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Luteni Marc Kyondwa, amesema waasi 40 wa Burundi wameuawa katika mashambulizi ya pamoja ya wanajeshi wa nchi hizo yaliyofanyika mwishoni mwa juma lililopita.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Luteni Kyondwa, majeshi hayo mawili yaliendesha mashambulizi makali dhidi ya waasi wa Burundi wa Kikosi cha Ukombozi wa Kitaifa (FNL).

Alisema majeshi hayo mawili yaliiondoa FNL kutoka kwenye vilima vyote vinne vinavyoelekea mji wa Nabombi na kwamba ilizingatiwa kama wadhifa wa amri ya jenerali wa FNL aliyejitangaza Aloys Nzabampema.

"Jeshi la DRC lilitoa wito kwa wakazi wa eneo hilo kushirikiana na vikosi vya kawaida na vijana kujitenga na makundi yenye silaha," alisema.

Taarifa hiyo pia ilimnukuu Jenerali wa DRC Meja Ramazani Fundi, ambaye ni kamanda wa operesheni katika eneo la kusini mwa jimbo hilo akisema, "FNL ni tawi la kundi la zamani la waasi la Agathon Rwasa, ambalo sasa ni upinzani mkuu wa kisiasa nchini Burundi".

Alisema tangu mwezi Agosti, wanajeshi wa Burundi wanaohusika na mapigano na makundi yenye silaha wamekuwapo katika eneo la Kivu Kusini nchini DRC, kama sehemu ya kikosi cha Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki (EAC).

Kinshasa, ambayo inaishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono kikamilifu waasi wa M23 huko Kivu Kaskazini, imekataa kuruhusu Kigali kushiriki katika kikosi hicho.

Kwa takriban miaka 30, mashariki mwa DRC imekuwa ikikumbwa na makundi yenye silaha ya waasi. **BBC**



Hoteli iliyoshambuliwa na al-Shabaab mwezi Agosti mwaka huu.

# Wanne wauawa shambulizi la Al-Shabaab Somalia

**MOGADISHU,** SOMALIA

WATU wanne wameuawa baada ya kundi la kigaidi la Al-Shabaab nchini Somalia kushambulia hoteli moja karibu na makazi ya rais katika mji mkuu wa Mogadishu.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, uvamizi dhidi ya hoteli hiyo ya Villa Rose ulianza Novemba 27, ambapo washambuliaji wa kundi hilo lenye mafungamano na mtandao wa kigaidi wa al-Qaida, walitumia bunduki na mabomu kuingia ndani.

Ofisa mmoja wa polisi aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba baadhi ya maofisa wa serikali walilazimika kukimbia kwa kutumia madirisha ya hoteli hiyo.

Mkaazi mmoja, Ismail Haji, anayeishi karibu na hoteli hiyo aliiambia Reuters kwamba kufikia asubuhi ya jana, ikiwa ni zaidi ya saa 12 tangu uvamizi kuanza, bado kulikuwa na milio mikubwa ya silaha ndani ya hoteli na kwamba bado walikuwa wanaendelea kusalia majumbani mwao tangu mzingiro wa vyombo vya usalama uanze usiku wa jana.

Ofisa mmoja ambaye hakutaka kutajwa jina, alisema vikosi maalum vya usalama, vifahamikavyo kama Gaashaan na Haramcad, vilichukuwa uratibu wa operesheni hiyo, kwa mujibu wa ofisa mmoja wa polisi aliyepo kwenye eneo la tukio.

"Wapiganaji walioanzisha mashambulizi bado wanapambana ndani ya hoteli dhidi ya vikosi vya Haramcad na Gaashaan na maofisa wa usalama wanajaribu kuwaokoa watu waliokwama ndani ya hoteli," alisema.

Ofisa mmoja wa usalama wa taifa, Mohamed Dahir, aliiambia AFP kwamba washambuliaji wamejificha kwenye chumba kimoja cha hoteli hiyo huku wakiwa wamezungukwa na vikosi vya serikali.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, miongoni mwa waliojeruhiwa walikuwa maofisa wa serikali na kwamba karibuni watafanikiwa kuidhibiti hali.

**BUNGE LASITISHA VIKAO**

Bunge la Somalia lilisema kuwa lilipaswa kusitisha vikao vya mabaraza yake yote mawili kutokana na mashambulizi hayo.

Kupitia taarifa iliyotumwa kwenye ukurasa rasmi wa Facebook wa bunge hilo, wajumbe wote wa mabaraza hayo ya bunge waliarifiwa kuahirishwa kwa mkutano uliokuwa umepangwa kufanyika jana.

Pia ilibainishwa kuwa kundi la Al-Shabaab, ambalo linataka kuiangusha serikali na kuanzisha utawala unaofuata tafsiri ya siasa kali ya Sheria za Kiislamu, limekuwa likifanya mashambulizi ya mara kwa mara mjini Mogadishu na kwengineko nchini Somalia.

Aidha, ilielezwa kuwa Oktoba 29 mwaka huu, magari mawili yaliyojaa mabomu yalilipuka mjini Mogadishu yakifuatiwa na milio ya risasi, ambapo watu 121 waliuawa na 333 kujeruhiwa, mashambulizi yanayotajwa kuwa mabaya kuwahi kufanyika kwenye taifa hilo.

Rais Hassan Sheikh Mohamud, aliyechaguliwa mwaka huu, ameanzisha operesheni kali ya kijeshi dhidi ya kundi hilo.

**DW**

## Wanajeshi Urusi watarajiwa kuondoka Zaporizhzhia

**KYIV,** UKRAINE

MKUU wa shirika la nyuklia nchini Ukraine Petro Kotin, amesema kuna ishara kwamba wanajeshi wa Urusi wanajitayarisha kuondoka kutoka kiwanda cha nyuklia cha Zaporizhzhia ambacho wamekuwa wakishikilia tangu mwezi Machi baada ya kuvamia nchini hiyo.

Pia inaelezwa kwamba endapo hilo litatokea, itakuwa mabadiliko makubwa katika vita vya Ukraine katika sehemu za kusini mashariki mwa eneo la Zaporizhzhia ambapo wanajeshi hao hawajabadilisha sehemu wanazoshikilia kwa muda wa miezi kadhaa.

Makombora ya kila mara karibu na kiwanda hicho cha nyuklia, yalisababisha kuwapo wasiwasi mkubwa kuhusu uwezekano wa janga kubwa la nyuklia endapo kiwanda kingeharibiwa.

Urusi na Ukraine wamekuwa wakishutumiana kwa miezi kadhaa kwa kurusha makombora karibu na kiwanda cha Zaporizhiizhia, ambacho kwa sasa hakizalishi nishati.

Aidha, wanajeshi wa Ukraine wamefanikiwa kudhibiti mji wa Kherson mwezi huu, pamoja na sehemu kubwa ya ukingo wa kulia wa Dnipro, mashariki mwa Zaporizhzhia. **VOA**

## Marufuku kutoka nje yawekwa Uganda kuikabili ebola

**KAMPALA,** UGANDA

KIONGOZI wa Uganda, Rais Yoweri Museveni, ametoa amri ya watu kutotoka nje katika wilaya mbili ambazo mlipuko wa virusi vya ebola ulianzia kwa muda wa siku 21, akisema serikali inafanikiwa kudhibiti maambukizi ya ebola nchini humo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, amri hiyo itatekelezwa hadi Desemba 17, mwaka huu, huku ikielezwa kuwa awali kulikuwa na amri kama hiyo ya siku 21 kuanzia Oktoba 15, na ilimalizika Novemba tano mwaka huu.

Museveni alisema hatua hiyo imechukuliwa ili kuhakikisha kwamba mafanikio ambayo yamepatikana kufikia sasa katika kukabiliana na mlipuko wa ebola, yanaendelea na kuhakikisha hakuna kabisa maambukizi ya virusi hivyo nchini humo katika muda wa siku chache zijazo.

Serikali ilisema kwamba hakuna maambukizi mapya yaliyoripotiwa katika wilaya hizo mbili, na kwamba watu 55 wametajwa kufariki na wengine 141 wakithibitishwa kuambukizwa ebola nchini Uganda, tangu Septemba 20 mlipuko uliporipotiwa.

Hata hivyo ilielezwa kuwa hakuna chanjo dhidi ya virusi vya ebola aina ya Sudan vinavyoripotiwa Uganda.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 350 LA 2018**
**SAMWELI AMANI MAKUNDI.....MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JANETH GERVAS MGONELA......MDAIWA/WADAIWA**
**WITO/KUITWA SHAURINI**
**JANETH GERVAS MGONELA - POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SAMWEL AMANI MAKUNDI** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 07/12/2022 saa 4:00 asubuhi mbele ya Mh. SILAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

**Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 Mwezi wa 11, 2022.**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FAB CARS LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **BMW** yenye usajili namba **MC 568 AKK,** CHASSIS NAMBA: **WB1041341YZD26413** na ENGINE NAMBA: **05006164.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **DAR/KIJ/RB/454773/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BIGABIGA EMILIAS MPUTI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S0153-0010** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SONGEA BOYS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIF: **DAR/KIG/RB/459106/2022**

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1072 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**ATHANAS HAKILIMINGI MSUNGU**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**ANGELINA PESAMBILI MUNYI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**All persons** claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **15th day of 12, 2022**.

Dated at DAR ES SALAAM this 18 day of 11 2022.

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA VYETI



**MARTIN HEMED KISUTE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0329/0084** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAKUMIRA SECONDARY** SCHOOL mwaka 2001 na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P 1189/0096** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BIAFRA SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka 2002. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/460503/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......84/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: AMINA RAMADHAN SABU WA MJI MPYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA RICHARD BENARD MICHAEL**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 29 Mwezi 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 11 mwaka 2022**

**HAKIMU MFAWIDHI**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SILVERLANDS TANZANIA LTD.** Tunatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya ... yenye namba za usajili **MC 513 ABC** Yenye chases namba **KE6250F000132** Injini namba **167FMMKBF00132** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi

Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/429064/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI (RESULT SLIP)



**BENJAMIN MANASE LINGULA,** Anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP ya KIDATO CHA SITA Yenye Index No S0334/0798** iliyotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Mwenge Secondary School Mwaka **2022.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. **TAARIFA YA POLISI: DSM/PHQ/RB/421807/2022**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SONGWE**
**ILIYOPO MBOZI**
**SHAURI NO.32/2022**
**JAHA OMARY KALINGA::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**ANDREW EDSON MWILWA:::::::::::MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**
**KWA : ANDREW EDSON MWILWA**

Fahamu kwamba JAHA OMARY KALINGA amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 01/12/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwakuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Songwe.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza la siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria .Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Mnadani Vwawa.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 17/11/2022.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**17/11/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 2302/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BURUHANI RWEGAHURILA RUBAGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**1. DAVID BURUHANI RUBAGA**
**2. ISAAC BURUHANI RUBAGA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi wa 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 28 Mwezi wa 11 Mwaka 2022.

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO;49/2022**
**KAIS JAMES MWAMBONA..............MDAI**
**DHIDI YA**
**BOSTA SHORA.......................MDAIWA**
**ISAKWISA KAYUNI[Msimamizi wa mirathi ya marehemu JACKSON MATAI KAYUNI............MDAIWA**

**YAH; KUITWA SHAURINI**
**KWA; ISAKWISA KAYUNI,**
Fahamu kwamba KAIS JAMES MWAMBONA amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.Shauri limepangwa kutajwa tarehe 06/12/2022 saa 2;30 asubuhi mbele ya MH. T. Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu taerehe ya wito huu.Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe22/11/2022.

**T. Munzerere**
**MWENYEKITI**
**22/11/2022**
.............................................

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## BURUDANI



# MAMA AMBARIKI ZUCHU KUWA MKE WA DIAMOND

KHADIJA Khopa ambaye ni mama wa msanii Zuhura Othman Soud 'Zuchu', amesema haoni ajabu kwa mwanawe kuitwa mke na msanii ambaye ni bosi wake, Naseeb Abdul 'Diamond' kwa kuwa huenda msanii huyo anaiona kesho yake na binti yake.

Hayo yamekuja siku kadhaa baada ya msanii Diamond kuweka wazi kile kinachoaminiwa kuwa ni uhusiano wake na Zuchu na kumwita mke, huku pia mama mzazi wa Diamond akimwita mkwe wakati akimtakia tamasha jema Zuchu nchini Marekani.

"Sioni shida mama Diamond kumwita Zuchu mkwe kwa sababu ana mtoto wa kiume, pia sishangai Diamond kumwita Zuchu mkewe inawezekana anaiona kesho yake njema na binti yangu," amesema Khadija.

Akizungumzia kuhusu suala la posa, iwapo familia ya Diamond imekwishatoa kwa ajili ya binti yake, mama huyo alisema suala hilo bado halijafanyika ila wakati ukifika kila kitu kitakuwa wazi.

Amefafanua kuwa binti yake huitwa mkwe kila upande na wala hajui atakayemuoa kwa kuwa amekuwa 'mkwe wa taifa' kutokana na yeye kuwa maarufu pia ni mtoto wa kike.

# NDEGE YA DIAMOND TAYARI




CHAWA wa WCB, Baba Levo, ameeleza kuwa, suala la ndege mpya aliyonunua Diamond kutua nchini ni la muda tu.

Baba Levo ametoa kauli hiyo juzi baada ya kuulizwa na waandishi wa habari kuhusu baadhi ya madai kuwa, Diamond hajanunua ndege hiyo.

"Ndege si kama Bajaj unaagiza leo na kuja leo. Ndege tumeshalipia, itakuja. Kuna mambo mengi ya kukamilisha hadi ndege itue ikiwamo taratibu za kiserikali," alisema Baba Levo.

Mapema mwaka huu, meneja wa Diamond, Salam alisema wameamua kununua ndege hiyo kutokana na kupoteza gharama nyingi kwenye kusafiri nchi mbalimbali kwa kulipia tiketi za ndege hivyo bora wanunue ndege yao ambayo pia watakuwa wanaikodisha.

# MOBETO:
## NAMPENDA JORDAN



HAMISA Mobeto amekiri kwamba amekufa na kuoza juu ya muigizaji wa Marekani, Michael B Jordan.

Kwenye akaunti yake ya TikTok, mama huyo wa watoto wawili ameposti video ya mkusanyiko wa picha kadhaa za Jordan na kumtambulisha kama mwanaume ambaye angetaka kuolewa naye.

"Ona mwanaume ninayetaka kuolewa naye..." Ameandika Hamisa chini ya video hiyo iliyoanza na picha yake.

Michael B Jordan ni muigizaji wa Marekani na ni mkurugenzi na mtayarishaji wa filamu.

Anajulikana kwa uhusika wake katika filamu maarufu kama The Wire (2002) Fruitvale Station (2013), Creed (2015) na Black Panther (2018, 2022).

Mwaka 2020, Jordan alitajwa kuwa mmoja wa watu 100 wenye ushawishi mkubwa zaidi ulimwenguni na Jarida la Time na pia kama mwanaume mzuri zaidi aliye hai.

Muigizaji huyo alijitosa kwenye mahusiano ya kimapenzi na mwanamitindo wa Marekani, Lori Harvey mnamo Novemba 2020.

Juni, 2022 ilitangazwa kuwa wawili hao walikuwa wametengana.

# MWAMBUSI ATAKA STRAIKA WAWILI USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI ikishuka dimbani leo kuikaribisha Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya, benchi la ufundi la Klabu ya Ihefu FC, limesema linatarajia kuongeza wachezaji wawili kwenye usajili wa dirisha dogo kwa lengo la kuiongezea nguvu timu hiyo.

Ihefu imeuanza msimu vibaya, kwani katika mechi 13 ilizocheza hadi sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, imeshinda mbili, sare mbili na kupoteza tisa, hivyo kuvuna alama nane tu zinazoifanya kuburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo inayojumuisha timu 16.

**Na leo itakuwa na kiba rua kingine kigumu ny umbani itakapowa karibisha mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo, Yanga, katika mechi nyingine ya ligi hiyo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Juma Mwambusi, alisema anahitaji idadi hiyo ya wachezaji ili kuiongezea nguvu safu yake ya ushambuliaji na ambayo imeonekana kuwa na mapungufu msimu huu.

"Safu ya umaliziaji ina mapungufu, mara nyingi washambuliaji wangu wanapata mipira [sehemu sahihi] lakini wanashindwa kufunga, hivyo inanipasa nifanye usajili mzuri," alisema Mwambusi.


Kocha huyo alisema washambuliaji wake wamekuwa hawatulii kwenye lango lao jambo lililowasababishia kupoteza michezo yao iliyopita.

"Michezo yetu iliyopita hatujafanya vizuri kutokana na upungufu huo, japo timu inajitahidi kucheza ikiwa uwanjani lakini umaliziaji ndio tatizo.

Kuhusu mechi dhidi ya Yanga, Mwambusi alisema wamejipanga vizuri kukutana na timu yake hiyo ya zamani licha ya kuwakosa nyota wake wanne ambao ni majeruhi.

Alisema anahitaji kupata matokeo mazuri kuliko wapinzani wao kwani wapo kwenye nafasi ambayo si nzuri.

BOOMPLAY...



Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli (wa pili kushoto), akichangia mjadala wa kupunguza pengo lililoko kwa wasanii wa muziki wa Kiafrika katika kuzifikia nyanja za kimataifa kupitia Kongamano la Muziki Barani Afrika (ACCES), lililofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa juma. Wengine ni Mkuu wa Lebo na Uchapishaji, Universal Music Africa (Ivory Coast), Pit Baccardi (kushoto), Meneja wasanii na uhusiano wa The Orchard, Beth Achitsan (wa pili kulia) na Meneja wa Kanda Afrika kwa Ditto Music, Wendy Verwey Bekker. **MPIGAPICHA WETU**

# *Kallaghe arejea kuongoza riadha*

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HATIMAYE uchaguzi mdogo wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), umefanyika Ukumbi wa African Dreams jijini Dodoma jana na kushuhudiwa William Kallaghe akiibuka mshindi katika nafasi ya makamu wa rais.

Uchaguzi huo mdogo, umefanyika baada ya waliokuwa wakishikilia nafasi za makamu wa rais na Mjumbe Kanda ya Pwani, kujiuzulu kutokana na sababu mbalimbali.

Katika uchaguzi huo, ambao ilibidi ufanyike mara mbili, baada ya awamu ya kwanza wagombea wa nafasi ya makamu wa rais kufungana kwa kura, jumla ya wagombea watatu walikuwa wakichuana, ambao ni William Kallaghe, Shabani Hiki na Kanali Mstaafu Juma Ikangaa.

Akitangaza matokeo hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Wakili Msomi Benjamin Kalume, alimtaja Kallaghe kupata kura tisa sawa na Kanali Ikangaa huku Hiki akiambulia sita tu.

Kutokana na matokeo hayo ilibidi wawili hao kupambanishwa upya katika uchaguzi wa duru ya pili na Kallaghe kuibuka kidedea kwa kuzoa kura 15 dhidi ya tisa za Kanali Ikangaa, hivyo sasa ataliongoza shirikisho hilo chini ya rais Silas Isangi.

Kabla ya kurejea juzi, Kallaghe aliondolewa mwaka jana na Shirikisho la Riadha baada ya kukiuka taratibu za katiba kwa kufanya mambo kinyume, hivyo mkutano mkuu uliokuwa chini ya Anthony Mtaka uliwaondoa kwenye uongozi.

Kwa upande wa nafasi ya Mjumbe wa Kanda ya Pwani, mgombea pekee Felix Chunga, alipata kura 21 za ndiyo huku tatu zikimkataa.

Jumla ya wapigakura 24 kati ya 26 walipiga kura katika uchaguzi huo na hakuna kura iliyoharibika.

Baada ya kutangazwa washindi, Msajili wa Vyama na Klabu za Michezo, Riziki Majala, alimpa fursa Wakili Simon kuwaapisha washindi na shirikisho hilo likaendelea na mkutano wake wa kawaida.

## Sarakasi yazindua CHASAMATA

**Na Sabato Kasika**

WACHEZAJI wa mchezo wa sarakasi nchini wamezindua chama chao kiitwacho Chama cha Sarakasi Tanzania (CHASAMATA), ambacho kitakuwa na jukumu la kuwaunganisha wachezaji wa fani hiyo.

Uzinduzi wa chama hicho, ulifanyika jijini Dar es Salaam juzi, na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa burudani, huku ukinogeshwa na vikundi vya sarakasi na vya ngoma za asili.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Sanaa za Maonyesho, Betty Kazimbaya, alisema wanaunga mkono na kuwapa nafasi vijana kwa kuwa ndio wakati wao wa kutekeleza majukumu yao.

Alifafanua kuwa, kwa sasa sanaa ni kazi kama zilivyo kazi nyingine na ni ajira, huku akiwapongeza wachezaji sarakasi kwa kuanzisha chama chama, ambacho alisema kinaweza kuwaunganisha.

Mwenyekiti wa CHASAMATA, Selemani Pembe, alisema awali chama hicho kilikuwa ni cha Mkoa wa Dar es Salaam tu, na kwamba sasa kimepanuka na kuwa cha nchi nzima.

## Sanaa ya uchoraji yapigiwa debe

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imeendelea kuhamasisha sanaa ya uchoraji kwa Watanzania kupitia bia yake ya Guinness, kwa kufanya shindano la uchoraji lililofanyika katika ukumbi wa Fuego Lounge.

Shindano hilo lililoitwa "Guinness Brews and Brushes" lilifanyika jana jijini Dar es Salaam na lilikuwa na lengo la kuwaleta kwa pamoja, watumiaji wa bidhaa za SBL, wachoraji na wadau mbalimbali wa sanaa.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa SBL, Rispa Hatibu, alisema sanaa ya uchoraji imekuwa ikipanuka nchini na kuvutia watu wengi hasa watalii na kuifanya Tanzania kuwa moja ya kituo cha sanaa ya uchoraji barani Afrika.

"Tumeamua kuwapa watu nafasi ya kuonyesha vipaji vyao na kuwafanya waweze kung'ara kwa vile bia ya Guinness ina kauli mbiu yake inayowasihi watu kung'aa, hivyo tumefurahi kuwa hapa na kuona vipaji vikipata nafasi ya kuonekana," alisema Rispa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MESSI HUYOOO MAREKANI**

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35, anatarajiwa kufikia makubaliano ya kujiunga na Inter Miami msimu ujao. (***Times***)

**PULISIC AGEUKA LULU EPL**



MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic, mwenye umri wa miaka 24, anafuatiliwa na Manchester United, Newcastle na Arsenal. (***Mail***)

**LIVERPOOL KUSAJILI VIUNGO**

LIVERPOOL wanataka kusajili viungo wawili mwaka ujao huku mikataba ya wachezaji wao watatu wa kati wakubwa - Alex Oxlade-Chamberlain mwenye miaka 29, James Milner, 36, na Naby Keita, 27, - zikikamilika mwishoni mwa msimu. (***Football Insider***)

**LIVERPOOL NA KUNUNULIWA**

LIVERPOOL wamefanya mazungumzo na miungano miwili ya kampuni zenye makao yake Mashariki ya Kati juu ya kuinunua. (***Mail***)

**SANTOS ATAKIWA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle United iko tayari kumnunua kiungo wa kati wa Vasco da Gama, Mbrazil Andrey Santos, mwenye umri wa miaka 18 katika dirisha la usajili la Januari. (***Northern Echo***)

**BECKHAM KUINUNUA UNITED**

RIO Ferdinand amesema mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United, David Beckham "atakuja na muungano wa makampuni" kuinunua klabu hiyo ya Old Trafford. (***FIVE***)

**HINCAPIE ASAKWA CHELSEA**

CHELSEA imekuwa ikimsaka beki wa Ecuador na Bayer Leverkusen, Piero Hincapie mwenye umri wa miaka 20. (***Mirror***)

**WILLIAMS AMULIKWA JUVE**

KLABU ya Juventus inapanga kumsajili mshambuliaji wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye miaka 20. (***AS***)

**OKAFOR CHAGUO LA MILAN**

AC Milan wanataka kumsajili mshambuliaji wa Uswisi, Noah Okafor mwenye umri wa miaka 22 kutoka Red Bull Salzburg. (***Calciomercato***)

**ZIYECH ANUKIA KWA MKOPO**



AC Milan pia wanataka kumnunua kiungo wa Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29 kwa mkopo kutoka Chelsea. (***Gazzetta dello Sport***)

**BALDE MKATABA MPYA**

BARCELONA itampa mkataba mpya wa miaka mitano beki wa kushoto wa Hispania, Alejandro Balde,19. (***Fabrizio Romano***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO ATUMA UJUMBE MZITO KUMFARIJI NEYMAR

●●● Brazil inakupenda, mashabiki wa kweli wale wanaokukubali wanahitaji mabao yako...

**DOHA,** Qatar

NEYMAR lazima awapuuze wale ambao wameshereheka jeraha lake la kifundo cha mguu kwenye Kombe la Dunia na kuzingatia kurejea kwa nguvu, kwa mujibu wa nyota wa Brazil, Ronaldo de Lima.

**Kumekuwa na hisia tofauti kwa Neymar kutoshiriki mchezo wa Brazil dhidi ya Uswisi, na pengine mechi inayofuata dhidi ya Cameroon pia, hata miongoni mwa wafuasi wa 'Selecao' hao.**

Uungwaji mkono wa Neymar kwa mgombea urais wa Brazil, Jair Bolsonaro, ambaye alishindwa na Lula katika uchaguzi mwezi uliopita, kumeonekana kugeuka dhidi ya fowadi huyo wa umri wa miaka 30 wa Paris Saint-Germain.

Ronaldo alikuwa nyota wa timu hiyo iliyofanikiwa kutwaa taji la tano kati ya mataji hayo, huku mabao yake nane kwenye fainali ya mwaka 2002, yakiwamo mawili katika fainali dhidi ya Ujerumani, yakiifanya timu hiyo kutwaa ubingwa.

Alimtaja Neymar kama "mzuri" katika maoni ya wazi kwenye Instagram, Jumapili.

Ronaldo alisema: "Nina uhakika kwamba Wabrazil wengi, kama mimi, wanakustaajabia na kukupenda. Kipaji chako, kwa njia, kimekupeleka mbali, juu sana, kwamba kuna upendo na pongezi kwako katika kila kona ya ulimwengu.

"Na pia ni kwa sababu hii, kwa kuwa umefika hapo ulipo, kwa mafanikio uliyoyapata, unapaswa kukabiliana na husuda na uovu mwingi.

"Katika kiwango cha kusherehekea kuumia kwa nyota kama wewe ni ajabu sana. Tumefikia wapi? Ulimwengu gani huu? Ni ujumbe gani tunawapitishia vijana wetu?

"Siku zote kutakuwa na watu wanaokupinga, lakini inasikitisha kuona jamii ikiwa katika njia ya kupuuza kutovumilia, ya kurekebisha matamshi ya chuki kuwa ya kawaida.

"Ni dhidi ya ukatili huu wa maneno yenye nguvu ya uharibifu ninayokuandikia leo: rudi ukiwa na nguvu zaidi! Nadhifu zaidi! Njaa ya malengo! Mema unayofanya ndani na nje ya uwanja ni makubwa zaidi kuliko wivu kwako.

"Usisahau hata sekunde moja safari iliyokufanya kuwa sanamu ya soka duniani. Brazil inakupenda! Mashabiki wa kweli - wale wanaokukubali - wanahitaji mabao yako, chenga, ujasiri na furaha! Sherehekea upendo unaotoka kwa wengi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 412,
MECHI KALI
IHEFU FC
VERSUS
YOUNG AFRICANS
1 | 6.63
X | 3.71
2 | 1.47
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GAKPO AKATAA KUKANUSHA KUHAMA



**DOHA, Qatar**

CODY Gakpo amesema "chochote kinawezekana" kuhusu mustakabali wake katika Klabu ya PSV Eindhoven baada ya kufanya vema kwa Uholanzi kwenye Kombe la Dunia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga katika mechi mbili za ufunguzi za nchi yake - ushindi wa 2-0 dhidi ya Senegal na katika sare ya 1-1 dhidi ya Ecuador - huku 'Oranje' hao wakiwa kileleni mwa Kundi A wakati wakiwa na mchezo mmoja wa kuhitimisha hatua ya makundi.

Hivi majuzi alifichua kuwa alisikitishwa kwa kukosa kuhamia Manchester United, wakati Liverpool, Real Madrid na Bayern Munich zimekuwa zikihusishwa naye.

Ingawa lengo la Gakpo ni kuisaidia Uholanzi kusonga mbele zaidi katika Kombe la Dunia, hakatai kuondoka PSV dirisha la Januari litakapofunguliwa.

"Kwa sasa nina shughuli nyingi na timu ya Uholanzi. Nitaona kitakachotokea. Katika soka, chochote kinawezekana," alisema katika mkutano na waandishi wa habari Jumapili.

"Sioni aibu kuhusu uvumi. Lakini ni mchezo wa timu, hauhusu mtu mmoja. Napendelea iwe kuhusu timu.

"Ni mambo mazuri ambayo watu huandika, lakini sijali sana na hilo. Sasa ninaangazia Kombe la Dunia. Ninazingatia tu hapa na kufanya bora yangu."

# Neuer: Ujerumani bado ina nafasi

**DOHA, Qatar**

MANUEL Neuer ameonyesha kufarijika kwamba Ujerumani "bado hai" katika Kombe la Dunia baada ya kuokoa sare ya 1-1 na Hispania Jumapili.

Matumaini ya Ujerumani kufuzu hatua ya 16 yalipata pigo la kushangaza walipopoteza mechi yao ya kwanza dhidi ya Japan.

Hata hivyo, Costa Rica ilijibu kichapo cha mabao 7-0 kutoka kwa Hispania kwa kuifunga Japan 1-0 na kuwaacha wote kusubiri hadi watakapocheza mechi za mwisho za Kundi E ili kuamua zitakazosonga mbele.

Alvaro Morata aliiweka Hispania mbele katika mechi kati ya vigogo hao wa Kundi E kwenye Uwanja wa Al Bayt, lakini Mjerumani Niclas Fullkrug aliingia akitokea benchi kusawazisha na kuihakikishia timu yake pointi ya kwanza.

Ili kusonga mbele, timu ya Ujerumani inayonolewa na Hansi Flick, lazima iifunge Costa Rica katika mechi ya mwisho ya kundi siku ya Alhamisi na inatumaini Hispania itawafanyia upendeleo dhidi ya Japan.

Kipa Neuer, ambaye alimnyima Dani Olmo bao la mapema alipopiga shuti lake dhidi ya lango, anafuraha kuona Ujerumani bado ina nafasi ya kukwepa kuondolewa mara ya pili mfululizo kwa Kombe la Dunia katika hatua ya makundi.

"Ilikuwa mechi ngumu dhidi ya timu nzuri sana ya Hispania," alisema nahodha huyo wa Ujerumani.

"Tulipambana na hatukuruhusu nafasi nyingi kwa dakika 90.

"Kazi yetu ya ulinzi ilikuwa nzuri sana kutoka mbele hadi nyuma. Ubabe wetu ulifanya iwe vigumu kwao kufunga bao dhidi yetu. Bao lao lilikuwa la ubora na gumu sana kulilinda dhidi yetu. Hata hivyo, tuliendelea kujiamini.

"Jambo kuu ni kwamba bado tuko hai. Kitu ambacho tunaweza kuwa na ushawishi juu yake ni kupata pointi tatu dhidi ya Costa Rica."



## HABARI MICHEZO


,613,570

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/12/22 | 02:30 | Deportivo Pasto vs Independiente Medellin | 3.01 | 2.92 | 2.35 |
| 02. 01/12/22 | 02:30 | America De Cali vs Rionegro Aguilas | 2.90 | 2.80 | 2.51 |
| 03. 01/12/22 | 04:35 | Independiente Santa Fe vs Millonarios FC | 3.35 | 3.00 | 2.29 |
| 04. 01/12/22 | 11:30 | Sreenidi Deccan FC vs Mohammedan SC | 2.76 | 3.20 | 2.35 |
| 05. 01/12/22 | 14:30 | Meizhou Kejia vs Shanghai Shenhua | 2.38 | 3.26 | 2.68 |
| 06. 01/12/22 | 15:45 | Viseu vs GD Estoril | 2.68 | 3.07 | 2.49 |
| 07. 01/12/22 | 18:00 | Croatia vs Belgium | 2.66 | 3.31 | 2.56 |
| 08. 01/12/22 | 20:00 | Maritimo vs Rio Ave | 2.75 | 3.25 | 2.50 |
| 09. 02/12/22 | 15:45 | Arab Contractors vs Ceramica Cleopatra | 2.60 | 2.75 | 3.05 |
| 10. 02/12/22 | 15:45 | Ismaily SC vs Smouha Club | 2.49 | 2.89 | 3.04 |
| 11. 02/12/22 | 22:00 | Serbia vs Switzerland | 2.55 | 3.19 | 2.75 |
| 12. 02/12/22 | 22:45 | Crewe vs Newport | 2.82 | 3.12 | 2.47 |
| 13. 02/12/22 | 22:45 | Doncaster vs Walsall | 2.63 | 3.13 | 2.63 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 29/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4238 | Artsakh vs Alashkert Martuni | 5.64 | 3.79 | 1.52 |
| 13:00 | 5870 | Turan Tovuz vs Sabah | 6.03 | 4.18 | 1.44 |
| 14:00 | 1312 | SP. Braga U23 vs CS Maritimo U23 | 1.42 | 4.47 | 5.83 |
| 15:00 | 1122 | Alessandria vs Olbia Calcio | 2.32 | 3.01 | 3.26 |
| 15:00 | 2707 | Bkma Yerevan vs Shirak Gyumri | 2.58 | 2.96 | 2.67 |
| 15:30 | 3161 | FK Sumgayit vs Gabala | 2.97 | 2.97 | 2.35 |
| 15:40 | 1998 | Bahla vs AL Etihad | 1.81 | 2.97 | 4.76 |
| 15:40 | 4079 | Al Suwaiq vs AL Musanaa | 1.83 | 3.07 | 4.38 |
| 16:00 | 2599 | ND Gorica vs Tabor Sezana | 2.21 | 3.21 | 2.97 |
| 16:00 | 4061 | Ihefu FC vs Young Africans | 6.63 | 3.71 | 1.47 |
| 16:00 | 5277 | Dire Dawa Kenema FC vs Wolkite City FC | 2.54 | 2.88 | 2.78 |
| 16:30 | 2473 | Kenkre FC vs Neroca FC | 3.50 | 3.36 | 1.94 |
| 17:00 | 1920 | CR Belouizdad vs CS Constantine | 1.58 | 3.65 | 6.20 |
| 17:00 | 2588 | RC Arbaa vs USM Khenchela | 2.14 | 2.78 | 3.65 |
| 17:00 | 3795 | MC Alger vs Paradou AC | 1.46 | 3.56 | 7.41 |
| 17:00 | 4200 | MC Magra vs USM Alger | 3.80 | 2.92 | 2.02 |
| 17:00 | 5157 | ASO Chlef vs El Bayadh | 2.03 | 2.81 | 3.98 |
| 17:00 | 5974 | US Biskra vs JS Kabylie | 2.29 | 2.73 | 3.36 |
| 17:30 | 4256 | Petro Luanda vs Primeiro De Agosto | 1.92 | 2.98 | 4.10 |
| 18:00 | 1571 | Ecuador vs Senegal | 2.41 | 3.15 | 2.95 |
| 18:00 | 4070 | Benfica U23 vs SC Farense U23 | 1.19 | 6.26 | 9.78 |
| 18:00 | 4481 | Netherlands vs Qatar | 1.19 | 6.59 | 12.99 |
| 18:15 | 3001 | Al Seeb vs Al Nahda (Oman) | 2.28 | 3.12 | 2.93 |
| 19:00 | 2019 | Estoril Praia U23 vs Portimonense U23 | 1.57 | 4.19 | 4.48 |
| 19:00 | 2130 | Sidama Bunna SC vs Fasil Kenema | 8.01 | 4.30 | 1.35 |
| 19:30 | 2882 | Pontedera vs Virtus Entella | 3.30 | 2.85 | 2.40 |
| 19:30 | 3710 | Sassari Torres vs Fiorenzuola | 2.09 | 2.96 | 3.96 |
| 19:30 | 5877 | Carrarese vs US Ancona 1905 | 2.33 | 3.04 | 3.19 |
| 20:00 | 2236 | ES Setif vs MC Oran | 1.51 | 3.55 | 6.42 |
| 20:00 | 4082 | Chindia Targoviste vs Universitatea Craiova | 4.05 | 3.11 | 1.96 |
| 20:00 | 5153 | Maribor vs ASK Bravo | 1.86 | 3.50 | 4.10 |
| 20:00 | 5952 | JS Saoura vs HB Chelghoum Laid | 1.09 | 7.42 | 19.53 |
| 21:00 | 3532 | Turkgucu Ataspor Munchen vs SV Heimstetten | 1.43 | 4.47 | 5.64 |
| 21:00 | 4040 | BSG Chemie Leipzig vs Berliner Dynamo | 2.11 | 3.45 | 2.97 |
| 22:00 | 1541 | Wales vs England | 6.90 | 4.20 | 1.46 |
| 22:00 | 4843 | Iran vs USA | 3.84 | 3.35 | 1.96 |
| 23:00 | 1634 | AC Siena vs Fermana FC | 2.60 | 2.95 | 2.90 |
| 23:00 | 2530 | Recanatese vs AC Reggiana | 2.70 | 3.05 | 2.70 |
| 23:00 | 3949 | San Donato Tavarnelle vs Aquila 1902 Montevarchi | 2.58 | 3.03 | 2.83 |
| 23:00 | 3956 | Lucchese vs Cesena | 3.35 | 2.90 | 2.34 |
| 23:00 | 4488 | Vis Pesaro vs Gubbio | 2.48 | 3.10 | 2.90 |
| 23:00 | 4745 | Rimini vs Imolese Calcio | 2.28 | 3.10 | 3.25 |
| 23:45 | 1184 | Santa Clara vs Oliveirense | 1.54 | 3.85 | 5.26 |

JUMATANO - 30/11/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:45 | 1187 | National Bank vs Enppi Club | 2.22 | 2.79 | 3.74 |
| 16:00 | 2209 | Vietnam vs Borussia Dortmund | 7.01 | 5.25 | 1.30 |
| 18:00 | 3437 | Tunisia vs France | 6.40 | 3.90 | 1.52 |
| 18:00 | 5296 | Australia vs Denmark | 6.38 | 4.09 | 1.50 |
| 22:00 | 1224 | Poland vs Argentina | 7.18 | 4.19 | 1.45 |
| 22:00 | 3253 | Saudi Arabia vs Mexico | 4.60 | 4.00 | 1.66 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# TANZANIA YANG'ARA MASHINDANO KUOGELEA KANDA YA TATU AFRIKA

**Na Mwandishi Wetu**

WAOGELEAJI wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wanaume na Wanawake (Tanzanite), wameipeperusha vema bendera ya nchi baada ya kushinda mashindano ya Kanda ya Tatu Afrika yaliyofanyika hivi karibuni kwenye Bwawa la Klabu ya Dar es Salaam Gymkhana.

Katika mashindano hayo yaliyoshirikisha jumla ya nchi 10, waogeleaji wa Tanzania walikusanya jumla ya pointi 3,061 na kuzishinda nchi tisa katika mashindano hayo yaliyokuwa na ushindani mkubwa na kusisimua.

Tanzania ambayo iliwakilishwa na waogeleaji 63 pia ilikuwa nchi pekee iliyoshinda medali nyingi kuliko nchi zote zilizoshiriki katika mashindano hayo baada ya kuibuka na jumla ya medali 110.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotolewa na chama cha mchezo huo cha Kanda ya Tatu Afrika, nafasi ya pili ilikwenda kwa Kenya ambayo ilijikusanyia pointi 2,768 na kufuatiwa na Uganda iliyojikusanyia pointi 2,521.50 na Zambia katika nafasi ya nne kwa kukusanya pointi 1,878.

Afrika Kusini ilishika nafasi ya tano kwa kupata pointi 1,385. 50 ambapo Burundi ilishika nafasi ya sita kwa kupata pointi 653 na Sudan Kusini ikimaliza katika nafasi ya saba kwa kupata pointi 213. Nchi za Djibouti (pointi 87), Rwanda (pointi 67) na Ethiopia iliyopata pointi 47 zilimaliza katika nafasi ya nane, tisa na 10 katika mashindano hayo yaliyodhaminiwa na Kilombero Sugar Company kupitia Bwana Sukari.

Wadhamini wengine ni JustFit, Kahawa Café, Spark rehabilitation, Gymkhana Club, International School of Tanganyika, FK International school, Hopac Hawks, Pepsi, Travelport, Azam, Stanmag Logistics, Wood Lab Décor, Burger 53, F&L Juice, G1 Security, Leo Club of Tanzania District 411C, Suraksha Team, Pyramid consumers, Four Points by Sheraron, Crown Hotel, Aura Suites na Protea Hotel Mariot- Courtyard.

Kwa upande wa medali, Tanzania ilikusanya jumla ya medali za dhahabu 38, Fedha 38 na Shaba 34 ikifuatiwa na Kenya ambayo ilipata jumla ya medali 108 ambapo 46 ni dhahabu, Fedha 32 na Shaba 30.

Uganda ilipata jumla ya medali 85 ambapo 28 zilikuwa za dhahabu, 25 fedha na shaba 32 na Zambia ilipata jumla ya medali 56, 22 (dhahabu), 21 (fedha) na 13 shaba.




Waogeleaji wa Tanzania na viongozi mbalimbali wakishangilia baada ya kutwaa ubingwa wa Kanda ya Tatu Afrika hivi karibuni. **MPIGAPICHA WETU**

## Pablo aishuhudia Azam, yafunguka

INATOKA UK. 32

kwa kuweka viti uwanjani ili kuwapo kwa uwezo wa kuingiza mashabiki elfu 10 hadi 12, kwa kufuata kanuni za Shirikisho la Soka Afrika," alisema Mhandisi.

## MGUNDA ATEMA CHECHE LIGI KUU

INATOKA UK. 32

bia mwenzake, Clatous Chama ambaye alitoa 'assist' mbili kwenye mechi hiyo.

"Lengo letu lipo pale pale, ni ubingwa, ushirikiano wangu na Chama, pamoja na wachezaji wengine utatufanya kuweza kuwa mabingwa msimu huu na sina cha kusema kuhusu Chama nadhani wenyewe mnaona, niseme machache tu kuwa ni mmoja wa wachezaji bora sana.

"Binafsi nitajitahidi kufanya mazoezi kwa bidii ili niweze kufunga mabao na kuwafurahisha mashabiki, tena kwenye viwanja vyote si Benjamin Mkapa tu," alisema Phiri mwenye mabao nane hadi sasa ikiwa ni mawili nyuma ya kinara wa ufungaji, Fiston Mayele wa Yanga.

Kocha wa Polisi Tanzania, John Tamba, alisema makosa madogo madogo ya wachezaji wake ndiyo yaliyosababisha Simba kupata ushindi kwani ina wachezaji bora na wenye uzoefu, huku akili yake akiiweka kwenye dirisha dogo kwa ajili ya kupata wachezaji watakaokiongezea nguvu kikosi chake.

# Michezo

Jumanne Novemba 29, 2022

Nipashe



UKURASA 29

## Ronaldo atuma ujumbe mzito kumfariji Neymar

NIMECHOMOA...



Mshambuliaji wa Cameroon, Jean-Eric Maxim Choupo-Moting, akishangilia baada ya kuisawazishia timu yake bao la tatu huku Kipa wa Serbia, Vanja Milinkovic-Savic na beki wake wa kati, Miloš Veljkovic wakiishia kushangaa mpira ukizama nyavuni, kwenye mechi ya Kundi G ya Kombe la Dunia iliyopigwa Qatar jana. **PICHA: MTANDAO**

# MGUNDA ATEMA CHECHE LIGI KUU

●●●Ashangaa wanaolia na ratiba, asema sasa ni zamu ya Coastal kuchezea, Phiri naye aapa...

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amewapongeza wachezaji wake kwa kujituma na kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Polisi Tanzania, akisema haukuwa rahisi, na kazi iliyoko ni kuendelea kuwapa furaha wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwenda kuifunga Coastal Union mechi itakayopigwa Jumamosi ijayo Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Akizungumza baada ya kikosi hicho kutua jijini Dar es Salaam jana kikitokea Moshi mkoani Kilimanjaro ambako kiliichapa Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika, Mgunda alisema haikuwa kazi nyepesi kwa sababu walicheza na timu ambayo ilikuwa na dhamira ya kupata pointi tatu au moja ili kujinanua iliko

"Nawapongeza vijana wangu kwa kuweza kupambana na kupata ushindi, haikuwa mechi nyepesi, tulicheza na timu ambayo ilikuwa inataka kujinasua kutoka huko iliko kwa hiyo ilikuwa ni mechi yenye ushindani mkubwa. Na kubwa niwashukuru wachezaji wangu wa 12 ambao ni wanachama na mashabiki," alisema kocha huyo.

Alisema baada ya kuumaliza mchezo huo hawana muda wa kupoteza, badala yake wanafanya maandalizi ya kwenda kuivaa Coastal Union ambapo azma yao ni kutaka kuendelea kuwafanya wanachama na mashabiki wa Simba waendelee kuwa na furaha.

"Mechi imekwisha, maandalizi yameanza ya mechi inayokuja, tunawaheshimu Coastal Union ni timu nzuri, lakini sisi tunataka ushindi. Sisi hatuwezi kulalamikia ratiba eti tunacheza mechi nyingi ugenini, tunaiheshimu kwa sababu nini ratiba ambayo ni lazima tucheze na hizo timu tulizopangiwa," aliongeza.

Alisema beki wa kushoto Mohamed Hussein 'Tshabalala' hakucheza mechi ya juzi kwa sababu ni majeruhi, lakini anaendelea vizuri ingawa kwenye mechi dhidi ya Polisi Tanzania madaktari walishauri asichezeshwe.

Naye straika Moses Phiri aliyefunga mabao mawili kwenye mchezo huo, alisema anakwenda kuongeza mazoezi na ubunifu ili aweze kufunga mabao mengi zaidi kwa ajili ya kuwafurahisha wanachama na mashabiki wa Simba, huku akimsifu Mzam-

INAENDELEA UK. 31

## Pablo aishuhudia Azam, yafunguka

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umesema mchakato wa kutafuta Kocha Mkuu umesimama na jukumu hilo la kukinoa kikosi chao linaendelea kubaki chini ya Kocha wao wa Washambuliaji, Kalimangonga Ongala.

Kauli hiyo imetolewa na Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', baada ya tetesi kwamba uongozi uko kwenye mazungumzo na aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Mhispania Pablo Franco, ambaye yuko nchini na juzi alikuwapo Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam akishuhudia mechi ya timu hiyo dhidi ya Coastal Union.

Pablo ambaye anadaiwa kuwapo nchini kwa ajili ya kukamilisha dili hilo na Azam FC, aliishuhudia timu hiyo ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2.

Akizungumza na gazeti hili jana, Popat alisema timu itabaki kunolewa na Kali kwa sababu wanaimani na kocha huyo baada ya kufanya vizuri katika michezo saba waliocheza na kushinda.

Alisema makocha waliopo ndani ya timu hiyo wataendelea kubaki hadi mwishoni mwa msimu kwa sababu wanaimani nao kwa timu kufanya vizuri katika michezo ijayo.

"Mchakato wa kutafuta kocha mkuu tumesitisha na tunaendelea kubaki na waliokuwapo, lakini suala la Pablo kuwapo uwanjani alikuja kwa ajili ya kuangalia mechi yetu," alisema Popat.

Alisema kocha huyo yuko nchini kwa ajili ya mambo yake na alikuwapo katika Uwanja wa Azam Complex kwa ajili ya kufuatilia mechi na hakuna jambo lingine.

Wakati huo huo Muhandisi wa Uwanja wa Azam Complex, Victor Ndozero, alisema hakuna ukweli kwamba uwanja huo ni mdogo bali una vipimo sawa na Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Alisema kuonekana udogo kwa uwanja huo ni kwa sababu ya majukwaa yako karibu na wanatarajia kufanyia ukarabati katika eneo la kukaa mashabiki.

"Tuko katika mchakato wa kubadilisha eneo la mashabiki

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >